Kikao cha Kumi – Tarehe 24 Machi, 2015

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha mezani, hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza, yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Maliasili, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza, yaliyotokiana na ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ya mwaka 2013/2014.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza, yaliyotokana na ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kwa niaba ya Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani kuhusu hotuba ya kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 29

Mazingira ya Kambi za Zimamoto Pemba

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Kwa kuwa kikosi cha Zimamoto ni miongoni mwa vikosi muhimu ya SMZ, na kwa kuwa kambi ya Zimamoto Pemba mazingira yake hayaridhishi hata kidogo.

Je, ni lini Serikali itawaandalia wafanyakazi wa kambi hiyo makaazi salama na yenye kuridhisha kwa maisha yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli makambi yetu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, hayajafikia ubora unaohitajika hasa katika maeneo yaliyowekwa vituo hivi karibuni. Hii inatokana na fedha zinazotengwa kuwa na mahitaji mengi ikiwemo kuhudumia vifaa vya kuzimia moto. Hata hivyo, jitihada zinaendelea ili kuziimarisha kambi hizo kadri hali itakavyoruruhusu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

(a) Mhe. Spika, kwanza nilitaka kujua kile kituo cha Zimamoto pale Wete walipo, wako katika eneo la Ofisi ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ au wako katika eneo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

(b) Je, kwa kuwa wizara ina mipango ya kuwajengea mazingira mazuri, na kwa kuwa wanaoishi pale mazingira yao ni hatarishi hata kwa afya zao, wizara haioni kuna haja ya kutafuta hali ya dharura ya kuwatengenezea ofisi, angalau ukarabati mdogo wakati tunajiandaa na lile kubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, eneo la kituo cha Zimamoto liliopo Mjini Wete, sio eneo linalomilikiwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali, linalomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Tulifanya mazungumzo kati yetu na uongozi wa mkoa na uongozi wa wizara wakatuazima kwa muda. Hata hivyo, serikali inaangalia uwezekano wa kuweza kufanya mazungumzo zaidi kati ya wizara hizi mbili; Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wizara yetu ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kupitia Wizara ya Fedha, ili kuona umuhimu wa jengo lile kutumika kwa ajili ya shughuli za Zimamoto na Uokozi katika kituo cha Wete.

Tuna mpango gani wa dharura. Mhe. Spika, lile tulilolifanya sasa hivi ndio mpango wa dharura, kwamba kulikuwa hakuna kituo na mahitaji yanahitajika, tukaamua kuazima eneo lile pale. Kwa hivyo, ule ulikuwa ni mpango wa dharura.

Tunajiandaa katika kuandaa mpango wa kudumu wa kuweza kuhakikisha kwamba Kituo cha Zimamoto kinakuwepo cha kudumu na kuimarisha makambi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati anajibu swali lake la mwisho alisema kwamba wana mpango wa kuweka miundombinu mipya kwa ajili ya Vikosi vya Zimamoto. Je, mpango huo utafanyika lini na utafanyika katika sehemu gani?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, mpango huo utafanyika baada tu ya serikali kuwa na uwezo wa kuweza kukiwezesha Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, kujenga maeneo madhubuti kabisa kwa ajili ya shughuli zao. Pia utafanyika katika yale maeneo ambayo tumemilikishwa viwanja kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kikosi hiki cha Zimamoto ni miongoni mwa vikosi vyetu na ni kikosi muhimu sana kulingana na shughuli zake. Viko vingine ambavyo viko mwahala muhimu kama *Airport* kule Pemba, lakini makaazi yao hayaridhishi.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwafanyia askari wetu hawa wapate pahala pazuri pa kukaa na kufanyakazi zao vizuri?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, suala hili la kutokuridhisha makaazi ya askari nimekuwa nikilijibu mara kwa mara hapa, na bado naendelea kusema pale serikali itakapokuwa na uwezo wa kutosha basi makaazi haya yataimarishwa, kwa sababu sisi tungependa vituo vyetu vyote viwe katika hali nzuri kama vilivyo vituo vyengine vya Zimamoto duniani. Ahsante sana.

Kero ya Maji Machafu Eneo la Mchina Mwanzo

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutuondolea kero ya maji machafu kwa Mchina Mwanzo.

(a) Je, ni lini mtaro uliochimbwa kutoka Mchina Mwanzo kuelekea Mpendae utamalizwa.

(b) Kwa kiasi gani Serikali imezingatia uharibifu unaowapata wananchi wa Mpendae.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mtaro uliochimbwa na Idara ya *UUB,* yaani Ujenzi wa Barabara, kutoka kwa Mchina Mwanzo kuelekea Mpendae, ni mtaro wa maji ya mvua ambao unategemewa kumalizwa, baada ya kukamilika ujenzi wa mtaro mkubwa wa kuchukua maji ya mvua chini ya Mradi wa *ZUSP,* ambao unatarajiwa kujengwa kutoka Magomeni kwa Makada hadi Mpendae.

(b) Mhe. Spika, athari kubwa inayowakibili watu wa Mpendae ni mafuriko katika eneo hilo wakati wa msimu wa mvua kubwa na kusababisha baadhi ya nyumba kujaa maji na wengine kuhama makaazi yao kwa muda. Serikali inakusudia kuzipunguza athari hizo kwa kujenga mtaro mkubwa wa kupitishia maji ya mvua kutoka Magomeni kwa Makada, pamoja na ziwa la kwa Binti Hamrani hadi Kilimani na hatimaye baharini chini ya Mradi wa Huduma Mijini (*ZUSP*).

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kabla ya kujengwa mtaro huu maji yalikuwa yakisambaa maeneo mbali mbali, lakini baada ya kujengwa mtaro huu umesababisha maji mengi ku-*flow* kwa nguvu katika lile bwawa na kuleta athari kubwa. Ikiwa ile dhamira ya serikali ya kujenga mtaro mkubwa kutoka kwenye bwawa kupeleka baharini imechukua muda mrefu.

(a) Je, wizara yako haioni kwamba kucheleweshe mradi huu unapelekea kuhatarisha usalama wa wananchi wa eneo lile kwa kasi?

(b) Je, wizara ina jitihada gani za kuwasaidia watu wale ambao wanapata maafa ya mafuriko katika kipindi hicho?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka niwahakikishie wananchi kwamba sio nia ya serikali au taasisi ya serikali kujenga mtaro ule kupitia Idara ya Barabara kwa ajili ya kuwasumbua wananchi. Nia ilikuwa ni kuihami barabara ambayo ilikuwa inaelekea kuharibika mara kwa mara kutokana na kutuama kwa maji ya mvua.

Hata hivyo, serikali hivi sasa kama nilivyosema kwenye masuala ya wiki iliyopita, kwamba hivi karibuni tu Mkandarasi wa kujenga mitaro kupitia mradi wa *ZUSP*, atateuliwa na kazi hiyo itaanza mara moja.

Serikali inawasaidiaje wananchi wanaopata maafa? Nadhani utaratibu wa kiserikali upo ambao umewekwa, kwa pale serikali itakapoona kwamba wananchi hao wamepatwa na matatizo ya kuweza kuingizwa katika utaratibu wa maafa, basi wizara inayohusika ipo na Masheha na uongozi wa maeneo

hayo na wananchi kwa jumla wafike kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ili waweze kuhudumiwa kwa kupitia utaratibu huo wa watu wanaopatwa na maafa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wananchi wa Mpendae hawaathiriwi na maji, lakini wanaathiriwa mpaka na miundombinu mibovu ya barabara, na kwa kuwa dhamana wa kutengeneza barabara katika mtaa ule ni Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.

Je, Wizara yake kwa kupitia Halmashauri ya Magharibi ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba miundombinu ya watu wa Mpendae inaboreshwa?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka nitoe masahihisho kwamba Mpendae haiko katika Wilaya ya Magharibi, iko katika Wilaya ya Mjini. Kwa hivyo, wanaohusika na suala hilo ni Baraza la Manispaa, kwa mujibu wa utaratibu wetu. *(Makofi)*

Lakini serikali inajiandaaje katika kuboresha au kuimarisha miundombinu ya barabara za ndani ambazo zinasimamiwa na Mabaraza ya Miji na Halmashauri. Ndio maana tumeleta sheria, ile sheria ambayo tuliileta kwa dharura, baadhi ya Wawakilishi wakahoji kwa nini inakuja kwa dharura. Lengo lake lilikuwa ni kuwahi bajeti ya mwaka huu, 2015/2016, ili taratibu za kisheria zifanywe za kuweza kuweka utaratibu maalum wa kuweka ada za kuchangia Halmashauri, ili Halmashauri ziweze kupata uwezo wa kuweza kutengeneza barabara hizo kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara, pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Nam. 41

Matengenezo ya "*Lift*" Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu hili namba 41, naomba uniruhusu kwa dakika moja nimshukuru Dkt. Mwinyihaji Makame kwa jitihada alizochukua kwa kipindi kile kuweka *lift* mpya.

Nimshukuru sana. Mhe. Spika, vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake aliyoitoa jana Kisiwani Pemba huko, kwamba madaktari kutoka Pemba kurudi Unguja kwa hivi sasa basi na sisi tunahitaji matibabu *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, kusimama kwa mguu mmoja ni tabu. Naomba serikali itoe jawabu la swali la wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba, nambari 41.

Kwa muda mrefu sasa "*lifti*" ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa mbovu na inahitaji matengenezo.

Je, ni lini "*lifti*" hiyo itatengenezwa kwa kuwa muda mrefu sasa imekuwa mbovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 41 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa kuna *lift* mbili, ambapo moja ni nzima na inafanya kazi ndio hizo shukurani alizotoa Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub kwa Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame wakati ule wa *MDRI* ambazo fedha zake zimetumika kutengeneza hiyo *lift* ambayo inafanya kazi hivi sasa.

Na ya pili Mhe. Spika, ni mbovu na ni mbovu kwa kipindi kirefu sana na hiyo haifai kabisa, hivyo mafundi wa kampuni ya *OTIS* kutoka Tanzania Bara walikuja kutushauri kwamba kufanyiwa matengenezo *lift* hiyo matengenezo yake yatakuwa makubwa sana. Kwa hivyo ni vyema kubadilisha mfumo mzima wa *lift* hiyo na kuweka mfumo mpya wa *lift* ya kisasa, matengenezo hayo Mhe. Spika, yatafanyika mara tu tutakapopata fedha. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, kwa siku hii ya leo naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Suala la pili ningeiomba Serikali nafikiri Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alikuwa hayupo kipindi kirefu sana atasema kwa niaba ya Serikali kujibu suala hilo.

(1) Lini Serikali itafikiria kuwa na *lift* zaidi ya moja, kwa sababu wananchi wengi wakiwemo walemavu wa viungo ndio wanaoteseka katika hospitali ile, kusimama kwa mguu mmoja ndio pale inakuwa tabu kuliko kuwa na miguu miwili.

(2) *Lift* inakuwa na huduma zake unavyokabidhiwa kwenye kiwanda kama miaka mingapi inafanya kazi na muda gani wa kufanya kazi, *lift* katika kutoa huduma zake inapewa mkataba wake maalum kama miaka miwili au mitatu au minne katika kutumikia *lift* ile na chombo chenyewe ni kimoja, na *lift* kwa hesabu ninayofanya mimi inahitaji kama dola elfu hamsini mpaka sabini. Hili ningemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ikatoa jawabu hili Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa upande wako nitakuwa nimekuonea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nitaanza na kifungu (b)

(b) Wale wanaotengeneza *lift* huwa maisha ya *lift* huwa kati ya miaka saba au tisa ambapo matengenezo makubwa yanatakiwa yafanywe baada ya hapo. Lakini wakati huo huo huwa wanapewa na kitu kinaitwa Mkataba wa kufanyia ukarabati au matengenezo kwa kila mwaka ambapo hufanyika *greasing* na zile kama waya zinaonekana zimechakaa na kubadilishwa. Kwa hiyo, yakifanyika *maintenance* hayo yote, *lift* hizo huweza kuchukua zaidi ya muda wa miaka kumi.

Kuhusu swali lake la mwanzo kabisa naomba nirudie tena Mhe. Spika, kwamba jumla ya fedha zinazotakiwa kwa lift hiyo kubadilishwa zote ni jumla ya dola elfu thamanini za kimarekani ambazo ndio *quotation* tulipokea kutoka kwa kampuni ya *OTIS* kutoka Tanzania Bara kubadilisha mfumo mzima. Naelewa *lift* kwa kawaida huwa baina ya dola lefu hamsini mpaka sitini elfu lakini kwa sababu inabadilishwa na mifumo ndani ya reli zile zinazopitisha waya zake na bahati nzuri nilibahatika kufika hapo na kweli ile *lift* ni ya zamani sana.

Kwa hiyo, kauli za serikali ni hiyo hiyo, mara zitakapopatikana fedha hizi maani Wizara ya Fedha wanalijua suala hili tushafanya mawasiliano nayo tutakapopata fedha hizi tu basi tutaingia kwenye mkataba huo mwengine wa kubadilisha *lift* hiyo. Kwa hivi sasa *lift* hiyo inafanya kazi inatosheleza ni kweli tumesimama kwenye mguu mmoja, lakini huo mguu mmoja tumesimama imara hatuyumbi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, lazima tukiri kwamba tatizo la *lift* limekuwa ni usumbufu na mara nyingi inapelekea *lift* ile kusimama njiani na kuleta bughudha kwa wananchi na Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu ametaka *estimate* ya gharama ya elfu thamanini ambazo zinahitajika kwa *lift*.

Je, tatizo ni nini, ni pesa au tatizo ni utendaji au ufuatiliaji wa suala hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tatizo sio ufuatiliaji wala utendaji, tatizo ni fedha. Mara tu zitakapopatikana hizi fedha basi hili suala la *lift* ya pili litaweza kutatuliwa. Kuna mawasiliano kadhaa ambayo tumeshafanya Wizara ya Fedha, kwa hiyo utendaji hapo umekwenda vizuri na *correspondence* nzuri ya barua mbali mbali kwenda Wizara ya Fedha kulikumbushia jambo hilo na sisi tupo katika *waiting list,* mara tu fedha zitakapopatikana huwa tunatiliwa kwa Mnazi Mmoja.

Lakini fedha zote zinazotiliwa sasa kwa pale Mnazi Mmoja kunatumika katika uendeshaji wa Hospitali Kuu ambazo pia nazo wakati mwengine huwa tuna *deficit* ndogo hazitoshelezi.

Kwa hiyo, fungu hili ni tafauti na fungu lile la mara moja ambalo litahitajika kulipwa kampuni, kwa hiyo, ni suala lile lile ufanisi upo na utendaji upo mzuri kupata fedha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:

(a) Mhe. Spika, *lift* hii ya Mnazi Mmoja tangu kuharabika kwake.

(b) Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba hii *lift* iliyopo ya mguu mmoja ni tatizo kwa wagonjwa ambao hawawezi kutembea kwa miguu pamoja na wale walemavu ambao hawawezi kupanda kwenda kufanyiwa shughuli zao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nitaanza na kifungu (b)

(b) *Lift* hii ina wafanyakazi sasa hivi inaendelea vizuri na jana mimi mwenyewe nilifika pale tena kuiangalia kwa sababu nilikuwa najua leo swali hili nitalijibu, nimepanda *lift* hiyo inafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, hakuna tatizo lolote kwa walemavu wala wagonjwa mahututi wanaopelekwa juu kule *theater* na maeneo mengine. Naamini kamati wakati inatembelea chini ya Mhe. Mgeni Hassan Juma walitembelea pia eneo hilo. Kwa hiyo, *lift* hiyo moja hivi sasa inafanya kazi, hofu iko pale itakapoharibika hii ndio huo mguu moja aliousema Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Lakini mpaka sasa *lift* hii pia tuna mkataba wa kuifanyia *maintenance* chini ya fungu lile la *MDRI, maintenance* inaendelea kufanyiwa kila mwaka kuna *major maintenance* na kila baada ya miezi mitatu huwa inafanyiwa *maintenance* ndogo ndogo za kawaida kama kuitia *greasing* na mambo mengine. Kwa hiyo, hofu hiyo ndio maana tunataka *lift* hii ya pili itengenezwe.

(a) Naweza kusema ile *lift* iliyoko pale ni ya zamani sana. Nadhani suala ingekuwa imetumika kwa muda wa miaka mingapi. Nasema imevunja rikodi, imetumika zaidi ya miaka 20 *lift* ile iliyoko pale mara ya mwanzo. Kwa hiyo, siwezi kusema kuwa iko kwenye kazi kwa muda gani kwa sababu ilianza kuacha kufanya kazi, inafanya inaacha tena kwa sababu muda wake umeshapitiliza. Kwa hiyo, imevunja rikodi kwa kufanya kazi na ule muda ambao umekusudiwa maisha yake ile *lift* ulipitiliza kwa sababu ilifanya kazi zaidi ya miaka 20. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 64

Wakulima wa Mikarafuu kupatiwa Utaalamu

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:– Aliuliza**:-**

Kama tunavyofahamu uchumi mkuu wa Zanzibar ni karafuu na hivi sasa tukiangalia miti mingi ya mikarafuu imeshapotea na zao la karafuu linashuka bei haidhuru inaonekana vitalu vingi vinavyooteshwa miche ya mikarafuu.

Je, Serikali inaeleza nini kuhusu wakulima wa karafuu hawapatiwi utaalamu katika kukuza na kuendeleza upatikanaji wa miche ya mikarafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 64 kama ifuatavyo:-

Kwa kupokea agizo la Rais la kuhakikisha zao la Karafuu linapewa umuhimu unaostahiki kama zao kuu la biashara ambalo linaipatia fedha za kigeni nchi yetu na ni tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar. Wizara ya Kilimo na Maliasili inatekeleza agizo hilo kwa kuzalisha miche ya mikarafuu na kuitoa bure kwa wakulima. Pia Wizara imewashajihisha na kuwasimamia wakulima binafsi wa karafuu kuanzisha vitalu vyao kwa ajili ya kuzalisha miche ili kukidhi mahitaji yao na ile ya ziada kuwauzia wakulima wenzao kwa bei ndogo.

Pamoja na kuwashajihisha wakulima Wizara pia imekuwa ikiwapatia mafunzo wakulima hao juu ya namna ya uzalishaji wa miche bora ya mikarafuu na pia uanzishaji wa skuli za wakulima katika maeneo mbali mbali ya visiwa jambo ambalo limesaidia sana uzalishaji bora wa miche hiyo hapa nchini.

Hali hii imetokana na ukweli kwamba wakulima wa karafuu wameamka na kuona fursa ya wao kujitoa katika dimbwi la umasikini kwa kulifufua zao hili. Ndio maana mahitaji ya miche yamekuwa makubwa kuliko uwezo wa Serikali kuwapatia miche hiyo bila ya malipo. Hayo yanafanyika kwa makusudi mazima ya kulifufua zao hilo.

Mhe. Spika, Sensa ya miti iliyofanyika mwaka 2013 inaonesha kwamba zaidi ya asilimia hamsini (50% +) ya mikarafuu yote iliyopo Zanzibar ni umri wa kati ya miaka miwili hadi sita. Takwimu hizi zinaashiria kwamba katika kipindi kisichozidi miaka mitano uzalishaji wa karafuu Zanzibar unaweza kuongozeka kwa zaidi ya asilimia mia moja, kwa maana ya kwamba ni kutoka wastani wa tani elfu tano za hivi sasa hadi elfu kumi.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, hizo skuli za wakulima wanazofundishwa wapandaji wa miche ziko maeneo gani tunazozijua ni *nursery* za serikali tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, skuli za wakulima ambazo wanafundishwa uoteshaji wa miche kwa hapa Unguja pana skuli nane, kuna skuli Kitope, Donge Vijibweni, Donge Karange, Koani, Mwakaje, Kwampani na Kiboje ninazozifahamu kwa ufahamu wangu kwa hapa Unguja ni hizo. Lakini kwa Pemba kuna Mkoani ziko tatu, Chake chake ziko nne, Wete ziko tatu na Micheweni ziko mbili.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, kwa kuwa jibu lake alisema mahitaji ya miche yamekuwa makubwa kuliko uwezo wa serikali kutoa miche hiyo. Je, Mhe. Naibu Waziri mahitaji halisi ni kiasi gani ya miche ambayo inatosha kwa mwaka huu na hivi sasa iko miche mingapi kwa msimu huu wa masika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika,mahitaji halisi ni miche milioni moja kwa mwaka. Miche milioni moja kama itahudumiwa kisawa sawa basi inatutosha kwa sababu miche milioni moja ina wastani wa kuotesha eka ishirini na tano elfu. Lakini hivi sasa kwa msimu huu wa masika ambao tayari sasa hivi tuko katika kipindi cha kutoa miche hiyo, tuna miche ambayo haipungui kunako laki tisa thamanini na moja elfu na mia nane sabini na mbili.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwa kuwa hivi sasa ni wakati muafaka wa kutoa miche ya mikarafuu, na kwa kuwa mara nyingi wananchi wanalalamika kuwa miche hiyo haipatikani na hiyo kidogo inayopatikana huwa inapatikana msimu wa mvua umeshamalizika.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika wa utoaji wa miche hiyo.

(b) Je, wizara imejipanga vipi kuotesha miche mingi ya kutosheleza ili kuondosha uhaba wa miche hiyo hasa Mhe. Spika, ukizingatia hesabu ni ndogo tu iliyotafautiana ya Mhe. Waziri aliyotwambia itatosheleza.

(c) Kuna taarifa miche mingi inayooteshwa inakufa, je, ni sababu zipi zinazosababisha miche hiyo kufa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:

(a) Mhe. Spika, mfumo ambao tuliojipangia kutoa miche hiyo tulikuwa mfumo wetu tuna Maafisa wa Kilimo wa Wilaya na Maafisa wa Misitu wa Wilaya. Miche hiyo hupelekwa kwa Masheha kwa kushirikiana na Maafisa hawa ili kusambazwa miche hiyo kwa wananchi, lakini hivi juzi tu tulitoa barua kwa Wakuu wa Wilaya tumewapelekea barua ili watupe utaratibu mzima jinsi ya kugawa miche hii kwa sababu wakati ndio huu. Lakini hadi leo hatujapata jawabu lolote, kwa hivyo tunawasubiri endapo wakatapotuteremshia basi sisi tutakaa pamoja tuone mfumo ambao wa kutoa. Ikiwa hawakututeremshia tutatumia mfumo ule ule ambao tuliotokana nao.

(b) Kuna suala la sababu za kufa miche hiyo kwamba inaoteshwa miche mingi halafu inakufa. Mhe. Spika, kwanza tuchukulie kwamba kila kilicho hai kitakufa, lakini na hivyo vifo vina sababu yake. Kwanza miche hii inapotolewa chini ya umri wa miezi 18 basi mche huo una *risk* kwenda kuupanda wewe, lazima ifike umri wa miezi 18.

Miche inapotolewa wakulima wengi wanakuwa hawaishughulikii, wakishaiweka kwenye ardhi wanaona kwamba wameshaiweka wanamwachia Mwenyezi Mungu. Lakini miche ya mikarafuu inataka huduma hasa hasa wakati wa kiangazi wakati wa jua kali pale ndio inapopotea miche mingi inapotolewa na watu wengi inakuwa inawashinda kuhudumia, hizo ni sababu ambazo zinasababisha miche hii kufa kwa wingi.

Mhe. Spika, hili jengine naomba arejee kidogo.

Mhe. Spika: Mheshimwia Mjumbe hebu rejea swali lako la "c".

Mhe. Salma Mohammed Ali: Je, serikali imejipanga vipi kuotesha miche mingi ya kutosheleza kwa kuondoa usumbufu uliopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:

(c) Suala la kujipanga kuotesha miche mingi ambayo itatosha. Hili ni suala kama nilivyosema kwamba miche ambayo itatukidhia haja ni miche milioni moja kwa mashamba yetu tuliyonayo ili kufanikisha katika uzalishaji huu wa miche ya mikarafuu. Kwa hiyo, kwa suala hili tumejipanga kuhamasisha vitalu vyetu ambavyo vinavyooteshwa na watu binafsi na kuzidi kuwasomesha wakulima wetu ili kufikia idadi hii tuweze kutosheleza. Lakini kama tunavyojua kila siku watu wanahamasika kwa kuwa zao letu limepanda chati na wakulima nao wanaongezeka.

Nam. 51

Uchakavu wa Majengo ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi karibuni katika Mji Mkongwe wa Zanzibar majumba mawili yameanguka kwa nyakati tofauti kutokana na kukabiliwa na uchakavu wa muda mrefu.

a) Je, serikali imejifundisha nini na imechukua hatua gani kwa usalama wa wananchi wetu wanaoishi katika majengo yanayokabiliwa na uchakavu.

b) Kwa kuwa majengo mengi yanahatarisha usalama wa wananchi na uwezo wa kuyakarabati ni mdogo, kwa nini serikali isiyauze majengo hayo kwa watu wenye uwezo waweze kuyajenga na fedha zake kuingizwa katika Shirika jipya la Nyumba la Zanzibar.

c) Ni nyumba ngapi zinazomilikiwa na Serikali ambazo zinakabiliwa na uchakavu wa majengo yake katika Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 51 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kila tukio ni somo kwa serikali, na serikali huchukua tahadhari ya hali ya juu kwa kutafuta namna ya kuliepuka ili lisiweze kujitokeza tatizo.

Mhe. Spika, serikali kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe inaendeleza hatua ya kuyakagua majengo yote ya Mji Mkongwe kama utaratibu wake wa kawaida kutokana na hali ya majengo ilivyo. Pia katika ukaguzi mamlaka inawaita wananchi husika kufanya mazungumzo nao na kuwaelimisha vya kufanya ili majengo wanayoyatumia yasizidi kuathirika na hususan katika kipindi hichi cha mvua.

Mhe. Spika, ni kweli kuna majengo ambayo yapo katika hali mbaya na yanahatarisha usalama wa wananchi na mali zao. Ni juu ya serikali kushirikiana na wamiliki ambao hawana uwezo wa kuyakarabati majengo hayo wawatake wapangaji wao wahame.

Mhe. Spika, nyumba ambazo zinamilikiwa na serikali ambazo zipo katika hali ya uchakavu ni nyumba 27 ambazo zipo chini ya Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa amekiri katika swali la msingi nililoliuliza kuna nyumba chakavu ambazo zinahatarisha usalama wa watu na mali zao.

a) Je, ni lini serikali itakamilisha nyumba hizo kuzifanyia matengenezo au tunaendelea ule msemo tumsubiri mdudu mbaya yule UNESCO tulomtaja jana hapa kwa kulizuia soko lilokuwa linataka kujengwa kule bandarini Malindi.

b) Kwa kuwa Baraza hili si muda mrefu tumepitisha sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba, hizo nyumba zilizokuwa katika hali mbaya kwa nini serikali haiziuzi angalau tukapata kuwa na mtaji kule Shirika la Nyumba baada ya kuwa haina mtaji na kuna nyumba nyengine watu wanadai nyumba zao hawataki kupewa. Ni lini serikali itafikiria hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika,

a) Lengo la serikali ni kuzifanyia ukarabati nyumba hizi, lakini vile vile serikali inaangalia hali ya upatikanaji wa fedha. Kwa hivyo hali ya upatikanaji wa fedha utakaporuhusu basi tutazifanyia ukarabati nyumba hizo.

b) Mhe. Naibu Spika, nyumba za watu binafsi hizo hazimo katika umiliki wa serikali. Kwa hiyo pindi watu binafsi watakaposhindwa basi katika suala la mauzo wao wataangalia katika hali ya kufanya hivyo.

Vile vile katika hizi nyumba za serikali kama alivyoeleza Mhe. Jaku Hashim kwamba hivi karibuni tumepitisha Mswada ambao unahusiana na Shirika la Nyumba, lakini lengo vile vile ni kuzikarabati nyumba hizi au kuzifanyia matengenezo makubwa.

Lakini pia suala la kuhusiana na suala la mauzo tutaangalia, iwapo kuna haja ya kufanya hivyo basi tutafanya, lakini pia kama kuna haja ya kuziendeleza nyumba hizi kwa kuzifanyia ukarabati ili zitumike vizuri basi serikali kwa kupitia idara hii italisimamia hili.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Mwaka 2014/15

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea ninao wachangiaji kama saba nafikiri wanatosha sana kwa shughuli hii. Mchangiaji wa kwanza kwa asubuhi hii ni:

1. Mhe. Hassan Hamad Omar,
2. Mhe. Mohammed Haji Khalid
3. Mhe. Saleh Nassor Juma, na wengine wajitayarishe.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nami nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu katika ripoti ya Kamati ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) aliyetujaalia kuwa na uhai uzima na afya na kuruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze watu wa Kamati na wizara zote mbili zilizowasilisha, ripoti ya utekelezaji na maagizo ya Kamati kwa Wizara. Wakati nikiendelea na mchango wangu nitajikita sana katika Sekta ya Uvuvi katika ukurasa namba saba.

Mhe. Spika, kama inavyoeleza agizo la Kamati ukurasa namba saba, agizo namba moja naomba kunukuu.

"Wizara iharakishe kutengeneza "*Business Plan*" itakayoongoza katika mchakato wa ununuzi wa boti za wavuvi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, ambazo wizara na wavuvi wetu wanaweza kuzimudu kulingana na mahitaji na mazingira ya Zanzibar"

Mimi niipongeze Kamati kwa kuliona hili, Mhe. Spika, wavuvi wetu ni wavuvi wadogo wadogo na hawamudu kwenda masafa marefu, lakini Kamati imeliona hilo kupata boti ambazo zinaweza kufikia uvuvi wa bahari kuu ni jambo zuri.

Katika utekelezaji Mhe. Spika, wizara imesema kwamba tayari wameshafanya *Business Plan* na kufanya mazungumzo na Kampuni ya *Hairu* kwa ajili ya uwekezaji na kupata hizo boti zinazokusudiwa, lakini Mheshimiwa namuomba Waziri husika atakapokuja hapa atwambie kwamba maboti haya yana ukubwa wa kiasi gani, ili tuweze kukidhi hiyo haja ya kuwapeleka wavuvi wetu katika bahari kuu.

Kwa mfano sisi tuna wavuvi wetu wa Kikojani wanazo zile ngwanda za kivuvi, wanavua nyavu za mtando, lakini boti yao moja inabeba watu 60 mpaka 70, sijui nyinyi mliofanya mazungumzo na hawa Kampuni ya *Hairu* ina uwezo wa kubeba watu wangapi? Ukilinganisha nchi yetu ni kisiwa na wavuvi ni wengi kila kona ya Zanzibar hii Unguja na Pemba. Naomba Waziri utakapokuja hapa utupe maelezo ili na wadau ambao ni wavuvi wapate kufahamu.

Mhe. Spika, vile vile nikiendelea hapa hapa. Je, watakaofaidika na hizi boti ni wavuvi wa aina gani, tunataka kuwajua. Kwa sababu hapa zinaweza zikaja boti lakini wakapewa watu waliokuwa hawahusiki na shughuli za uvuvi na wavuvi wakaachwa pale pale. Hili si jambo zuri hata kidogo, na tumeyaona sehemu mbali mbali.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika Sekta hii hii ya Uvuvi agizo namba tatu. Agizo la Kamati limesema naomba ninukuu:

"Wizara ihakikishe kwamba inawapatia hati miliki ya matumizi ya ardhi katika maeneo na madiko wanayoyatumia wavuvi wetu."

Hili ni jambo zuri, tena napenda kuipongeza Kamati kwa kuliona hili. Kwa sababu kama kuna kazi ya wavuvi mojawapo ni hii hapa. Lakini katika utekelezaji Wizara imejitahidi imeshawapatia hati miliki madiko yasiyopungua saba na naomba niyataje, kuna baadhi ya madiko tayari wameshapatiwa hati miliki nayo ni Nungwi, Tazari, Kilimani, Matemwe, Kigomani, Pwani Mchangani, na Kendwa na bado wizara inaendelea kutengeneza hati miliki za maeneo mengine.

Mhe. Spika, hoja yangu Wizara ya Uvuvi na Mifugo hii imeenea Unguja na Pemba lakini masikitiko yangu makubwa ni kuwa kule Pemba hata diko moja halijapatiwa hati miliki na wizara ni hii hii moja, sijui ni kwa sababu gani za msingi, lakini pamoja na kusema kama ni endelevu ni vizuri, lakini hatimiliki hizi zitawakomboa wavuvi wetu. Kwa mfano, tumeona kadhia nyingi sana walizopata wavuvi, ukiangalia kule Nyanjale wavuvi walikuwa wanafanya shughuli zao za kivuvi na ukiangalia Sekta hii ya Uvuvi inaajiri watu wengi sana. Kuna wavuvi wenyewe kuna watu wengine wanakuja kununua, na kuna watu wanaofanya kazi kwa kubeba na kujipatia rizki, lakini hati miliki ya madiko na sehemu ile wakamiliki wavuvi kwa shughuli zao za kivuvi ni jambo zuri sana.

Naipongeza sana wizara mmekwenda mbali, lakini mjitahidi, watu wanapata dhiki na Nyanjale kule tayari wameshafukuzwa na kuwepo maeneo ambayo wao hawastahili wala hawayapendi, kwa sababu wavuvi wanafanya shughuli zao kando kando ya bahari, lakini leo serikali inaweza ikawachukua ikawatupa juu kabisa kinyume na matarajio yao. Hata pale Bububu watu wamejikusanya vizuri sana, Maruhubi wamejikusanya pale watu hawapungui elfu mbili wamejikusanya pale, lakini na wao wapo hatarini kuwafukuza.

Serikali imefanya jambo jema vile vile ni lazima tuipongeze. Wameambiwa wale watu watafute maeneo ili mpate eneo la kufanya shughuli zenu. Wadau na wao walipata sehemu ya eneo wakaielekeza serikali, lakini serikali haikuwakubalia sehemu hiyo na ikawapa sehemu nyengine ni juu mbali. Mtu anabeba dagaa anabeba masafa marefu na wale wanatamani wengine wanachemsha hilo dagaa wavuvi wakishauza wanunuzi wanalichemsha na kulianika. Ni ajira watu waje wapate kipato, lakini mnawasukuma na wengine wanakata tamaa. Hii ni hali mbaya hadi tuijue, ambapo watu hawa tusipowapatia nafasi nzuri na kufanya kazi zao, basi tunazalisha vibaka wengi ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika Sekta ya Uvuvi nije katika agizo namba 5, ukurasa wa 9, Mhe. Spika, naomba kunukuu kama kawaida nilivyoanza michango yangu.

"Wizara ihamasishe uwepo wa ufugaji wa samaki wa maji baridi pamoja na kuwapa kipaumbele na mashirikiano kwa wale wote wanaoanzisha huu ujasiriamali kwa kuwapa misaada na chakula cha samaki."

Mhe. Spika, na hili vile vile ni jambo zuri kuwapa misaada hao walioanzisha katika wajasiriamali katika kuwapa misaada ya chakula, lakini tuelewe kama hapa Wizara inahamasisha watu kufuga samaki wa maji ya chumvi, na sasa hivi wizara inahamasisha wajasiriamali kama walivyotajwa hapa kufuga samaki ndani ya maji baridi.

Mhe. Spika, ikumbukwe serikali na wizara iliwachukua wajasiriamali hawa kwenda nao China kwenda kuwafundisha namna ya ufugaji wa samaki, lakini kwa bahati mbaya uono wangu mimi naona safari zile hazikuzaa tija, kwa sababu sioni maendeleo ya wafugaji samaki na ukaona kweli kwamba hawa wamefikiwa kiwango cha kuondoa umasikini na kujipatia tija sioni kabisa. Unaona mtu anakwambia kila ukimkagua anakwambia ana vifaranga vya samaki elfu mbili lakini ukiangalia matatizo, hatuoni samaki waliofugwa mitaani au katika masoko.

Mhe. Spika, hii inatokana na usimamizi mbovu katika sekta hii ya ufugaji wa samaki. Watu wanakwenda kuoneshwa tuta hatuoni samaki, tunadanganywa tu, lazima kuwe na usimamizi mzuri katika sehemu za maendeleo, tuangalie wenzetu huko tulipokwenda kujifundisha, jinsi samaki wanavyowatoa, wanakuja kwa makontena lakini hapa ni kinyume na matarajio yaliyopo.

Mhe. Spika, taratibu zetu tunazozipanga ni nzuri lakini usimamizi wetu ni mbovu, tukishaanza huku katika ufugaji wa samaki wa maji chumvi leo tunaelekea katika ufugaji wa maji baridi. Tumeshindwa katika maji chumvi je, maji baridi? Mimi naona hapa bado hatujafikia malengo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika shughuli hizi wamezungumzia katika kutoa kitabu kwa ajili ya kujua utaratibu au muongozo, Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, kutoa miongozo kwa wavuvi kujua mambo ya kisheria ya uvuvi. Mimi nawapongeza sana ni jambo zuri sana.

Lakini tukumbuke Sheria Namba 7 ya Mwaka 2010. Sheria hii wametoa kwa lugha ya Kiingereza ambapo wavuvi hawaifahamu. Baada ya kwisha kuitengeneza inabaki humo humo Afisini wavuvi hawaifahamu. Tuombe huo muongozo basi utolewe kwa lugha ya Kiswahili na wadau wapelekewe. Tunazo jumuia za kivuvi kama KOFDO inafanya kazi vizuri tu na nyote mnaielewa. Inafanya kazi nzuri kuwaelimisha wavuvi. Mshirikiane hao ndio wadau wenyewe, lakini leo tunajitungia mambo tu bila ya kuwashirikisha wadau ndio tunapokuja kupata matatizo na hatimaye kukamatana bila ya watu kupata uelewa.

Mhe. Spika, inatakiwa ikumbukwe kabisa kama Sheria hii Namba 7 ya Uvuvi kwa mujibu wa mtazamo wa KOFDO ina mambo matatu muhimu nadhani na wahusika wenyewe wa uvuvi wenyewe wapo pale juu na Mhe. Waziri yupo atajua.

Sheria Namb. 7 ya uvuvi ya mwaka 2010, Sheria hii kwa mtazamo wa Jumuia ya KOFDO wakambieni KOFDO ambao hamuwashirikishi imezingatia mambo makuu matatu yafuatayo na naomba niyataje.

1) Kulinda na kuhifadhi mazingira ya baharini na fukwe pamoja na viumbe vya baharini.
2) Kutunza maeneo tengefu kwa ajili ya kuhifadhi matumbawe ili kuboresha shughuli za kitalii.
3) Kuendeleza kudhibiti shughuli za uvuvi ziendane na matakwa ya kisheria hapa.

Ni vizuri kulinda hizo taratibu za kivuvi ili ziendane na kisheria, lakini je, hawa wavuvi mnawafichaficha, ili na wao wakatoa ya kwao mkaenda sambamba. Tusijidanganye mimi nadhani hawa wavuvi wakubwa wakubwa watachukua miaka na miaka, lakini wavuvi wadogo wadogo hawatoondoka hata siku moja, kwa sababu bado hatujawawezesha kuwapeleka huko sehemu ya bahari kuu, lakini hawa tukitunga jambo tukiwashirikisha tutakuwa tumefanya jambo la maana na katika utendaji wetu wa kazi tutakuwa hatupati tabu.

Tuliambiwa Waheshimiwa nakala hizo watapata ili kuelimisha wananchi wao, lakini mimi nasema pamoja na Waheshimiwa kupatiwa hizo nakala basi watu wa kwanza wapatiwe hao wadau wenyewe ambao ni wavuvi, na kule kunako wavuvi kuna viongozi wao, kama sisi hapa kiongozi wetu wa sehemu hii ya jengo letu hapa tunapozungumza ni Mhe. Spika, na yeye tunamuongoza. Ndio maana wavuvi wana manahodha, ukiwapa hizo nakala watawaelimisha na huyu nahodha akijua atajua kuwaambia mabaharia wake anaowaongoza, kinyume na hivyo vyovyote tutakuwa hatufiki katika malengo.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana na mimi namalizia tu, nikimalizia niende katika sekta ya habari kuhusu jambo moja tu. Katika Baraza hili tumepiga kelele sana katika kuwalipa posho hawa ndugu zetu wanaofanya kazi hii, lakini imekuwa ni kikwazo kikubwa sana miaka yote kila ikifika tunazungumza kwenye bajeti, lakini bado kabisa hatujasikilizwa. Mimi nasema hii kama ni haki yao basi mnatudharau sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutofikia malengo.

Kwa haya machache Mheshimiwa ninakushukuru sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kusema machache sana kuhusu ripoti hii iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kufika hapa kuendelea na shughuli zetu za kazi zetu za kawaida.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja na Wizara ya Habari na agizo namba 1(a) hapa kamati iliiagiza Serikali ihakikishe inaweka majenereta ya uhakika katika vituo vya *ZBC* pamoja na kujenga vizuri katika gharama za uendeshaji wa majenareta hayo. Sasa ametoa maelezo marefu kuwa wamenunua, wametengeneza lakini kuna kitu kidogo tu mwisho walichosema jenereta limefanyiwa matengenezo na linafanya kazi vizuri isipokuwa Shirika linatafuta waya maalum kutoka kwenye jenereta hadi kwenye mitambo ya studio.

Sasa huu waya maalum kama unatafutwa naona haujapatikana, kwa hivyo agizo hili litakuwa bado halijatekelezwa, kwa sababu itakuwa pamoja na matengenezo yaliyofanywa na kila kitu, lakini ili lifanye kazi vizuri na kuunganisha mambo mengine huu waya lazima upatikane na ioneshe kuwa haujapatikana ndio maana hapa ukatajwa hivyo, je waya huu ambao ni waya maalum una ukubwa gani, na gharama zake zikoje mpaka ikawa ni kitu ambacho agizo pengine halikukamilika kutekelezwa kulingana na ukosefu wa huu waya maalum ambao unatafutwa.

Mhe. Spika, agizo hilo namba 1(e) ambalo liko ukurasa wa 4 linalozungumzia *ZBC* iwe makini na ihakikishe kwamba taarifa zake za habari zinakwenda na wakati na pia wahakikishe kwamba hawapitwi na habari muhimu hasa za kitaifa na kimataifa.

Umetajwa utekelezaji wake, Mhe. Spika, *ZBC* Radio na Televisheni ndio mdomo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ni chombo ambacho kipo zamani kabla ya vyombo vyengine vya habari vilivyojitokeza baadae. Pamoja na kuwa ni chombo cha Serikali chenye kutoa huduma lakini kwa upande mmoja Mhe. Spika, pia ni chombo cha biashara, kuna huduma zinapotolewa lazima zidhibitiwe, kwa hivyo ni chombo cha huduma cha Serikali lakini pia ni chombo cha biashara kwa upande mwengine.

Sasa Mhe. Spika, redio yetu imepikuliwa na redio zilizokuja juu juu hivi sasa, watu walio wengi wa Zanzibar wanasikiliza hizi *FM radios* kuliko *redio* yetu ya *ZBC*. Watu walio wengi wanaangalia *channel* za Tanganyika zaidi kama *Channel* 10, *ITV* na nyenginezo kuliko tunavyoangalia hii ya kwetu. Kwa hivyo ningeomba wizara iangalie kwa nini Wazanzibari wakawa hivyo kuacha chao kwa kutegemea kile cha wenzao. Bila shaka itakuwa kuna sababu nyuma yake ambayo kuna sababu mbele ya kila kitu ikiwa mtu anajua. Lazima kutakuwa kuna sababu ya kufanya hivyo watu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa upande mmoja chombo hiki ni cha biashara, kwa hivyo zile taasisi ambazo zinafanyiwa kazi pale ambapo inabidi malipo yatolewe ni kuwa taasisi hizo malipo hayo wayafanye. Hapa imeonekana kuwa ziko taasisi ambazo zinatumia huduma ya chombo hiki na hazitoi malipo, pengine ndio maana ikawa baadhi ya mambo yanakosa ufanisi kwa kukosa ile pesa ndogo ndogo ya kujiendesha.

Kwa hivyo ningeomba Mhe. Spika, wale ambao wana madeni ya vyombo vyetu hivi kwa kupeleka matangazo na mambo mengine walipe madeni yao ili hiki chombo kiweze kwenda vizuri. Kadhalika Mhe. Spika, redio zetu na televisheni tunazitumia katika sherehe zetu maalum, kama za sikukuu zote mbili; Eid, Maulid, Sherehe za Kitaifa za Serikali na kadhalika. Je, sherehe hizi zinapofanywa

vyombo hivi vinapatiwa malipo au ni kwa sababu cha Serikali wanafanya tu kwa sababu ni shughuli ya Serikali. Kama tunafanyiwa hivyo hatutoi malipo ya aina yoyote kwa hivyo tunawakwaza katika shughuli zao za kazi za kawaida.

Hapa Mhe. Spika, nimeona kuwa na sisi humu vyombo hivi vinatuhudumia, lakini kumbe hatulipi na sisi tunasimama kuwaombea posho hawa wanaosimama masaa yote ambayo sisi tumekaa kitako humu, mtu hata akisimama ama anazungumza au anaomba kutoka nje lakini takriban wakati wote wamesimama na tunawaombea posho lakini kumbe hilo halitopatikana kama sisi kama tutawajibika kulipa humu na ikawa hatulipwi. Kwa hivyo ningeomba taasisi hii ambayo inafanyiwa kazi mara zote katika vikao hivi kama ina malipo kazi hii kwa vyombo hivi vya habari, kwa hivyo tuwafanyieni huruma tuweze kuwahudumia kuwalipa hizo shughuli zao.

Vile vile nimeona Hoteli ya Bwawani iko hivyo hivyo tunaitumia, taasisi za Serikali wanaitumia wengine wanalipa wengine hawalipi, tusiwakwaze hao wenzetu, tuwalipeni ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi ili waendelee vizuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa Wizara ya Habari au vyombo vyetu vya habari ndio mdomo wa Serikali, agizo liko kuwa watoe habari *up to date*. Mara nyengine habari inayotolewa na chombo chetu inaweza kuwa imepita siku mbili nyuma katika redio za kidunia sisi tukai-*quote* siku mbili baadae. Habari kama hii huwa tayari imepitwa na wakati. Halafu kulingana na uhaba wa vyombo vya kutendea kazi, *coverage* yao mambo mbali mbali kama kutakuwa pengine Mhe. Rais yupo pahala fulani, Mhe. Makamu wa Pili yuko pahala fulani kuna mtu mwengine ana haja pahala fulani ufuatiliaji wake unaweza ukakwazika kulingana na pengine na uhaba wa vyombo vya kufuatilia taarifa zao hizi. Kwa hivyo wizara hii lazima kwa kuwa ni mdomo wa Serikali, huu mdomo upambwe vizuri ili uvutie na uweze kupiku hizi redio ambazo zimejichomoza.

Mhe. Spika, nitoke kwenye Wizara ya Habari nije kidogo vile vile katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi nayo wizara hii ni wizara muhimu kwa upande wake na ina maagizo kadhaa. Mhe. Spika, kwa wizara hii ningeomba nianze na agizo namba 4, naomba maelezo juu ya utekelezaji wa agizo hili na ningeomba Mhe. Spika, nisome ili nifahamike hicho ninachotaka, agizo liko hivi:

Wizara iwahamasishe wafugaji ili wachukue tahadhari mapema ya kuwakinga wanyama wao na maradhi mbali mbali kwa kuwapeleka kwenye chanjo.

Utekelezaji hapa ndio Mhe. Spika, ninapotaka maelezo kidogo. "Tahadhari ya mapema ya magonjwa ya mifugo na kuwalinda wanyama kwa kutumia chanjo, mfumo wa tahadhari wa magonjwa ya mifugo kwa magonjwa ya mripuko na unaendelea kutumika". Mimi hii sentensi Mhe. Spika, sikuifahamu ningeomba Wizara ifahamishe maana ya sentensi hii.

Halafu Mhe. Spika, lile agizo lilikuwa kwa mifugo lakini majibu yanayoendelea yamejibu kwa ng'ombe na kuku tu, wakati ambapo mifugo wako mbuzi, mabata, njiwa, paka na mbwa, hawa hawakutolewa ufafanuzi wao katika kufugwa kwao.

Agizo namba 7 ukurasa wa 6 agizo liko hivi:

"Kamati inaishauri wizara kuandaa mpango maalum utakaoainisha kujikinga kwa ugonjwa wa ndui unaowashambulia mifugo kama kuku, njiwa na mabata mzinga baada ya mifugo hiyo kupatiwa chanjo ya mahepe".

Utekelezaji, pamoja na kuwa wametajwa kuku, njiwa na mabata mzinga waliotolewa ufafanuzi ni kuku pekee hawa wengine hawakutolewa majibu yoyote ya tiba yao. Bado ina maana wanyama wengine wote wanaofugwa Wizara ama haiwatambui au hawana njia ya kuwatibu isipokuwa kuku na ng'ombe.

Mhe. Spika, agizo jengine ni agizo namba 8 ukurasa wa 7 ambalo hili agizo linaagiza kuna shamba fulani Pangeni lipatiwe hati miliki, utekelezaji unasema hivi:

"Shamba la Pangeni lishapimwa tokea miaka 50 iliyopita, watu wasiokuwa waaminifu wanang'oa alama za mipaka *beacon*, watu waliokuwa wamechukuliwa sehemu zao pia wameshalipwa tokea mwaka 1959, wizara imepeleka ombi la kutengenezewa hati miliki Wizara ya Ardhi, lakini bado Wizara ya Ardhi haijatupatia hati miliki".

Mhe. Spika, hili shamba inaonesha kuwa ni la zamani sana kwa mwaka uliotajwa kuna watu wengi walio humu ilikuwa hawajazaliwa na hadi leo kwa shamba hilo Serikali imeshindwa kulipatia hati miliki. Ili kuondoa uvamizi wa shamba hilo nami Mhe. Spika, ningeomba Wizara inayohusika na utoaji wa hizi hati miliki ilipatie hati miliki hili shamba ili wizara hii ya Mifugo na Uvuvi waweze kulidhibiti vizuri na kulijengea uzio ili kuondoa huo uvamizi ambao unaonekana unaendelea siku hadi siku.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu machache hayo naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nashkuru na mimi kunipatia fursa kidogo kuweza kueleza chochote kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutupa uwezo wa kuishi na kuja hapa Barazani.

Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja katika hoja iliyoko mbele yetu na nianze na hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Katika agizo namba 4 katika wizara hii wizara inatakiwa ifanye marekebisho ya sheria ya mifugo kuwadhibiti wafugaji wakaidi ambao wanakwepa mifugo yao kuipeleka kwenye chanjo.

Kwa kweli haya majibu ya Serikali kwanza napenda niipongeze kwa hili na kwa vyovyote vile hii Tume ya Kurekebisha Sheria kwa sababu jambo liko mikononi mwao ni vyema kuharakisha kuona kwamba huu mswada unaletwa hapa kwa ajili ya kuwa sheria. Nimelazimika kusema hivyo kwa sababu Mhe. Spika, Wazanzibari tumewekeza maisha yetu katika suala zima la mifugo na *infact* katika hili sisi kama wafugaji wadogo wadogo tunaweza tukasema kwamba Serikali haitupi ile *moral support,* kwa sababu ukija katika vijiji huko aina ya mifugo tunayofuga na njia tunazofugia mifugo ni zile za kizamani. Kwa mfano, katika masuala ya ufugaji wa kuku bado mpaka sasa hivi tunaendelea kutumia ile *deep litter system* unaweka makapi ya landa mule ukishaweka makapi ya landa mifugo inakaa mule ya kuku, zikiingia churua yote inakufa. Hawa Maafisa Ugani, sijui maafisa mifugo katika ngazi za Wilaya hatuwaoni kukutembelea kutupa angalau elimu ya ufugaji bora. Leo tunaambiwa tu hapa kwamba sijui churua, utumie dawa hii tunaenda katika maduka ya madawa kule ili kuona kwamba tunaenda kutibu *by trial and error*. Sasa ilikuwa tuulizane kwamba serikali ingetuletea maafisa mifugo katika maeneo yetu ili kutupa *knowledge* ya ufugaji bora.

Mhe. Spika, mimi juzi nilibahatika kwenda kutembelea JKT Ruvu, tulipokwenda kule tulibahatika kuona mambo mengi katika mambo ya mifugo. Sasa wale mbali na kutumia ile *deep litter system* katika kuku wao wanakitu wanaita *battery cage system*. Hii *battery cage* kila kuku anakuwa na kisanduku chake akizaa yai linateremka chini, sasa sisi mambo kama yale ni mageni hapa Zanzibar.

Kwa hiyo, wizara ipo, serikali ipo lakini sisi tunachokiona kule ni kwamba tunafuga *by trial and error*. Sasa serikali hii ule mpango wake wa kupunguza umasikini na kujiongezea kipato kwa sisi wananchi inakuwaje wakati mifugo yetu inaathirika kwa maradhi. Mhe. Spika, katika hili nadhani serikali iwe makini katika kutupatia *knowledge* ya suala zima la ufugaji.

Mhe. Spika, sisi katika miaka ya nyuma wafugaji wa ng'ombe wa kienyeji kule sehemu za Vitongoji kulikuwa na josho tangu lilipoondoshwa lile josho hakujajengwa jengine, tunachotumia ni ile *spray* ya mkono kuwatilia ng'ombe wetu dawa ambapo hata ile *proportionality* ya michanganyo hatufahamu.

Sasa niliiomba serikali katika hili kama mtakuwa na uwezekano hata yale majosho muyarejeshe kusudi vile vipimo vya kuweza kutia katika maji yale na ng'ombe kuingia mnavijua nyinyi wataalamu. Lakini sisi tunachukua matenki ya maji tunaweka madawa wakati wengine ng'ombe hivi karibuni ng'ombe wetu waliumwa na ngozi. Ng'ombe waliteketea sana mpaka sasa hivi wanafanya maradhi ya ngozi, ng'ombe wengi wamefarijika kipindi hiki. Naamini kwa sababu hatukuwa na *technical advice* ya wale wataalamu katika mambo ya mifugo wameendelea kututoka mpaka hivi karibuni ndio naona kidogo umepungua. Lakini katika hili badala ya kupunguza umasikini sisi wafugaji tunaongezeka umasikini kutokana na suala zima la ugonjwa wa mifugo yetu.

Aidha, mimi nilizungumza hapa katika Ofisi ya Makamu wa Pili nilileta suala nilitarajia kwamba hii ni ofisi kubwa ingetusaidia, kwamba sisi wafugaji wa kuku, sisi ambao tunatumia ile *extensive system* tunawaachia asubuhi wanakwenda nje jioni wanarudi katika mabanda yetu kwa sababu hatumudu kuwanunua chakula wengine hawamudu kuwanunulia chakula. Sasa wanatumia ile *extensive system* ya *food keeping* unawaachia asubuhi jioni wanarudi. Lakini wakifika kule *mortuary* wanaliwa, wanaibiwa kuku, wanachukuliwa pale *mortuary,* watu wanakunywia gongo, na kwa bahati ilikuwa hawaamini watu kama kuna *mortuary*. Kwa bahati nzuri nikamchukua mdogo wangu Mheshimiwa hapa Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais tukaenda mpaka *mortuary* na akaona pale, na vitu aliviona sambamba jinsi ya watu mpaka yale mazungumzo alikuwa hayafahamu hapo tulipokwenda akawahoji watu hawafahamiki.

Mhe. Spika, katika hili la mifugo naunganisha na ofisi ile kwamba si maradhi tu ya kuku ambao yanatuumiza pamoja na mbuzi wetu, ni pamoja na wizi wa *mortuary* hili liko nje ya uwezo wako lakini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ione hilo kwamba wafugaji tunaathirika vile vile na mifugo ambayo imeachiwa.

Ile mifugo iliyoachiwa kama mbwa, mbwa wanakamata kamata kuku vibaya sana halafu ng'ombe anazaa pale leo ukienda ndama ameshaliwa na mbwa. Vile vile ni tatizo, hivi juzi karibu ng'ombe kumi na tano pale katika eneo la Vumba, eneo la Umangani, eneo la Changuo, eneo la Kibokoni ng'ombe karibu kumi na tano ndama zao wameliwa na mbwa.

Zamani kulikuwa na bwana mmoja pale Wawi anaitwa Abdalla Upepo naamini Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili anamfahamu bwana Abdalla Upepo kwa sababu alikuwa CCM mwenzake sana huyu. Alikuwa ana magobore anapiga wale mbwa pori ambao wanatumalizia mifugo, lakini sasa bwana Upepo amefariki gobore lile alikuwa akiazimwa bwana mmoja anaitwa Ajili, tunashukuru kwamba ilikuwa akitusaidia sana bwana Ajili kudhibiti mifugo yetu isiliwe na mbwa lakini siku hizi hapewi.

Sasa naomba kwamba Mheshimiwa katika hili naunganisha baina ya mifugo na Ofisi ya Makamu wa Pili kwa sababu bila ya gobore huwezi kutupatia kwa ajili ya mifugo ambayo ndio sehemu ya kazi yetu, lakini kwa bahati leo nachangia hii Mhe. Makamu wa Pili yupo uone kwamba sisi si maradhi tu yanayoathiri ni pamoja na mbwa, mbwa anaathiri sana.

Mimi nilikuwa nataka kutoa utaalamu wangu pale tuwa-*control* mbwa kwa kutumia *predator prey relationship* kwa kuweza kuchukua wale wanyama wanaoweza kuwala mbwa ambao ni fisi, tukaona aah kuja kuwaingiza fisi wakishamaliza mbwa hawa wanakuja kula sisi, nikashindwa. Sasa lazima tutumie *mechanical system* ya kuweza kutumia magobore. Mhe. Spika, Mheshimiwa atusaidie sichangii Ofisi ya Makamu wa Pili nachangia haya mambo ya mifugo lakini *prevention* ya hao mbwa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nimalizie kuja katika sekta ya uvuvi. Mhe. Spika, sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana, kwa sababu asilimia karibu 80 ya Wazanzibari tumewekeza maisha yetu katika sehemu ya uvuvi. Na *infact* katika kuvua tuna tatizo kubwa sasa, wavuvi tulikuwa tunawachukua samaki wetu tunauza madagaa yakiwa hayamalizi madagaa, tunayaanika katika *beach* na tulikuwa tunafanya hivi hapa Maruhubi hapa. Pale pana watu zaidi ya elfu nne wamewekeza maisha yao pale,

kuna wavuvi na wale wachuuzi ambao wanakuja pale karibu watu elfu nne wamewekeza maisha yao. Maruhubi pale ambapo panataka kujengwa hili bandari.

Mhe. Spika, sasa pale wanataka kuondoshwa lakini serikali mpaka sasa hivi hawajui hawa watu watakwenda wapi kufanya shughuli zao. Kwa hivyo, takriban wavuvi sasa hivi tunaendesha shughuli zetu katika *trial and error system*, ni tatizo serikali haiko *serious*. Kwa sababu serikali mngekuwa na viwanda vya kutuajiri, mngekuwa mna mafuta tunachimba tunaenda katika kujaza mafuta, basi tungekuja huko tungeacha kuvua, lakini viwanda hamna, ajira hamna, tumewekeza katika uvuvi leo kila wavuvi wanawekeza Maruhubi pale kuanika madagaa sasa hivi mnaanza kuwaondosha.

Nyanjale kapewa jamaa ajenge viwanja vya kucheza *golf* badala ya kuweka watu elfu nne wale wakwezi na wakulima wa nchi hii ambao ndio waliokuwa wanatakiwa wafaidi matunda ya Mapinduzi ya mwaka 1964, leo eneo kubwa ambalo wanaanika dagaa lao watu wa Nyanjale wamenyang'anywa na anapewa mtu anataka kucheza *golf*. Faida ya mapinduzi iko wapi, *we are slaves within our country;* ni watumwa katika nchi yetu sasa hivi. Kwa sababu kama ni kuwekeza ule ni uwekezaji mkubwa kudhibiti maisha ya watu waliowekeza karibu elfu nne ukawaambia raia wa nchi wayumbe hawana pa kuweka maisha yao wakienda hapa wanaondoshwa, wakienda hapa wanaondoshwa kuna sehemu ya Nyanjale wameondoshwa, kuna sehemu ya Mto Mkuu sijui sehemu za Kaskazini yaani ni shida tu.

Sasa mimi nadhani serikali katika hili muone kwamba tuna tatizo hapa, kutuajiri hamtuajiri, tukishajiajiri mnatukwama, maana hatua za kufukuzwa ni kukwama, mnatukwama katika maeneo tunayofanya shughuli zetu sasa twende wapi? Sasa katika hili ile idadi ya wavuta bangi, idadi ya wizi katika nchi inaweza ikaongezeka. Nadhani suala la wavuvi katika sehemu za Maruhubi, Nyanjale, Mto Mkuu Kaskazini huko naomba serikali itupe jibu kama watawaweka wapi na lini watawapatia pahala pa kudumu.

Mhe. Spika, jambo jengine tunalokumbana nalo hasa wavuvi wadogo wadogo ni pamoja na mazao yetu hayako *stable,* yaani hawa samaki wetu *price* inapanda na kushuka, bei ina-*fluctuate according to production.* Sasa sisi jamani nataka nijiulize miaka karibu hii 52 ya Mapinduzi mpaka leo hii sio wavuvi wa samaki tunavua kwa kuganga njaa tu, wenzetu hawana bahari wana ziwa, lakini wavuvi wa kwenye ziwa wana mazingira mazuri sana na soko la kudumu.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba hapa wenzetu katika Ziwa Victoria wana samaki wawili tu wa aina kubwa wale Satto na Sangara na wanawaita wawekezaji pale ku-*install* viwanda vya kusindika minofu ambapo mnofu wa sangara ni mdogo ukilinganisha na mnofu wa papa, ukilinganisha na mnofu wa jodari, ukilinganisha na mnofu wa kangaja, sijui leo kwa nini wale waweze ku-*install* viwanda kama vile sisi miaka 52 ya Mapinduzi tushindwe.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tatu tu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Hizo zinanitosha sana, Mheshimiwa kwa kumalizia *ZBC*.

Mhe. Spika, *ZBC* ni mdomo wa nchi. Leo kila unapoona eti wao katika *ZBC* agizo lililotolewa kwamba wanaboresha vifaa, wanaboresha vifaa, wanaboresha vifaa, hawa wafanyakazi je? Kama kuna watu wanafanya kazi nzuri Mheshimiwa ni hawa kwa sababu ni *connective link* baina ya wananchi na Baraza lao la Wawakilishi, hawa ndio wanaotoa habari sana wananchi kuona Bunge lao linafanya kazi gani.

Leo kwa taarifa tulizonazo hapa wakitoka wanapeperusha mifuko, hivi siku nyingi hawajalipwa hawa. Kama ni hivyo basi ni aibu kubwa, haya hawa wakisema siku hiyo hawataki kuonesha wameshachoka, wameshateketea kwa njaa hawawezi kuingia humu kwa njaa wananchi watapata wapi habari. Mimi nadhani Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya madukhuli katika hili basi wafanyieni huruma hawa vijana wetu, pamoja na kwamba mnataka kuboresha baada ya kununua vifaa vya *SONY* sijui haya lakini hao mkishapata vifaa vya *SONY* hao wafanyakazi wataweza kwa mashaka ya njaa?

Kuna wafanyakazi wa *ZBC* kule Pemba juzi juzi tu huu mwezi uliopita wamenipa habari kwamba zile elfu ishirini ishirini katika mishahara yao hawajaingiziwa mpaka hivi sasa, jamani kama ni kweli huo ni uonevu mkubwa.

Sasa mimi nadhani Mheshimiwa ujitahidi sana, na katika hili taarifa ya waziri au nilitegemea tu kwamba taarifa ya kamati nayo ingeweza kutetea madukhuli angalau tungeona madukhuli ya hawa jamaa zetu wa *ZBC,* pamoja na kwamba taarifa zetu nyengine sisi wanazikatakata hawatutolei, lakini sisi tuna wajibu wa kuwatetea hawa ni walipa kodi wa nchi hii.

Naiomba sana serikali hawa au hili Baraza ikiwa Baraza haliwalipi Spika leo kwa bahati mwenyewe upo katika kiti chako cha enzi hicho na sisi tutakuheshimu sana, ikiwa hawa hawapati madukhuli wakija kurusha habari zetu na kiti chako ni mas-uul basi tunakuomba sana kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu uwapatie malipo yao hawa vijana ili watu waendelee kunufaika na Baraza lao, huu ndio mdomo wa wananchi huu. Ikiwa hawa vijana hawakufanya kazi vizuri wakiwa wanashiba katika tumbo wakashindwa kufanya kazi wananchi watakosa kile wanachokihitaji, yaani taarifa za Baraza.

Nimalizie Mhe. Spika, kwa jambo moja tu wawe makini katika kutoa habari Maalim pale kwamba habari za mipasuko zile mbona zinachelewa kutupatia mpaka wanatoa hawa jamaa wa *Zenji FM* habari mpasuko, *breaking news* ni tatizo gani hatupati *breaking news*. Naunga mkono taarifa, ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Spika ahsante, na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti hizi za wizara mbili; Wizara ya Habari pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na michango mitatu tu katika Wizara ya Habari nitakwenda katika *page* 5, agizo Nam. (g) hili ambalo linahusiana na Shirika la Utangazaji.

Mhe. Spika, agizo hili linasema "Kamati inaitaka wizara kukaa pamoja na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala la kulipia matangazo ya mikutano ya Baraza la Wawakilishi kwa *ZBC*, kwani kamati inaamini kuwa *ZBC* inaweza kujiimarisha endapo Baraza la Wawakilishi litalipia matangazo hayo".

Mhe. Spika, hii mimi ninaliunga mkono, naiunga mkono kwa sababu Mhe. Spika, ili Shirika lijiendeshe linahitaji lipate vyanzo mbali mbali vya mapato likiwemo hilo pato ambalo litatokana na hili Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, kulipwa kutoka Baraza la Wawakilishi shirika hili Mhe. Spika kutasaidia shirika lenyewe kujiimarisha hata yale matatizo madogo madogo ya kulipwa maposho wafanyakazi yanaweza yakapungua kwa asilimia kubwa.

Mhe. Spika, watu wengi wamezungumza kuhusu malipo ya hawa wafanyakazi wa *ZBC* ambao wanachukulia matangazo humu Barazani. Naomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi kwa sababu hawa vijana wetu wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi nzuri na pia wana uzalendo wa nchi yao. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri alifanyie kazi suala hili na pia nilitaka kujua hasa ni muda gani hawajalipwa hawa maposho yao hayo, malipo yao ya mwisho yalikuwa muda gani? Mhe. Waziri naomba unijibu na vikao vingapi ambavyo wanavidai, maana yake hawajalipwa maposho yao? Nilikuwa naomba nipate maelezo Mhe. Waziri kwa sababu kufanya hivyo ina maana tunawavunja moyo hawa wafanyakazi, wanafanya kazi kwa moyo kabisa.

Nitakwenda katika Kamisheni ya Utalii iko katika *page* 10.

Mhe. Spika, Kamisheni hii ya Utalii imesema kama kuimarisha hali ya usalama wa watalii, wawekezaji na mali zao. Na suala la amani na utulivu Mhe. Spika kwa wawekezaji na hata kwa wananchi ni muhimu. Na ukiangalia sekta ya utalii Mhe. Spika inachangia karibu zaidi ya asilimia 30

katika pato la Taifa. Kwa hiyo kutetereka kwa wawekezaji, kutetereka kwa utalii hapa nchini kunaweza kukashusha hali ya uchumi ya hapa nchini.

Kwa hiyo, suala la kuimarishwa ulinzi, usalama wa watalii, wawekezaji na mali zao pamoja na wananchi wa nchi hii ni muhimu sana. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi kuna matukio mbali mbali ambayo yametukabili hapo mbele, kuna suala zima la Katiba inayopendekezwa kupiga kura, suala la uchaguzi, lakini wote watatumia fursa hii kuvuruga amani na utulivu uliopo.

Kwa hiyo suala la kuimarishwa amani na utulivu ni muhimu sana na hasa katika kipindi hiki ambacho tunakwenda katika harakati hizi. Harakati hizo ndio watu wengi wanatumia kuvuruga amani ya nchi yetu. Hapa naiomba serikali kwa makini kabisa ijitahidi kuzidisha amani na utulivu wa nchi yetu hasa kipindi hicho ambacho tunaelekea katika matukio mawili mazito ya nchi.

Mhe. Spika, sasa niende katika Wizara ya Mifugo agizo namba 8 ambalo liko katika ukurasa wa 7, kuhusu shamba la mifugo Pangeni ambalo linahitaji hatimiliki. Suala la hatimiliki ni muhimu na kuna mashamba mengi ya serikali yamevamiwa na wananchi pengine kwa kutokujua uelewa wao mdogo, lakini suala la hatimiliki ni muhimu na niiombe tu Wizara ya Mifugo kama tunasubiri hatimiliki japo uzio ule wa kuzuia angalau lile eneo, tusiwaache wananchi washavamia, washajenga, matokeo yake serikali inakuja kupata hasara ya kuwalipa fidia wale watu ambapo si jukumu la lazima maana yake ilikuwa tunaweza kuliepuka hapo mwanzo kabla ya uvamizi.

Pia naishauri wizara iwe inafuatilia haya mashamba wasiache watu mpaka tena anaanza *foundation* anaangaliwa mpaka anamaliza, anaezeka tunaangalia tu, sasa hapo ndio tunakuja kushtuka kwamba mashamba yamevamiwa. Ufuatiliaji nao ni muhimu wa siku hadi siku katika maeneo muhimu kama hayo ya serikali.

Mhe. Spika, baada ya hapo sina mengi naomba niunge mkono tu ripoti hizi kwa asilimia mia moja.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, ahsante. Awali ya yote na mimi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kumshukuru Allah (*S.W*) kunijaalia na kuwajaalia na nyinyi wenzangu kuwa katika hali ya uzima na afya njema na pia kumtakia rehema Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*). Lakini la tatu kukuomba na wewe kwamba nipate fursa asubuhi hii kutoa mawazo yangu machache katika kamati hii ili kuweza kusema yale ambayo kwa upande wangu nimeona yanahitaji kufanyiwa kazi kwa uharaka.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na suala zima la Wizara ya Mifugo katika ukurasa wao wa tano hapa kuna agizo namba tatu. Agizo hili kamati iliitaka wizara kuvipatia taaluma zaidi vikundi mbali mbali vya wafugaji. Majibu ya wizara kwa mwaka huo kwa Zanzibar nzima walivipatia vikundi 16 na wafugaji binafsi 19,600.

Mhe. Spika, ukiangalia takwimu hii na jinsi wananchi wa Zanzibar walivyoshawishika katika taaluma mbali mbali wanazozipata kwa ufugaji wamejaribu sana kuwekeza katika sehemu hizi, lakini serikali bado ufuatiliaji wao umekuwa ni mdogo, kwa kweli vikundi 16 vya wafugaji ni hatua ndogo sana na hatua kama hii inawavunja moyo wale wafugaji wengine na utakuta watu wanajiwekeza huko lakini muda mfupi mitaji yao inakufa haraka. Kwa sababu wanakosa taaluma, wanakosa ushauri, kwa hivyo mwaka mzima kufuatilia vikundi vya wafugaji 16 yaani hatua ndogo sana. Ningelishauri sana kama kamati ilivyoishauri wizara ikusudie, wakurugenzi watoke maofisini wawafuatilie wafugaji wetu, ili ule mradi mtu anaoona huu unaweza kunikwamua katika maisha uweze kumkwamua kweli katika maisha.

Mheshimiwa tunaona kwamba pia kuna yule kijana aliyeamua kufuga *Alhamdulillah* mambo yake yanakwenda vizuri, kamati ikaiomba wizara yule kijana asaidiwe masuala ya umeme ili aweze kufanikisha haya mambo wizara imeshindwa. Sasa wanaposhindwa wao wafadhili wadogo wadogo wengine wapo kwa nini hawawatafutii watu kidogo wakaweza kuwakwamua? Unapomtafutia mtu mfadhili akamfikishia lile jambo tayari wizara imeshafanya wajibu wake, si lazima tu kwamba kila

kitu ikifanye yeye wizara. Kwa hivyo, na yule mfugaji wetu anapata motisha na anapata nguvu, lakini miaka inapita huduma haipatikani. Hili kwa kweli huwadhoofisha sana wafugaji wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele niendelee katika Sekta ya Uvuvi. Hapa sina budi niishukuru serikali ndani ya jimbo letu la Tumbe kutujengea soko kwa ajili ya wavuvi wa Tumbe na wilaya nzima ya Micheweni. Hili ni jambo la hongera sana na *Alhamdulillah* hivi karibuni Mhe. Rais alikwenda kulizindua lile soko ili lianze kufanya kazi zake vizuri. Kwa hivyo, mtu haki yake apewe, ni hatua moja kubwa ambayo tayari wavuvi wa Tumbe na maeneo mengine watafaidika katika kufanya kazi zao vizuri na kuzalisha mazao mbali mbali katika eneo lile la Tumbe.

Mhe. Spika, Zanzibar katika sehemu moja kubwa sekta inayoajiri wananchi wetu wengi ni sehemu ya uvuvi, na tukizungumza uvuvi kuna uvuvi wa aina mbali mbali. Lakini ndani ya shughuli hizi kunatokea matatizo mbali mbali wizara au idara inayohusika pale yanapotokea matatizo ni vyema kwenda mapema na kuyazuia matatizo yale ili yasiendelee. Kwa sababu asili ya moto ni cheche ndogo lakini itakapoanguka ile cheche kama haikushughulikiwa ikazimwa hatima yake inakuwa ni mripuko mkubwa, tatizo lile likaendelea na kuathiri maeneo mengi.

Kwa hivyo, ndani ya ujengaji wa soko hili tayari malumbano na matatizo mengine yameshaanza kujitokeza, na hili soko hadi leo halijaanza kufanya kazi zake rasmi. Kwa hivyo, uwekezaji ule wa serikali ni pesa nyingi zilizokwishatumika pale na malengo pesa zile ni kurudi kidogo kidogo ili wananchi wa eneo lile wafaidike, lakini serikali nayo iweze kupata mapato. Hivyo ningeliomba sana wizara ifuatilie tatizo liliopo Tumbe ili soko liweze kufanya kazi zake vizuri na wananchi wa Tumbe na maeneo mengine waweze kufaidika na soko lile.

Mhe. Spika, pia katika agizo la nne kwa kamati hii linasema kwamba, kamati ilitaka kuongezwa muda zaidi wa doria baharini na angani, kwani zinasaidia kuwashajiisha wenye meli na wavuvi wa bahari kuu kukata leseni na hatimaye kuongeza mapato ya mamlaka na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, hili ni wazo zuri na ni kweli kwamba meli zisizokuwa na usajili Zanzibar zinafanya kazi na zinaiba samaki wa Zanzibar na mambo mengine yaliyo ndani ya bahari kuu ya Zanzibar. Sisi wananchi maeneo mbali mbali tushashuhudia meli kubwa zinaweza kutia nanga muda mrefu karibuni mwezi. Maeneo ya pwani ya Micheweni, Tumbe, Msuka; maeneo hayo mara nyingi kuna vipindi meli kutoka nje zinakuja kutia nanga pale na kufanya uvuvi na meli zile kwa taarifa tulizonazo kwamba si meli ambazo zina usajili wa kuvua katika maeneo hayo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa wizara hii amesema kwamba mwaka 2013/14 kwa upande wa doria za baharini walifanya karibuni masaa 912. Masaa hayo ukiyafanyia hesabu kama sitokosea haraka haraka ni siku 38, karibu mwezi mmoja na siku nane kwa mwaka mzima. Kwa hivyo, siku 38 kwa mwaka ukiangalia ni muda mdogo mno. Sasa wavuvi hawa wa nje watapewa muda wa kuchukua samaki wetu na mambo mengine yanayopatikana baharini utakuwa ni mkubwa zaidi kwao kuliko doria zetu sisi tunazozifanya. Kwa hivyo ni lazima wao watafaidika zaidi kuliko pato la nchi, nchi itakuwa haipati pato lake.

Mhe. Spika, niungane na kamati kuitaka wizara na serikali, kwa sababu hizi doria zina gharama kubwa na hapa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, anipe takwimu sahihi ni shilingi ngapi katika siku hizi 918 ambazo wizara iligharamika kwa suala la doria ya baharini. Sasa kama hapa serikali haitaongezea bajeti wizara hii kazi hii ya doria itakuwa ngumu na haitoweza kufanyika.

Kwa hivyo, ni vyema ili kuinusuru bahari yetu vitoeleo vinavyopatikana na mambo mengine katika bahari hizi basi ni lazima serikali kama kweli inaamua iongeze bajeti ili tuweze kuhakikisha kwamba uharamia huu haupatikani.

Mhe. Spika, nikitoka katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi nije katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nianze katika sehemu ya Shirika la Utangazaji.

Mhe. Spika: Kwa dakika tano.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante. Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji ni shirika ambalo linaleta taaluma nzuri na linalifanya mpaka hili Baraza letu liweze kuwa hewani na kuweza kufaidika wananchi walioko Zanzibar na nje ya Zanzibar. Nikubaliane kwamba kamati ilizitaka wizara tatu zikutane ili haya tunayoyasema hapa Barazani ambapo kwa muda mrefu linatutoa hewani basi Baraza liweze kutoa gharama yake kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Baraza tumetumia muda mrefu na tunavyovitumia ni vyombo na vyombo hivi vitafika pahali vimalize hii huduma ianze kukosekana, lakini taarifa hii toka mwaka juzi, mwaka jana inazungumzwa lakini kwa majibu ya Mhe. Waziri anasema bado haya mambo ya mawasiliano hayajakaa vizuri.

Jamani serikali ni moja, mawaziri wote mnakutana katika Baraza la Mapinduzi, kwa nini hamuandai hili suala likafika kikomo angalau hili shirika likaanza kuja juu vizuri, itakuwa sisi tunalilaumu shirika lakini kumbe uwezo wa shirika wa kujiendesha ni mdogo mno hali ya kuwa nyenzo moja ya kutaka kulifanya shirika liweze kupiga hatua ni ofisi hii ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hili ni jambo zuri sana na linahitaji kupewa msukumo wa hali ya juu ili shirika lisije likamalizika.

Mhe. Spika, katika kutembelea shirika hili hasa eneo la *TVZ* Mkurugenzi wa ile ofisi ya shirika hata ile meza ya kukalia hana, hili ni tatizo. Kiti cha kukalia hapana, mtu mpaka anachukua *assets* zake nyumbani, ukiona huku nje utasema shirika zuri inadanda, inaita, lakini kumbe ni jeneza kilichobebwa ndani ni maiti muda mdogo tu kinanuka.

Kwa hivyo, jamani hii sio hali, hawa watu ni lazima wawezeshwe, haiwezekani kukaa katika maeneo ambayo yanafanya ile akili angalau ikawa inafanya kazi. Lakini mtu umemuweka pahali maana kama aliyetupwa tu nenda kule, kwa kweli itakuwa hatuwatendei haki watendaji wetu. Kwa hivyo, ili mambo haya yaende vizuri basi lazima watendaji tuwatunze na wao wawekwe katika maeneo ambayo yanastahiki kutokana na cheo chake alichonacho. Hilo ni jambo muhimu namuomba Mhe. Waziri alione sana hilo.

Mhe. Spika, nije katika Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani hii ni jicho la Serikali ya Zanzibar na eneo ilipo hoteli hii ni dira ya mji wa Zanzibar, lakini hali iliyofikia hoteli hii ni mbaya Mheshimiwa.

Hii hoteli ina muda mrefu haina Meneja, pana yule anayeitwa Naibu Meneja anakaimu sijui huu ni mwaka wa ngapi mpaka bwana yule anafikia kustaafu ni kaimu. Huku si kuwatendea haki, anamaliza kazi bado yumo katika kukaimu kaimu, haina meneja, hakuna bodi, sijui hii hoteli itakwenda vipi.

Kwa hivyo, mambo yetu wenyewe tunayakwamisha halafu tuwalaumu viongozi wa hoteli hii, hili si jambo zuri hata kidogo.

Mhe. Spika, ni vyema wanaohusika na uteuzi na mambo mengine ili hoteli iwe hai basi ifanyiwe kazi. Mhe. Spika, nakuona unatizama saa lakini naomba nimalizie na suala la mwisho la Makumbusho ya Mambo ya Kale.

Mhe. Spika, kitu makumbusho ni jambo zuri sana kwa sababu zile ni kumbukumbu za kizazi kilichopo na kijacho. Lakini nakuomba siku moja angalau fanya ziara uende haya makumbusho ya hapa Mnazi Mmoja, pale ni karibu mno tu uende ukajionee makumbusho ya pale. Mhe. Spika, pale hakuna kitu kunawekwa watu wanakaa tu hatima yake unawafanya wafanyakazi wetu ile taaluma waliyonayo waisahau, hapana kivutio cha kumvutia mtu pale. Lile eneo sijui kama serikali wameshasamehe ama vipi lakini hakuna. Ukiingia pale utakuta picha nne tano sita na labda jengine utakalolikuta pale ni ile ngoweo na kitanzi. Mhe. Spika, sijui ngoweo inafahamika?

Hata ukimleta huyo mgeni unaaza kumtisha maana anaona kwamba akiingia kule anakiona kitanzi kinamkalia hatimaye ataona kwamba anaweza akaja kufanyiwa yeye tatizo la kutundikiwa kitanzi,

hakuna historia yoyote inayoeleweka pale. Kwa hivyo, huku usigusie kuurejesha Utamaduni wa Mzanzibari kujua historia ya waliokuwepo kabla ya wao waliopo.

Kwa hivyo, ningeomba sana Shirika na ningelimuomba sana waziri anayehusika na swala hili zile kumbukumbu kama zipo zirejeshwe ili wafanyakazi pale waone kwamba ile pesa wanaipata kutokana na jasho lao wanaofanyia kazi pale. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutumia nguvu zake kunipa na kuweza kusimama hapa.

Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti ya utekelezaji ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Lakini vile vile kuchangia ripoti za utekelezaji za wizara mbili Wizara ya Habari na Wizara ya Mifugo.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu katika ukurasa wa nne wa utekelezaji wa maagizo ya Wizara ya Mifugo ambapo pana agizo namba moja.

Mhe. Spika, kamati ilishauri marekebisho ya Sheria ya Mifugo ili iweze kuwadhibiti wafugaji wakaidi ambao wanakwepa kuipeleka mifugo yao katika chanjo za kujikinga na maradhi ya wanyama.

Utekelezaji hapa tumeona hivi sasa sheria iko kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Kwa hili naomba iharakishe sana kuileta hii sheria, kwa sababu nikweli na nimeshuhudia wako wafugaji ambao ni wakaidi kipeleka mifugo yao katika chanjo.

Mhe. Spika, inapofika kipindi cha chanjo mfugaji anapembejewa kupeleka mifugo yake ipate chanjo lakini wengine wanakaa, hasa mifugo ya mbwa kwa kuzuia kichaa cha mbwa. Kwa kweli hili ni tatizo na ni lazima sheria iletwe na iwe madhubuti. Kwa sababu mimi binafsi nimewahi kumuona Punda Pemba ambaye anasadikiwa kuwa amepata ugonjwa huu wa kichaa cha mbwa. Mhe. Spika, kwa kweli hali ilikuwa hairidhishi Punda yule kafungwa lakini kaekewa vyuma na mawe anatafuna huku anatoka mate. Sasa sijui wale wenyewe walihofia baada ya kuacha yale mawe na nini atatafuna kamba aje akate.

Sasa Mhe. Spika, hili ni jambo la kuzingatia sana kwa sababu punda yule angeliondoka pale na akamtafuna binaadamu au mnyama mwengine basi kwa kweli athari kubwa ingelitokea hasa ukizingatia kuna mifugo ambayo tunaishi nayo kama hawa mbwa, paka wamo katika vijiji vyetu. Sasa ukiwa huu utaratibu wa kinga haukuwekewa sheria na wafugaji ikawa bado wanatabia ya kukimbia, hili kwa kweli tutakujafikwa na matatizo makubwa.

Nataka niende kwenye agizo namba nne Mhe. Spika, agizo hili lilieleza kuhamasishwa wafugaji ili wachukue tahadhari mapema na majibu ya wizara tuliyaona kuna namba moja walieleza chanjo zinazotumika kwa mifugo ya ngombe. Lakini sehemu ya pili hapa wameeleza chanjo zinzaotumika kwa mifugo ya kuku.

Mhe. Spika, hapa naomba kidogo nifahamishwe kwa sababu kuna hii chanjo ya mahepe tumeelezwa humu kwamba inatolewa kila baada ya miezi mitatu na kila vinapozaliwa vifaranga vipya. Kwa wafugaji wa vijijini ambao bado hawajawa na uwezo wala utaalamu kwa hili mimi silikubali, kama linafanyika. Kwa sababu wafugaji wamezoea au tumezoea kufuga pengine mwezi huu atatotoa kuku wake vifaranga vitatu au vinne, kweli pale kutakuwa na ufatiliaji wa kila kifaranga kinachozaliwa kupewa chanjo hii.

Kwa kweli hili Mhe. Spika, sifikirii kama liko sahihi isipokuwa naomba wizara kwa sababu kuna ufugaji ambao ni ufugaji mzuri wale wale kuku wetu wa kienyeji wanaweza wakaelimishwa wafugaji na wakazalisha pengine kwa kipindi kimoja, kuku hamsini basi watumie utaratibu huu wa kuwaelewesha wafugaji ili iwe hivyo. Lakini si kweli kila vifaranga vitano vitakavyozaliwa kuwa vinapata chanjo. Hili mimi silikubali.

Sasa naomba pia nije katika agizo namba saba hapa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya huduma za utabibu wa mifugo imeweka utaratibu kwa kila wiki mara mbili, Jumatatu na Ijumaa kutoa chanjo; ushauri na maelezo juu ya chanjo zote za kuku katika hospitali ya mifugo Maruhubi. Hapa imeonesha kama kwa upande wa Unguja ndio kuna siku mbili ambazo zimetengwa kwa suala hilo, lakini na kule Pemba wapo wafugaji sasa namuomba Mhe. Waziri atufahamishe kwa Pemba ni siku gani na siku gani, au wafugaji wa Pemba wanajiendea kwa sababu nilitegemea hapa itawekwa kwa upande wa Unguja Maruhubi, lakini na kwa upande wa Pemba itaelezwa.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye agizo linalohusu mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano. Katika Hospitali ya Chake Chake kuna mradi wa mbegu za ng'ombe kutoka Italia kwa ajili ya wafugaji wa Chake Chake, hapa naomba kupata maelezo nini mafanikio ya mradi huu kwa wafugaji wa Wilaya ya Chake Chake na je kuna uongezeko la uzalishaji wa ndama katika kipindi cha mradi tangu uanze.

Jambo jengine hapa ambalo niombe niliseme ni namna wizara ilivyotoa mashirikiano kwa uingizaji wa mbegu za ng'ombe wa aina ya Jazz kutoka nje kwa ajili ya Pemba. Kwa kweli hapa nina masikitiko makubwa wizara ilitoa usumbufu mkuba kwa mfanyakazi ambaye alikwenda Dar es Salaam kufuatilia hizi mbegu, mfanyakazi yule, aliyekwenda kule alipata usumbufu na kama si uzalendo wake na kwa kuwahurumia wale wafugaji basi naamini mbegu zile zingelikosekana.

Mhe. Spika, naombanitumie nafasi hii kumpongeza mfanyakazi yule kwa ustahamilivu wake mpaka akahakikisha mbegu zile zimefika katika kisiwa cha Pemba, na namuomba Mheshimiwa atueleze waziri analiambia nini Baraza kwa suala hili lililotokea.

Mhe. Spika, kwa kumalizia Wizara ya Mifugo naomba kidogo niende pale Mwenyekiti wa kamati aliposikitishwa na wataalam hawa wa mifugo wanavozichukua mbegu katika chupa za chai kwa kukosa chombo cha kuchukulia katika muda ule wanapokwenda kufanya kazi zao. Naomba nikueleze kama wewe umeona Chupa za Chai lakini mimi nimeshuhudia mbegu zikichukuliwa kwenye chupa za maji ya *drop* au uhai. Watalaalam wale wanatia maji wanazamisha mbegu halafu wanaenda katika hiyo shughuli ya upapishaji.

Mhe. Spika, hapa kweli pana umadhubuti hapa, Serikali hii Mapinduzi yamekuwepo tokea mwaka 1964 wakati mama yangu aliyenizaa ana umri wa miaka 8, nitizame mie sasa hivi umri niliokuwa nao nimeshazeeka leo ati madaktari wanatoka na mbegu za mifugo kwenye chupa ya maji, kwa kweli ni aibu tosha. Ni aibu kabisa mbegu zile ni mbegu ambazo zinatakiwa kuhifadhiwa vizuri, leo kila siku utasikia ng'ombe wanapandishwa lakini hawashiki, watashika vipi mbegu wanachukuliwa kwenye chupa ya *drop!* kwa kweli nasikitika sana.

Naomba sasa niende katika Wizara ya Habari, Mhe. Spika, Wizara ya Habari kuna agizo namba moja ya *ZBC* Mimi naishi Chake ambako kituo cha *TV* Mkanjuni kipo , kama miezi miwili iliyopita nilikwenda kituo hicho kulipia king'amuzi, lakini pia kuulizia kwa nini matangazo yanakatika katika. Naomba nitumie nafasi hii pia kuwapongeza wafanyakazi watano ambao walinipokea vizuri, lakini majibu yake hayakuniridhisha kwa sababu ni kweli wizara imejitahidi sana kuweka miundombinu ya *digital* na kujenga *studio* mpya ya kisasa ya *TV*. Lakini jibu nililolipata ni kwamba king'amuzi kile kinakatisha katisha matangazo kwa sababu mkonga wa taifa haujafanya kazi, na *studio* mpya pia haijaanza kutumika ikisubiri mkonga huo.

Mhe. Spika, naomba niulize ni hadi lini wananchi wa Pemba wataendelea kusumbuka kwa kusubiri kutumika mkonga huo, wakati wananchi wote wa Pemba tulishuhudia mkichimba Pemba nzima kwa kuwekwa mkonga, na naomba niulize kwa nini mkonga huo haujafika Mkanjuni?

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nimalize, nilipokwenda pale kwenye kituo cha *TV* Mkanjuni waliokuwa wakitoa maelezo ni wanaume watupu, wanawake ni wafanyakazi wa chini wakiwemo wafyagiaji na wafanyakazi wadogo wadogo, lakini maafisa wote waliopo pale *TV* Pemba

wote ni wanaume na wizarani. Kwa kweli Wizara ya Habari Pemba imetawaliwa na mfumo dume, jambo hili nililisema katika bajeti ya wizara hii mwaka jana utafiti niliofanya, hakuna marekebisho yoyote yaliyofanyika, hivi wanawake wenye uwezo kule Pemba hakuna? Au Mhe. Waziri na hili pia linahitaji ufadhili au pesa kiasi gani.

Mhe. Spika, tunavyosema hapa Barazani lazima wizara izingatie maoni yetu isitupuuze ikaona wanaume tu ndio wenye uwezo wa kufanya kila kitu. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hapa...

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbewanaotoka nje mara baada ya kumaliza dharura kwa muda mfupi basi warudi katika ukumbi huu tumalize shughuli hii.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Spika, na mimi nitachangia maagizo haya ya kamati kwa sababu maagizo ya kamati ndio maagizo ya wananchi, wananchi tunapowatembelea huwa wanatupa malalamiko yao na matatizo yao na kamati wanachukua matatizo haya kuja kupeleka katika Serikali.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu nitauanzia hapa katika sekta ya uvuvi, agizo namba moja ukurasa wa saba, kwa kusema kwamba:-

"Wizara ihakikishe kutengeneza *business plan* itakayoongoza katika mchakato wa ununuzi wa boti za wavuvi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, ambazo wizara na wavuvi wazoefu wanaweza kumudu kulinganisha na mahitaji yao ya Wazanzibari".

Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ambayo imezungukwa na bahari pande zote na ina uchumi wa samaki wengi sana ambao wanaweza wakatutajirisha, lakini mpaka leo wavuvi wetu bado wanavua uvuvi wa kimasikini.

Kwa hivyo, maagizo ya kamati ni kuwanunulia wananchi wetu boti ambazo zitakidhi haja kutokana na uvuvi wa bahari kuu, bahari kuu ndio yenye samaki wengi na ina samaki wakubwa. Hasa kutokana na hali ya nchi yetu ilivyo, idadi kubwa ya nchi yetu ni wavuvi lakini idadi kubwa ya watu masikini ni wavuvi kwa sababu hawana nyenzo zile za kuvuliya, kama inavyozungumzwa hapa kwamba watatengenezewa maboti ya kuvua uvuvi wa bahati kuu. Mimi naiomba serikali kwamba wananchi wetu wapewe nyenzo hizi kwa uhakika kama inavyoagiza kamati.

Kamati zinapoagiza matatizo ya wananchi ni wajibu serikali isikilize, kama upande wa kwetu Matemwe kuna wavuvi wengi sana lakini wanashindwa kwa sababu hawana zana za kisasa, uvuvi wanaovua hivi sasa ni ule wa kimasikini. Kwa hivyo, maagizo ya kamati yahakikishwe kwamba ni maagizo ya wananchi si maagizo yetu sie ni maagizo ya wananchi. Tunapokwenda kwa wananchi ndio wanatupa maagizo, wanatupa malalamiko na malalamiko tunaleta hapa. Kwa hivyo Serikali naiomba ihakikishe kwamba wananchi haya ndio wanayoyataka.

Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo agizo namba saba Kamisheni ya Utalii. Mhe. Spika, kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii, wawekezaji na mali zao. Lalamiko kubwa la wananchi wakati tunapokwenda kutembelea wanalalamika kwamba utalii umeletwa Zanzibar lakini wazaliwa hawapati kazi ndani ya utalii huo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hata huu ulinzi na usalama. Mlinzi wa nchi hii ni mwananchi, ukimpeleka mgeni katika hoteli hana usalama kwa sababu yule mtalii ameletwa pale kwenye kijiji. Kwa mfano, mtalii akija Matemwe mwenziwe ni huyu mtu wa Matemwe. Hivyo kama hakupewa mlinzi wa Matemwe hayupo katika usalama. Hivyo ninaiomba Wizara na Serikali waangaliwe wananchi kulinda mahoteli ndipo utakapopatikana usalama wa nchi. *(Makofi)*

Tutasema sisi hapa kwamba ulinzi na usalama, lakini ulinzi na usalama analetwa mtu wa Kenya atakulinda hapa. Kwa hivyo naomba Wizara na Serikali iangalie wananchi kulinda mahoteli. Wananchi wanatulalamikia kwamba kazi hawapati ndani ya mahoteli. Mahoteli Zanzibar yametuzunguka kama bahari pembe nne, bahari ikifurika yanaanza kuzamishwa mahoteli lakini wananchi hawapati kazi ndani ya mahoteli hayo na Serikali imeleta utalii ili kupunguza tatizo la ajira. Kila unapokwenda leo unaambiwa wananchi hawapati kazi za hoteli, wanaambiwa hawakusoma, kwa nini hii elimu gani inayotakiwa ndani ya hoteli.

Baada ya kumpelekea Mzungu bia na chakula, tena kuna elimu gani, baada ya kutia maji katika bustani pale kuna elimu gani, hata Wazanzibari wanaambiwa hawana elimu ya kutosha hawawezi kufanya kazi ya mahoteli. Kuna elimu gani katika hoteli. Elimu iliyokuwepo katika hoteli uweke vijiko pale, umma na kisu basi, jambo gani jengine. Kama akija mgeni ukimwambia madafu unamwambia panda nini, ninakuletea ninakuchongea unampa yamekwisha bwana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vijana wetu bwana wapo wengi hawana kazi na Serikali imeleta utalii kwamba vijana wapate ajira, lakini ajira anatoka mtu Kenya, anatoka sijui Arusha, anatoka sijui wapi. Sasa hawa hapa wafanye nini. Ndiyo tutawafanya kwamba wakavute unga pale Darajani hawana kazi, na ukimwambia anasema mimi sina bwana. Mhe. Spika, kwa hivyo ninaiomba Serikali kupitia Wizara inayohusika na utalii ihakikishe vijana wa Zanzibar wanapata kazi ya mahoteli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaendelea kwenye Chama cha Mpira *(ZFA)*. Zanzibar hivi sasa tuna timu nyingi za mpira. Hivi sasa mtoto wa miaka mitano anacheza mpira lakini bado ufanisi hatujaupata. Ufanisi ni kwamba Serikali bado haijakuwa pamoja na hizi timu za mpira. Mpira hivi sasa unataka, maana yake kila kitu sasa kinataka elimu.

Mhe. Spika, ninaiomba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ihakikishe inakaa pamoja na *ZFA* kuwapatia walimu wa mpira. Sasa hivi jamani mpira ajira. Tunasikia wenzetu huko Uingereza ananunuliwa mtu sijui dola ngapi sijui, lakini sisi hpa kila wingu likija la mvua sisi tunazidi kudidimia, kwa nini. Hivyo ninaiomba Wizara agizo la kamati lifuatwe, maagizo ya kamati ndiyo maagizo ya wananchi.

Sisi hatwendi pale tukachukua maagizo yetu wenyewe, tunachukua maagizo ya wananchi, wananchi wanapolalamika ndipo tunapoleta hapa. Ninaomba Mhe. Spika, Serikali pamoja na Wizara hii ihakikishe inaagiza makochi kutoka nje ya nchi ili kuwaelimisha vijana wetu angalau na sisi tufanikiwe. Leo tutakuwa hapa hapa tu, timu hazitembezwi popote, hazijafika hata Nigeria kutembea. Sijasikia mimi timu ya Zanzibar kwenda angalau Nigeria. Tanzania Bara hapo, Monduli, tunakuja hapa basi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninaiomba wizara ipanue wigo wa michezo. Vijana wapelekwe nje ya nchi. Kwani tunaona hasara gani hapa kuichukua timu ya taifa kuipeleka Brazil angalau mwezi mmoja, eeh! jamani wakenda kupata mazoezi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili kwa kuheshimu muda wako, ninaiomba Wizara hii iwapeleke vijana nje ya nchi na wao wakapate mazoezi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Karibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa dakika 10, baadae Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante. Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Subuhana Wataalla kwa kutujaalia kuwa hai na wazima tukiendelea na shughuli zetu katika chombo hichi. Mhe. Spika, nikushukuru na wewe vile vile kwa kunipa fursa hii kwa dakika chache kama nilivyokuomba. Ninakushukuru sana. Kwa sababu ya ufinyu wa muda. Naomba niende katika yale ambayo nimekusudia kuyasema.

Mhe. Spika, mchango wangu kwa sababu ya muda utajikita kwenye Wizara moja tu; Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Naomba nianze na na agizo la saba ambalo wengi wamelichangia Kamisheni ya Utalii kwenye ukurasa wa kumi wa ripoti ya utekelezaji ya Waziri ambapo agizo lilikuwa linahusu kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii, wawekezaji na mali zao.

Mhe. Spika, maelezo ya Mhe. Waziri yamesema suala hili limefanyiwa kazi kwa kuunda Kikosi Maalum cha Ulinzi wa Watalii ambapo kipo chini Mamlaka ya JKU. Lakini hapa ninataka niungane sana na Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Matemwe Mhe. Abdi Mosi Kombo kwamba walinzi wa wageni ni sisi wenyewe wananchi Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini niseme kwamba kama alivyosema yeye tutaendelea kuwa na changamoto kubwa ikiwa wananchi wenyewe hawaoni kama wananufaika na sekta ya utalii. Lakini hapa ninataka niseme moja tu mimi, kwamba leo tunapolalamika Wawakilishi wa wananchi kwamba Wazanzibari hawapati kazi, hili tujilaumu wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wala hakuna wa kulaumiwa na wala si Serikali.

Mhe. Spika, ilipokuja au ulipokuja Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kamisheni ya Utalii, nilisimama hapa nikataka kufanya marekebisho katika kifungu kusema kwamba kipa umbele cha ajira lenye neno "Mtanzania" liondoke iwekwe "Mzanzibari", Wajumbe wenzangu wakakataa humu ndani. Tukabakia wachache tunatetea. Sasa haya leo ndiyo matokeo tunayoyapigia kelele kwamba Wazanzibari hawapati ajira. Hakuna nguvu ya kisheria ya kumfanya Mzanzibari apewe kipa umbele katika ajira. Hili Mhe. Spika, niseme tutazungumzia usalama.

Mhe. Spika, biashara ya utalii kwa kawaida ni biashara *very sensitive*. Nchi inapoingia katika hali yoyote ambayo inaashiria hakuna usalama wa biashara hii inaathirika. Hali imekuwa nzuri sana, tangu tulipoleta maridhiano ya kisiasa ya mwaka 2009. Lakini inasikitisha tunapoelekea katika uchaguzi mkuu, hali hii kuna watu wanaonekana wamedhamiria kuichafua.

Mhe. Spika, kulikuwa na matukio katika Kisiwa cha Tumbatu kama wiki mbili zilizopita, ambapo inaonekana kuna watu, kwa sababu walikuwa na malengo waliamua kwanza kwenda kuashiria shari kwa kukata bendera katika matawi ya CCM ili kuhalalisha, baadae hatua nyengine kwa kukata bendera katika matawi ya CUF na ikasababisha vurugu. Lakini usiku wa kuamkia leo, Ofisi ya CUF ya Jimbo la Dimani imetiwa moto. Ninasema imetiwa moto kwa sababu haina umeme, hata ukasema inatokana na hitilafu ya umeme.

Mhe. Spika, matukio haya wanayoyafanya wanadhani yatawasaidia lakini anayekufa baharini mambo kama haya hayawezi kumsaidia hata siku moja, mfa maji ataendelea kushika maji lakini hayawezi kumsaidia hata kidogo.

Mhe. Spika, kwa hivyo hoja yangu ni kwamba tusipochukua hatua ya kuyadhibiti haya na wapingaji wa maridhiano wakapewa nafasi, tusidhani kwamba itasaidia kisiasa, haisaidii. Lakini tunaanza kupeleka ujumbe kwamba Zanzibar si salama na hii kuhusu utalii tunaozungumza hapa.

Mhe. Spika, hatuutendei haki wala hauwezi kusaidia na ukiathirika utalii, tutaathirika sote. Kama nilivyosema tusidhani matokeo kama haya yatamsaidia anayekufa maji akadhani kwamba ataokoka. Mhe. Spika, bavua likifika halina muokozi.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulizungumzia kwa haraka ni agizo la sita kuhusu Kampuni ya Zanzibar *Multiplex* na mradi wa *digital* Zanzibar. Hapa ninataka niungane na Mhe. Salma kwamba hili tutaendelea kuimba tu. Mradi huu hautofika pahali kwa sababu kuna ufisadi mkubwa katika mradi wa mkongo wa taifa ambao mpaka leo umeshindwa kufanya kazi.

Baraza hili miaka yake mitano yote tumekuwa tukiendelea kulizungumza, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa sababu sijui kunataka kufichwa jambo gani hapo au kunataka kulindwa watu

gani. Mradi huu wa mkonga wa taifa kama haufanyi kazi Mhe. Spika, suala la *digital* katika Zanzibar litaendelea kuwa wimbo wa taifa, hakuna chochote kitakachofanyika hapa tusidanganyane Mhe. Spika.

Mhe. Spika, na haya ndiyo matukio yanatokeo tunapojaribu kulinda watu na kukataa kuwaajibisha watu tukahakikishe tunalinda fedha za wananchi, malengo yaliyokusudiwa yakifikiwa. Tunapojaribu kuwanusuru watu matokeo yake nchi inaingia hasara, fedha za wananchi maskini wa nchi hii zinaendelea kutafunwa na tija iliyokusudiwa haifikiwi na mengi yataendelea kuathirika.

La mwisho Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza linahusu maagizo yanayohusu Shirika la Utangazaji. Hapa yameorodheshwa mengi na kwa sababu ya muda sitaki kuyasoma. Lakini vile vile kamati katika ripoti yake kwenye ukurasa wa sitini na tatu na sitini na nne umetoa maoni mazuri sana. Mimi ninaipongeza sana kamati imefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Lakini moja ambalo hawakuambiwa kuhusiana na Shirika la Utangazaji la Zanzibar na nimeona humu wameandika kuhusu Bodi. Mimi nikuombeni kamati kwa sababu bahati nzuri, mimi ni mjumbe wa Bodi ya *ZBC*, niiombe kamati iombe kukutana na Bodi. Hapa yote yanayotolewa, *management* itamdanganya Waziri na kamati itadanganywa. Hapa kilichopo, hili shirika mali ya mtu mmoja anayeitwa Hassan Mitawi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, utashangaa shirika limeundwa kwa mujibu wa sheria na linatakiwa liongezwe na Bodi katika baadhi ya masuala hasa yanayohusu sera. Bodi imezinduliwa 2013. Kama ingefuatwa sheria angalau Bodi ifanye vikao vyake, basi kungepaswa kufanyike vikao visivyopungua saba hadi sita vya kawaida, seuze vya dharura vikihitajika.

Mhe. Spika, nikiwa mjumbe ninataka nikuhakikishie kwamba kama kumewahi kuitwa vikao labda vitatu, tena vyote vya ajabu ajabu. Kimoja kiliitishwa wakati tupo katika Bunge la Katiba, kimoja tukaletewa karatasi nyumbani ili waridhie jambo. Lakini leo kwa sababu kunakuja bajeti, ndiyo juzi nimekabidhiwa hapa Barazani kabrasha lote hili kwamba kunaitwa kikao cha Bodi.

Kipindi hiki *management* ya shirika hasa Mkurugenzi Mkuu hataki shirika lile liendeshwe vizuri, na halitofanikiwa hata siku moja, tutasema sisi tukaingize fedha, sijui maagizo tele mengine. Humu imeambiwa kwamba kamati haijamshauri Waziri kuhusu hili, samahani Bodi haijamshauri Waziri. Bodi itamshauri vipi Waziri ikiwa Bodi haitwi kwenye vikao.

Mhe. Spika, bahati mbaya sana angalau ungekuwa na uongozi wa Bodi nao unashirikiana na wajumbe wake kuhakikisha kwamba inawajibisha *management*. Lakini ni wazi kunaonekana kumefunikwa mambo kusifanyike chochote. Wafanyakazi wa *ZBC* wanajituma sana, wafanyakazi hodari wangepata uongozi makini hawa wangeweza kulibadilisha sana shirika. Lakini haliwezi kubadilika chini ya Mkurugenzi aliyekuwepo hata siku moja. Tumelisema sana hili, tumemwambia sana Mhe. Rais kwa nini anamng'ang'ania mtu huyu, mimi sifahamu.

Sasa ninachosema kwamba kwa utaratibu huu kuwa shirika la umma limefanywa kama ni mali ya mtu binafsi anaendesha anavyotaka yeye, vyombo vilivyoekwa kisheria kuwa visaidie kuendesha shirika havipewi nafasi kufanya kazi yake. Tutadanganyana na nimpe pole sana Mhe. Waziri, nimwambie kwamba kwa hapa madam Mhe. Rais hajataka kumsaidia kwa kumpa Mkurugenzi Mkuu mwengine, hakuna kitakachobadilika katika *ZBC*.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Jussa tunakushukuru. Sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na baadae afuate Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utali na Michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na niungane na wenzangu wote kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kufika siku ya leo tukiwa na afya na uzima.

Mhe. Spika, michango ya Wajumbe mingi imetoka na mingi ilikuwa ni katika kufanikisha na kutuelekeza katika majukumu yetu ya kila siku ya utendaji wa kazi zetu. Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yetu, vile vile watendaji wa wizara hii.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja hii ya leo ambayo kwanza nianze na hoja ya Mhe. Farida Amour Mohammed. Yeye alitaka kujua wizara yetu kwa nini imepunguza kasi na vile vile kutokana na uhaba wa vifaranga; wafugaji wengi wamekuwa na tatizo la vifaranga.

Ninataka tumjibu tu kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kufanya ziara na kuwatembelea wafugaji wa samaki na kuwapatia ushauri wa kitaalamu, kufuga samaki bora wenye tija na kuhifadhi mazingira.

Aidha, tunamuomba Mhe. Mwakilishi tutafanya ziara ya pamoja na nitoe fursa hii kwa Wawakilishi wote ambao wapo tayari kufanya ziara katika majimbo yao, kwenye vikundi vyao vya ufugaji wa samaki basi tushirikiane kwa pamoja na yeye basi tukimaliza Baraza hili tutamualika ili tuwe pamoja tufanye ziara ya pamoja. Lakini isiwe tunakualika unatoa sababu kuwa huendi kule jimboni, tunashukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, jambo la pili nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Yeye alitaka kujua tu bei ndogo ya mwani lakini na vile vile soko hili la Malindi, yaani ambalo limekwama kwa sasa. Lakini tunataka kusema Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya kuwasiliana na *UNESCO* kupitia *Icomos*, ilitengeneza masharti ya mwanzo kuhusu michoro na baada ya kuhakikiwa kwamba michoro hiyo itafanyiwa marekebisho iliyoainishwa.

Hata hivyo, *UNESCO* iliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ieleze kama itafanya uchunguzi wa *physiology* kabla ya kuendelea na ujenzi. Wizara imeitisha kikao cha Makatibu Wakuu kwa hatua ya mwanzo na tayari inafanyiwa kazi na vile vile imebarikiwa na Rais wa Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nimjibu hoja nyengine Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe Mhe. Salim Abdalla Hamad. Yeye alitaka kujua tu baadhi ya vitu ambavyo vinaweza kusaidia wafugaji. Sasa nitamjibu baadhi na Mhe. Waziri ataendelea kumjibu.

Mhe. Spika, yeye alitaka kujua kwa nini baadhi ya wafugaji hawatumii chanjo. Hii ina sababu nyingi sana ingawaje hayupo hapa lakini tutamjibu hivyo hivyo, kwa sababu kwa faida ya wananchi. Chanjo zinazohitajika hapa Zanzibar ni ngapi. Ni chanjo za aina nyingi ambazo zipo hapa Zanzibar.

Jibu ni kwamba chanjo za aina zote zinazohitajika hapa Zanzibar kwa ajili ya mifugo zinapatikana, zinauzwa kwa gharama ndogo sana. Serikali ilibinafsisha jambo hili, likatoa matibabu na chanjo ilijivua ikalipeleka kwa wananchi wenyewe. Sasa kwa maana hiyo maduka mengi sana sasa yameanza kuuza na huo ni kujua ni jinsi gani utamaduni wa mifugo umeendelea katika kisiwa vyetu.

Moja ni kutokana na uuzaji wa chanjo, dawa na kuongezeka maduka ya madawa pamoja na maduka ya malishio au vyakula vya mifugo. Uone jinsi gani sasa lishe inapatikana kwa mifugo yetu.

La pili Mhe. Spika, alisema ni lini sera mpya italetwa hapa Barazani. Jibu ni kwamba sheria mpya ya mifugo italetwa Barazani baada ya kukamilika kwa taratibu zake. Tumezungumza mara nyingi sana wakati nikijibu maswali mengi, kuwa suala hili sasa hivi liko kwenye tume hii ya kurekebisha sheria na sisi kwa upande wa wizara limeshamaliza, tunategemea likitoka huko litapelekwa BLM kwa kubarikiwa na baadaye kuletwa katika Baraza lako tukufu.

Jengine alitaka kujua gharama za ujenzi wa kituo cha mifugo cha Unguja Ukuu na Kampuni gani inamalizia ujenzi huo. Gharama halisi ilikuwa ni milioni 15. Mwanzo kabisa tulijenga kwa kutumia mafundi wa wizara, lakini baadaye tukaona bado gharama inakuwa kubwa na tutakwenda kinyume na sheria ya manunuzi, ndio basi ikatuwajibika kuweza kuitisha *tender* na baadhi ya kampuni tayari tenda ile zimeshachukua na hii hatuwezi kuitangaza hapa, lakini baadaye kwa sababu ya kuwa bado hatujatoa kampuni ipi ambayo imepata tenda hiyo. Tutaitangaza baadaye na tutaileta kwa maandishi ya ile kampuni ambayo imepata tenda hiyo.

Hoja nyengine ilikuwa ni sababu zipi zimeshindwa ufugaji wa samaki kwa maji chumvi na sasa inaingia kwenye maji baridi. Nataka kusema tu serikali bado haijashindwa kwenye kushajihisha kwenye uvuvi huu wa maji ya chumvi na kwa sababu hiyo basi, hili lilitokea tatizo dogo la vifaranga na wenzetu wa *KOICA* wamekubali na tumeshatia saini kuweza kuweka huo mradi mkubwa wa *Hatcher* ya samaki ambayo tunaita *baby fish,* na hii itajengwa katika eneo la *Beit el Ras*, tukishirikiana na wenzetu wa *SUZA* kwa sababu tayari tunataka tufanye *research* mbali mbali ambazo zitaweza kudumisha ufugaji huu.

Vile vile tulitilia mkazo hili suala la samaki wa maji baridi. Suala hili tulilitilia mkazo kwa sababu vifaranga vyake vinapatikana kiuhakika zaidi, viko vingi na vinapatikana hakika tukaona tayari wananchi wetu wanaweza kufaidika juu ya hili. Moja katika hilo ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ameshajihisha sana na tayari ana mabwawa mawili hivi sasa anafuga wale samaki wa *flatfish*. Mhe. Makame Mshimba tukupongeze sana kwa kuwa mmoja wa washajihishaji.

Jambo jengine nijibu hoja ya Mhe. Saleh Nassor Juma, yeye alitaka kujua tu wale waanikaji wa dagaa, ambao anasema wanapata tabu wamefukuzwa katika maeneo tofauti, hakuna viwanda vya ajira, walipelekwa Maruhubi na Nyanjale. Nataka niseme tu wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Idara ya Mazingira zinashirikiana kwa pamoja ili kuona sehemu muafaka wapi itawapeleka na wao waweze kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi.

Hoja ya Mhe. Subeit Khamis Faki, kuwapatia taaluma zaidi wafugaji wa vikundi. Wizara inakubaliana na hoja hii ya Mhe. Subeit Khamis na taaluma inatolewa kwa vikundi kutokana na idadi ndogo ya vikundi vyenyewe vya ufugaji vilivyopo hapa nchini, basi tunaweza kuvisomesha na kuvipa ushauri mkubwa sana. Lakini jibu, tutaendelea na tutaona jinsi gani vikundi hivi tunavipatia taaluma ya nguvu zaidi.

Hoja ya Mhe. Mohammed Haji Khalid, yeye aliuliza tu maswali madogo madogo kupata ufafanuzi, alitaka kupata ufafanuzi wa tahadhari za ugonjwa wa mifugo ni nini. Jibu linakuja, tahadhari ya mapema maana yake ni kuendeleza utoaji wa taaluma na huduma za kinga ya tiba kwa kutoa chanjo matibabu na taaluma kwa wafugaji. Suala hili Mhe. Salma alitusaidia sana na tumpongeze sana, kwa sababu yeye anakaa na daktari karibu amejua mengi na amejua jinsi gani chanjo wafugaji wetu wanapokuwa wakorofi wa kutumia chanjo hizo. Mhe. Salma tunakushukuru nadhani na Mhe. Mohammed Haji Khalid alisoma vizuri sana juu ya suala hili.

Jengine alitaka kujua vipi chanjo ya ndui kwa mifugo mingine kama bata, bata mzinga na mifugo mingine kama ng'ombe imetajwa wengine hawakutaja. Nataka kusema tu matibabu ya ndui ni sawa sawa na kwa aina ya ndege wengine kama bata mzinga njiwa na kadhalika, na ile chanjo nyengine ya ng'ombe ni sawa sawa na mbuzi, kondoo, mbwa na kadhalika.

Mhe. Spika, jengine ni la Mhe. Hassan Hamad Omar yeye alitaka kutua tu uwezo wa boti zile ambazo zinakwenda bahari kuu kwa wavuvi wake, kwa sababu yeye ni mdau wetu mkubwa sana. Bila ya kutaja Kojani basi huwezi kusema Idara ya Uvuvi. Kwa hivyo, inabidi nikupongeze kwa hili kwa kufuatilia kwa ukaribu zaidi, na kutaka kujua huu uwezo zaidi wa wizara na Kampuni ya *KOICA*. Niseme tu uwezo wa boti zetu mpya zitakuwa na urefu wa mita 9 na mita 18, ambapo mita 9 zinao uwezo wa kuchukua wavuvi wanne na inaweza kukaa baharini kwa siku tatu, kuliko kwenda kidogo na tukaweza kurudi.

Vile vile zinaweza zikavua kilo 750 kwa hizo siku tatu za kwenda, kuanzia kilo 750. Lakini hizi za mita 18.5 zinao uwezo wa kuchukua watu 7 na pia inakuwa na uwezo wa kuvua tani 10 za samaki, zina uwezo mkubwa tunakuhakikishia. Vile vile zinaweza kukaa katika bahari kwa muda wa wiki mbili.

Mhe. Spika, niseme hayo tu machache, Mhe. Waziri anaweza akanisaidia mengi ya kujibu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, na naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii tukawa tuko hapa kutekeleza majukumu yetu ya serikali.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe, pia nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wa Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Pia niendelee kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Kwanza nianze na Mhe. Farida Amour Mohammed. Mhe. Farida alipokuwa akichangia alieleza kuhusu maeneo ya utalii, kisiwa cha Pemba, kisiwa cha Uvinje kuhusu mwekezaji, pamoja na Kisiwa cha Uvinje. Mhe. Farida Amour ni kweli mwekezaji huyu yeye mwenyewe binafsi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii pamoja na *ZIPA*, walikwenda kuzungumza na wananchi hao, wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kama ulivyoeleza kuwa Mwakilishi wa Wilaya ya Wete. Pia na mimi nikiwa ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na nikiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Pemba, pamoja na Kamisheni ya Utalii hapa Unguja Makao Makuu, tulikwenda kuzungumza na wananchi wa Uvinje. Nataka nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wa Uvinje tulizungumza nao kwa kina na tukatoa darasa tosha kwa wananchi wa Uvinje, wakiwemo wanawake, vijana wakiwemo na wazee wa Uvinje.

Mhe. Mwakilishi kwa kweli wazee wale, wanawake wale pamoja na wananchi kwa jumla walitufahamu vya kutosha na kwa kweli mwekezaji yule walimkubali. Wewe ulieleza kuwa kunajengwa hoteli au kuzungusha ukuta kwa mtutu wa bunduki. Hilo kama ni serikali sisi hatukubaliani nalo, kwa sababu kama tunavyojua matatizo mengi yanatokea kwa wawekezaji na watalii. Lazima pahali panapotokea mfarakano wowote au panapotokea maneno ambayo yakuwashtusha watalii ni lazima ulinzi utakuwepo na kwa kweli uliuliza kuwa ni hoteli ngapi ambazo zimejengwa kwa mtutu wa bunduki hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka kumuhakikishia kwamba hakuna hoteli hata moja na hilo ulilolieleza hapa, sisi wizara kwe kweli suala hilo hatunalo kwenye wizara yetu. Mhe. Mwakilishi nimuondoshe hofu hiyo, kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar alitangaza utalii kwa wote. Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum Wilaya ya Wete, Micheweni kuliwahi kuwekwa vikuta kwenye maeneo huru wakati wa Mhe. Rais Amani Karume. Wananchi wa Micheweni waliukataa utalii, kwa sababu kama tunavyojua utalii ndio pato letu kubwa hapa Zanzibar.

Pia Mhe. Rais alifanya ziara mwaka 2012, tulishiriki pamoja na watu *ZIPA*, akawaita watu wa Maziwa Ng'ombe pamoja na Kiuyu akawauliza vipi mnasemaje. Wakasema sisi utalii hatuutaki, lakini tunataka viwanda. Mhe. Rais akawakubalia, lakini kiwanda kinapokuwepo pahala popote pale lazima na utalii utakuwepo.

Sasa ukiwa ni Mwakilishi wa Wilaya ya Wete, nakuomba sana ukiwa wewe ni mwanamke, maendeleo yanapokuja tusimame pamoja na serikali, ili tuweze kuwaelimisha wananchi utalii wasiukatae, kwa sababu utalii unafaida zake. Kama nilivyokuambia tulitoa darasa na wakatufahamu

na walifurahi sana wao wenyewe binafsi watu wa Uvinje wakasema, Mhe. Naibu Waziri pamoja na uongozi wako tunakushukuru sana.

Sasa nakuhakikishia Mhe. Mwakilishi tukiwa pamoja tunatoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, tukiwa ni viongozi tuwaelimishe jamii ili waweze kushirikiana na serikali kuweza kukubali utalii, na kuweza kushirikiana na viongozi ambao wako madarakani na watalii. Kama tunavyojua watalii ni watu ambao wanaleta maendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea nije kwa Mhe. Rufai Said Rufai ambaye alizungumzia kuhusu makumbusho yaliopo Mnazi Mmoja. Mhe. Rufai Said makumbusho yale ni ya kihistoria. Vifaa vimo lakini kuna vifaa vyengine havijawekwa, tunakuhakikishia vifaa hivyo vitawekwa, kwa sababu kitu chochote kile kinapotengenezwa lazima uwende kuhamisha vifaa na kuweka sehemu nyengine, ili uweze kutengeneza nauweke vifaa kwa utaratibu maalum.
Huwezi kuchukua vifaa tu ukaviweka pahali ambapo havistahiki na vifaa vile ni vya enzi na enzi. Mhe. Mwakilishi tunakuomba sana kwa kushirikiana pamoja na kushirikiana na wizara, uweze kujua kwamba vifaa vile vipo na havijachukuliwa na mtu yeyote, ukitaka leo twende pamoja tukakuoneshe tutakwenda kukuonesha.

Mhe. Spika, niende kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe. Mhe. Mwakilishi alieleza kuhusu utalii, kwamba vijana wetu hawapati ajira. Mimi nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi Mkoa wa Kaskazini Pemba Hoteli ya Mantarif, wako vijana ambao wanatoka Makangale na wao wamesoma Chuo cha Utalii. Mhe. Mwakilishi mimi ninalokuomba uwashajihishe vijana wako, ili waweze kusoma na wao wapate ajira ambazo zitawaendeleza kwenye maisha yao.

Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana na wizara uje, kama ni kukuelekeza ni jinsi gani hao wanafunzi wako wapate kusoma katika Chuo cha Utalii, ili na wao wapate ajira kwenye mahoteli.

Mhe. Spika, mimi kwa kumalizia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Kabla sijawaita Waheshimiwa Mawaziri, niwaombe waheshimiwa wote walioko nje waje ili tumalize kazi hii. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ninayemuona anatoka, na yeye ningemuomba arudi ili tumalize hii kazi. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, baadaye atafuata Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuja hapa na kufanya majumuisho juu ya michango yote ya wajumbe ambayo imetolewa katika kuchangia hotuba hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa idhini yako kwanza niwatambuwe wale wajumbe wote ambao walichangia hotuba hii kwa maana ya kukosoa, kutoa ushauri au kwa namna nyengine yoyote ile ilimradi kuona kwamba wanapata jawabu sahihi kuhusiana na sekta hii ya mifugo.

Waheshimiwa Wajumbe wote takriban ambao wamechangia hotuba hii walikuwa takriban 13. Wa kwanza ni;

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ali Salum Haji
3. Mhe. Farida Amour Mohammed
4. Mhe. Nassor Salim Ali ingawa yeye hakugusa kabisa katika sekta hii.
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Hassan Hamad Omar
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Saleh Nassor Juma

10. Mhe. Rufai Said Rufai
11. Mhe. Marina Joel Thomas
12. Mhe. Salma Mohammed Ali
13. Mhe. Abdi Mosi Kombo
14. Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye yeye hakugusia kabisa katika sekta yetu.

Kwa hivyo, takriban wajumbe wote ambao walichangia walikuwa ni 13. Vile vile nisimsahau Mhe. Naibu Waziri ambaye na yeye alitoa mchango wake kwa kusaidia hotuba hii. Sasa kwa idhini yako Mhe. Spika, nianze kutoa jawabu ya majumuisho ya michango yote ambayo imetolewa na wajumbe.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha kwa mara nyengine tukiwa wazima na wenye afya bora.

Pili, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa michango yenu yote ambayo kwa kweli ilikuwa ni muhimu sana. Michango yote iliyotolewa ilikuwa na nia, kama nilivyosema awali ya kunisaidia mimi binafsi, lakini pamoja na watendaji wa wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi, na kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuwahudumia wananchi wetu, wadau wetu wa sekta ya mifugo na uvuvi.

Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu nitowe shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, kwa ushauri, nasaha na maelekezo waliyoyatoa katika kunielekeza wizara yangu na watendaji, ili kufikia malengo yetu ya kuwahudumia wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani. Tunaahidi wizara yangu itafuata maelekezo ya kamati kwa kadiri ya uwezo utakavyoturuhusu.

Mhe. Spika, hotuba kuhusiana na wizara yangu ilichangiwa na wajumbe kama nilivyowataja hapo. Kwa hivyo, sasa kama nilivyotangulia kusema awali nianze kutoa jawabu za hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza alikuwa ni mwenyewe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, na yeye hoja yake ilikuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifuatilie bei ya mwani duniani.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mashirikiana na Shirika la Chakula la Kilimo Duniani (*FAO*), ipo katika hatua ya maandalizi ya ziara ya kwenda Philippines, ili kufuatilia mambo ya kuendeleza sekta ya mwani pamoja na kufuatilia bei ya mwani duniani, safari ya kwenda Philippines inatarajiwa kufanyika mwezi wa Aprili mwaka huu.

Hoja ya pili, ya Mwenyekiti wa Kamati ni kuhusu suala la soko la Tumbe kupatiwa umeme wa uhakika. Jawabu ni kwamba suala la soko la Tumbe na uwekaji wa umeme, hakuna makubaliano yoyote ambayo yalikuwepo ndani ya mkataba baina ya wizara na mkandarasi. Kwa hivyo, suala la uwekaji umeme ni jukumu la serikali kupitia Wizara yangu ya Mifugo na Uvuvi, na hivyo ndio maana wizara yangu iliunganisha umeme huo kama ilivyopaswa. Kwa hivyo, suala la umeme halipo tena kwa sababu tumeshaliunganisha.

Vile vile Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aligusia suala lile la kuligawa shamba la Pangeni. Jawabu ni kwamba, ushauri wa kuligawa shamba la Pangeni hatuungi mkono, kwani wizara ina mipango ya kukifanya ni kituo cha utafiti na ni eneo pekee lililobakia kwa shughuli za utafiti wa mifugo.

Mjumbe mwengine alikuwa ni Mhe. Ali Salum Haji, na yeye alikuja na hoja, kwamba serikali imejipanga vipi katika kuwapatia mifugo wafugaji baada ya kuwapatia taaluma. Jawabu ni kwamba taaluma hutolewa kwa wananchi walio na mifugo, yaani wafugaji au wananchi wanaotaka kufuga na wapo tayari kununua mifugo hiyo. Wananchi hawa wakishapata taaluma wao wenyewe hununua mifugo kwa kuongozwa na wizara juu ya mifugo iliyobora wizara haina uwezo wa kuwapatia mifugo wananchi wote wanaohitaji mifugo.

Hoja yake ya pili nini maendeleo ya mradiwa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Jawabu ni kwamba mradi wa kopa ng'ombe na lipa ng'ombe unaendelea. Taarifa ya ng'ombe waliopewa wananchi katika mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe itatolewa kwa maandishi.

Hoja yake ya tatu mashamba ya mifugo kuvamiwa na wananchi. Jawabu mashamba yaliyovamiwa ni tatizo sugu la taifa ambalo halikabili wizara yangu tu. Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi tumeanza kuyapima maeneo yetu na kuweza kuyadhibiti, ushauri wa kuhama kutoka kituo cha upandishaji ngombe kwa sindano sio suluhisho la kuondoka kwa mavamizi. Namuomba Mheshimiwa alichunguze suala hili kwa makini kwa nini wamepata kiburi na kwa nini hawataki kuhama.

Mjumbe mwengine Mhe. Farida Amour Mohammed nae alikuja na hoja kadhaa nae kwamba. Wafugaji samaki wamekata tamaa kutokana na uhaba wa vifaranga vya samaki na upatikanaji wa chakula cha samaki. Hili Mhe. Waziri alilijibu lakini kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na kufanya ziara za kuwatembelea wafugaji wa samaki na kuwapatia ushauri wa kitaalamu.

Kuhusu ufugaji bora wa samaki wenye tija na kuhifadhi mazingira Mheshimiwa Mwakikilishi, tutamualika katika ziara zetu kama alivyoeleza Mhe. Naibu na tutakuwa pamoja ili kuona nini cha kufanya.

Mjumbe mwengine Mhe. Jaku Hashim Ayoub nae alikuja na hoja kwamba bei ya mwani ni ndogo ni hatua gani zimechukuliwa kuwasiadia wananchi. Jibu ni kwamba suala hili ni kama nilivyokueleza wakati nilipokuwa najibu suala la Mhe. Mlinde hilo nimeshalijibu. Kwa hiyo, hoja yake ya pili ni kuhusu ujenzi wa soko la samaki Malindi na suala la *UNESCO*.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya kuwasiliana na *UNESCO* kupitia *The International Council on Monuments and Sites* **(ICOMOS),** *UNESCO* imetengeneza masharti ya mwanzo kuhusu michoro baada ya kuhakikishiwa kwamba michoro hiyo itafanyiwa marekebisho ilioanishwa na *UNESCO*.

Hata hivyo *UNESCO* imeitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ieleze kama itafanya uchunguzi wa *archeology* kama haikuendelea na ujenzi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeitisha kikao na Makatibu Wakuu wa baadhi ya wizara ili kutafakari suala hili ili kuweza kutoa msimamo wa serikali.

Mhe. Salim Abdallah, Mjumbe mwengine ambaye na yeye alijibiwa vile vile na Naibu Waziri kwa hiyo sina haja ya kupoteza muda huo. Lakin vile vile yeye alikuja na baadhi ya masuala kama vile masuala ya chanjo kwa nini baadhi ya wafugaji hawatumii chanjo. Chanjo za aina zote zinazohitajika hapa Zanzibar kwa mifugo zinapatikana ingawa zinauzwa kwa gharama ndogo. Tatizo baadhi ya wafugaji huwa hawapendi kuchukuwa hadhari za kinga ingawa mifugo inapoumwa huchukuwa hatua za haraka kufuatilia matibabu alieza hapa Mhe. Salma kama kuna wafugaji wengine ni wakaidi kwa kweli.

Kwa hiyo, wizara yangu inaendelea kutoa taaluma hadi wafugaji watambue umuhimuwa chanjo kwani kinga ni bora kuliko tiba. Lini sheria mpya ya mifugo italetwa Barazani sheria mpya ya mifugo italetwa Barazani baada ya kukamilika taratibu za kisheria. Gharama za ujenzi wa kituo cha Mifugo cha Unguja Ukuu ni ngapi na kampuni gani ya kumalizia ujenzi huo.

Gharama hadi sasa zitaletwa kwa maandishi pili kamapuni ya kumalizia ujenzi bado imo katika mchakato. Sasa zipi kushindwa kwa ufugaji wa samaki wa maji chumvi zimeshaelezwa ufugaji wa samaki wa maji chumvi bado unaendelea ila tatizo kwa sasa ni mbegu za samaki tu nalo Mhe. Naibu Waziri ameshalitolea ufafanuzi, kwa hivyo sina haja ya kupoteza muda.

Mhe. Salim Abdallah ane amejibiwa na Mhe. Naibu Waziri Mhe. Hassan nae amejibiwa Mhe. Mohammed Khalid nae alijibiwa, Mhe. Saleh Nassor Juma nae amejibiwa, Mhe. Rufai nae halkahdalika, Mhe. salma nae alikuja na idadi ya ng'ombe walipandishwa kwa kutumia mradi wa *clays* ni wangapi katika Wilaya ya Chake.

Idadi ya ngombe waliopandishwa ni ngombe elfu tatu mia nne. Mjumbe mwengine alikuwa ni Mheshimiwa Salma yeye yeye alikuja na hoja za mfanyakazi aliekwenda kufuatilia mbegu za kupandisha ngombe kwa sindano. Jibu ni kwamba wafanyakazi wa Idara ya Uzalishaji wa Mifugo huwa wanalifatilia ujaji wa mbegu za kupandisha ngombe kwa sindano zilizotolewa na NG'Os ya Pemba *Island Support* .

Hiyo aliifanya kwa idhini ya wizara na kushauriana kila alipokwama katika kazi yake iliyotokea ni kwamba utoaji wa mbegu hizo ulichelewa kwa vile mzigo huo ulikuwa *address* kwa jina la mtu binafsi na sio wizara na ndio maana ikaleta tafrani. Mbegu hizo zimefika Pemba na zinatumika na stahiki zote za mfanyakazi huyo ameshalipwa.
Hali ya upandishaji kisiwani Pemba ipo katika hali nzuri kwa vile wana mbegu za kutosha na wanapatiwa *Liquid Nitrogen* kwa utaratibu mzuri. Kushika mimba ni suala linalohusisha mambo mengi na kutokana na takwimu tulizonazo ni kwamba asilimia 60% ya ngombe waliopandishwa hushika mimba. Hii ni takwim nzuri kupita sehemu nyengine zote ambazo wastani ni asilimia 57%.

Mhe. Spika, kulikuja na suala vile kuhusu doria za angani gharama za doria ya angani zilizofanywa na Mamlaka ya Bahari Kuu zilikuwa ni ngapi. Jawabu ni kwamba zilikuwa ni shilingi mia tatu arubaini na saba milioni laki saba hamsini na moja mia tisa na thalathini na tatu. Kwa ufupi huo ulikuwa ni muhtasari wa majawabu ya maswala ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo baada ya jawabu hiyo naomba kutoa hoja nashukuru sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa idhini yako naomba kutoa maelezo mbali mbali ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wakichangia ripoti ya kamati yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wametoa maelezo mengi na tumejitahidi sana kufanya muhtasari wa maelezo yenyewe, jumla ya wachangiaji wote 14 waliopata nafasi ya kuchangia wamegusa Wizara ya Habari Utamadini, Utalii na Michezo, na kwa kweli wamejaribu kugusa maeneo yote ambayo yamekuwepo katika maagizo ya kamati.

Kwa hivyo naomba nianze na Kamisheni ya Utalii ambapo waliochangia ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Marine Joel Thomas, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Abdi Mosi Kombo na Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Spika, naomba niseme kwanza kwamba si kila kitu ambacho kinafanywa katika sekta ya utalii huwa kimo katika usimamizi wa Wizara yangu, sekta ya utalii kuna mambo manne makubwa ambayo yanasimamiwa na Serikali yetu lakini yamegawika katika Wizara nne kama zifuatazo.

Ya kwanza masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na mapato yanasimamiwa na Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo inasimamia masuala ya uendeshaji na Utangazaji, masuala yote yanayohusiana na ajira yanasimamiwa na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma na masuala yote yanahusiana na ulinzi sasa yako chini ya Ofisi ya Rais, Kazi Maalum na Tawala za Mikoa.

Kwa hivyo, si kila kitu ambacho kinazungumzia masuala ya utalii yanasimamiwa moja kwa moja na Wizara yangu, kwa hivyo ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walifahamu hilo kwamba sekta ya utalii ni kweli kiujumla inasimamiwa na Wizara yangu lakini tumegawa majukumu katika Wizara nne, ili kuhakikisha kwamba inapata ufanisi zaidi.

Sasa katika suala la kutangaza utalii Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amelizungumza hili, nakuhakikishia kwamba Wizara yangu hili jukumu lake na inajitahidi na kama nilivyosema kwamba karibuni tunazindua rasmi Ofisi ya kuutangaza utalii nchini Mjini Mombai nchini India, ili kupata nguvu zaidi katika suala hili.

Katika suala la ulinzi kwa jumla tumepitisha sheria hapa kwamba JKU chini ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum hili ni jukumu lake, kwa hivyo wale wote ambao wamechangia masuala ya ulinzi ya watalii basi mratibu wa shughuli hizi ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, chini ya kikosi cha JKU kwa sababu tumepitisha sheria hapa na iko njiani kufanya kazi na kanuni zake.

Mhe. Farida Amour Mohammed amelizungumza suala la uwekezaji Fundo na Uvinje na hapa nataka niseme kwamba mpaka hatua hii suala hili liko chini ya ZIPA chini ya Wizara ya Fedha, lakini kiujumla na sisi kama waratibu wa shughuli tunashauriana. Kwa hivyo lilipotokea hili na Mimi natokea Wilaya ya Wete na nadhani Mhe. Farida angelikuja tukashauriana, lakini anaamua kwa sababu ameitwa na wapiga kura wake kulileta barazani si jambo baya ni pahali pake na kazi yake.

Kiujumla kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri alikwenda na mimi mwenyewe nilikwenda, nilichogundua ni kwamba wananchi wa Uvinje na Fundo bado hawajafahamu suala la utalii ule na bado hawajashirikishwa vyema kwa mujibu wa maoni yao. Kwa hivyo agizo ambalo nimelitoa kwamba hakuna sababu ya kufanya ulinzi mkubwa kama ule wakati wa ujenzi.

Bado turudi kwa wananchi tuendelee kuwaelimisha na naamini watafika pahali wataelewa, kwa hivyo hayo tumeelekeza na nadhani kwamba yanafanyiwa kazi na taasisi husika kimsingi kwamba wananchi wanaelekea kwamba bado hawajafahamu ni jukumu letu sote, kuwaelimisha na kwamba tumekubaliana na ZIPA. Tumekubaliana na Mkuu wa Mkoa kwamba jitihada zitafanywa kuwaelimisha wananchi bila ya kutumia nguvu.

Hivyo ndivyo tulivyokubaliana kwa hivyo bado Mhe. Muwakilishi naomba uchukue jibu hilo kwa wananchi wa Uvinje na Fundo kamba Wizara haina jukumu la moja kwa moja pale la kupeleka vikosi, kupeleka mtutu wa bunduki na kuweka wawekezaji bado taasisi nyengine zinazohusika, lakini kama Serikali ya pamoja tumekubaliana hilo tumefanya kikao pale kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa kwamba turudi kuwaelimisha wananchi bila ya kutumia nguvu. Hili tumelielekeza nadhani linafanyiwa kazi, kwa hivyo hilo ndio jibu ambalo la kulichukua sisi kama Kamisheni ya utalii, sisi kama Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo hatupendi kutumia nguvu katika masuala uwekezaji wa kitalii, kwa sababu sekta hii inahusu *hospitality* yaani ukarimu.

Kwa hiviyo ni vizuri kushirikiana na na wananchi kuelimishana, kufahamishana mpaka jambo tulifanye kwa pamoja, ili tukienda twende kwa pamoja kwa vile tumeelekeza, nadhani wahusika wanalifanyia kazi, ZIPA wanalifanyia kazi kwa mlengo wao na Mkuu wa Mkoa kule Pemba analifanyia kazi, kwa hivyo hili ndio jibu ambazo sisi tumesikitishwa na hilo lakini tumelielekeza vizuri na naamini linafanyiwa kazi.

Mhe. Ali Salim alizungumza suala la mkakati wa ulinzi nimeshalijibu. Mhe. Marina pia alizungumzia suala la ulinzi na ye linakwenda katika jibu hulo.

Mhe. Rufai Said Rufai amezungumza suala la kuhakikisha kwamba masuala ya utalii yanakwenda vizuri ushauri wake tunauchukua.

Mhe. Abdi Mosi na Mheshimiwa Ismail Jussa walizungumza kwa upana suala la ajira na kama ambavyo nimelizungumza kwamba masuala yote ya ajira yanasimamiwa na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais kazi na utumishi wa umma, tutashirikiana na wizara hiyo kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanafaidika na ua uajiri katika sekta ya utalii.

Mhe. Makame Mshimba, katika hoteli ya Bwawani amezungumza Mhe. Mshimba, Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mheshimiwa Rufai Said Rufai, ni kweli kwamba hoteli ya Bwawani sivyo ilivyokuwa enzi zile za miaka thamanini na miaka sabiini ni kweli, lakini sivyo pia ambavyo ipo vile ambavyo tumekabidhiwa sie.

Sisi tulikabidhiwa hoteli hii ikiwa na hali mbaya sana, kumbi zote zilikuwa mbovu, vyumba takriban vyote vilikuwa havifanyi kazi wafanyakazi wote ni wa kutwa, lakini leo ni tofauti na pale ambapo tumekabidhiwa sisi, kuna vyumba vingi vimeshafanyiwa marekebisho na wageni wanalala, kumbi zote zinafanya kazi ndio maana Salama Hoteli wakati wowote inafanya kazi. Mhe. Bhaa ananiangalia kuna mambo mambo pale yanafanyika yanakwenda vizuri.

Wafanyakazi takriban wote waliopo sasa tumewaajiri wa kudumu, kwa hivyo ni kweli kwamba upya wake na hivi sasa ni tofauti lakini pia tulipokabidhiwa na hivi sasa pia kuna *improvement* kubwa sana ambayo imefanyika katika kipindi hiki, na juhudi tunachukua kuhakikisha kwamba hoteli ya bwani inakwenda vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu ZBC takriban wachangiaji wote kumi na nne waliosimama walizungumzia suala hili, kwanza mimi naomba niipongeze ZBC kwa kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wanasikika Majimboni mwao hili jambo moja kubwa sana. Huko nyuma kabla ya awamu hii ya saba Wawakilishi tulikuwa tukiweka katika kipindi cha masuala na majibu, baadae kipindi kidogo cha nusu saa usiku.

Sasa Wawakilishi wanajimwaga saa 24 aliyeko Matemwe, aliyeko Micheweni wananchi wanamuona, kwa hivi hili ni jambo kubwa ambalo ZBC imefanya katika awamu hii, nadhani Mheshimiwa Mshimba akizungumza hapa akifika Kitope anaambiwa Mzee tumekusikia na tumekuona. Kwa hivyo hili jambo kubwa ZBC imefanya kipindi hiki, nadhani tuipongezeni sana.

Mhe. Spika, ili shirika la Utangazaji liwe na ufanisi linahitaji mambo manne, kwanza liwe na uwezo mzuri wa kutengeneza vipindi yaani *content production* maana yake ziwepo studio nzuri, ziwepo kamera za kisasa, ziwepo *link* na *logistic* za kufuatilia vipindi gari na mambo mengine.

La pili liwe na uwezo mzuri wa kutangaza vipindi, hivyo maana yake kuwa na studio nzuri na watangazaji wenye elimu, ujuzi na motisha mzuri.

La tatu liwe na uwezo wa kusafirisha vipindi hivyo kwenda kwa wateja yaani kuweko na *multiplex* kwa utangazaji wa sasa au minara kuhakikisha kwamba wateja vipindi vimewafikia, na nne kuwe na *management* nzuri.

Mhe. Spika, kwa kweli tumelirithi shirika hili likiwa na hali mbaya sana kwa kadri kipindi hiki tumefanya mambo mengi lakini hatujamaliza kazi, tumejaribu kuhakikisha kwamba kuna kamera nyingi za kutosha, tunazo kamera kama saba mpaka nane, kuliko kamera mbili tulizorithi zimetusaidia sana.

Tumehakikisha kwamba sasa hatutumii matangazo kupitia Zanzibar *cable* tumenunua *link* yetu wenyewe ambayo inasababisha kupeleka vipindi hazijatosha, lakini ni mwanzo, tumehakikisha kwamba tunajenga Studio mbili za kisasa moja Unguja na moja Pemba, studio za kisasa kabisa zimetugharimu sana. Lakini ili kusafirisha mawimbi na matangazo kwa wateja, tumejenga miuondombinu ya *multiplex*

Ili kusafirisha mawimbi na matangazo kwa wateja tumejenga miuondombinu ya *multiplex* kuhakikisha kwamba wateja wanapata huduma za kutosha. Jambo ambalo mheshimiwa tunalifanyia kazi hivi sasa ni kuwafundisha wafanyakazi wetu. Mhe. Spika, mimi mwenyewe nimeonana na Mkurugenzi wa mafunzo wa sauti ya Ujerumani Ofisini kwakwe, kumuomba kwamba atusaidie mafunzo ya wafanyakazi wetu, ombi ambalo amelipokea na amelianza vizuri sana.

Kwa hivyo ni kweli kwamba wafanyakazi wetu hawana ujuzi mzuri katika kutangaza, lakini tunashukuru sana Shirika la Utangazaji la Ujerumani kwamba ombi letu wamelichukua na wameanza kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wafanyakazi wetu.

Jambo ambalo tunahakikisha kwamba tunaliimarisha hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tuna uwezo wa kupeperusha mawingi yetu kwa kisasa, kuhakikisha kwamba matangazo yote yanawafika wateja wetu katika majumba yao bila ya matatizo. Ndio maana tukahakikisha kwamba kama ambavyo alivyosema Mhe. Salma Mohammed Ali na Mhe. Ismail Jussa kwamba tunajiunga na mkonga wa taifa. Hili tunalifanyia kazi ili shughuli za utangazaji ziende vizuri, lazima ama za usasa ama na satalaiti au na mkonga wa taifa.

Mhe. Spika, mkonga wa taifa umejengwa, umeanza matumizi na sisi Wizara ya Habari tumeshakaa na wataalamu wa mkonga wa taifa vikao viwili vitatu, na tayari wameshaleta mapendekezo yao kwetu namna gani Shirika la Utagazaji la ZBC pamoja na *Zanzibar Multiplex,* vituo vyote vitaunganishwa na mkonga wa taifa kazi ambayo tunaifanyia kazi hivi sasa.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna malalamiko kwamba ZBC inakimbiwa na wasikilizaji. Inawezekana hilo lakini mwishoni mwa mwaka jana Shirika la *Synovate* la Kilimwengu lilifanya utafiti hapa Zanzibar. Katika mashirika yote ya habari kuangalia ni Shirika lipi linapendwa na wasikilizaji yaani lina wasikilizaji wengi zaidi. Ripoti tuliyoipata na shirika hili ni kwamba Shirika la kwanza ni ZBC, Shirika la pili ni ZENJI FM, Shirika la Tatu ni Al- Nuur.

Kwa hivyo kunambia kwamba Shirika hili linakimbiwa na watangazaji sijui kwa takwimu ipi. Lakini hili Shirika la Kilimwengu ambalo limefanya study yake na likatupa ripoti kwamba kwa Zanzibar ZBC ndio Shirika ambalo linasikilizwa, linaangaliwa na watazamaji zaidi.

Sasa hiyo ndiyo data, sasa ukisema mimi nina televisheni na redio nyumbani kwangu, mwanangu ananambia funga inawezekana kwa sababu utafiti unaonyesha kwamba kila umri wa watu wana-*interest* zao katika chombo cha habari. Watu wazima wanapenda habari na vipindi vya kuelimisha, watoto wadogo wanapenda katuni na michezo. Vijana wanapenda michezo na muziki.

Sasa inategemea *interest* na ndio sisi tukaanzisha Zanzibar *Multiplex* kuna *channel* chungumzima kutegemea na mtu anataka kuangalia nini. Sasa kijana akitaka, tumeweka makusudi mle katuni, tizama katuni, muache kijana atizame mziki, mzee unataka taarifa ya hatari, *program* za *education* zipo *channel*, unataka mambo ya dini, mambo ya ustadhi na maamira na wao wana sehemu zao. Haya ndio sababu tumefanya hivi makusudi ili kuwapa watu wetu au wananchi *choice* kubwa zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu ZBC II ipo kwa majaribio, inapatikana katika king'amuzi chetu cha Zanzibar *Multplex*. Lakini ni kawaida ya vipindi vya majaribio huwa vinaanza kwa muziki, dunia nzima. Wakati siku zote hiyo ndiyo kawaida hatuwezi kuwa na mambo mengine. Na wakati huo huo tunapata maoni ya wateja wetu. Mimi nafurahi kwamba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wametwambia kwamba ZBC II isiwe na yale mambo ya vijana vijana. Maoni yao tumeyachukua na tutayafanyia kazi wakati itakapokuwa katika *full swing*

Mhe. Spika, kuhusu posho la waandishi wa habari ni kweli Mhe. Spika, kwamba hili limezungumzwa na wachangiaji takriban wote. Lakini si posho la waandishi wa habari tu lakini maslahi ya jumla ya waandishi wetu. Hili katika serikali tumeliona na kijumla serikali imekubali kutoa posho maalum kwa ajili ya waandishi wa habari. Waziri wa Fedha keshapewa agizo hilo na litakuwemo katika bajeti inayokuja ya mwaka 2015/16.

Mhe. Spika, kuhusu wanaokuja Baraza la Wawakilishi. Nilipewa maagizo ya Kamati kwamba watendaji wetu wameanza vikao, Makatibu Wakuu wetu wamekutana na sasa zamu yetu Mawaziri. Dalili inaonesha vizuri katika maandalizi ya bajeti hii, watendaji wa ZBC na watendaji wa Baraza la Wawakilishi wameshaanza kukutana, ili kuhakikisha kwamba maandalizi haya yanayofanywa ya bajeti ya 2015/16 basi wanaangalia vipi Baraza litaweza kulipia matangazo yake.

Mhe. Spika, mimi nawashukuru sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa namna ambavyo wanaumwa na hili. Nahakikisha kwamba kwa vile sauti zao zimesikika na uongozi wa Baraza la Uongozi wa Serikali na Uongozi wa Wizara naamini kwamba katika mwaka ujao wa fedha 2015/16,

basi Baraza la Wawakilishi litaanza kulipia japo kidogo au tuseme kuchangia japo kidogo katika masuala ya vipindi hivi ambavyo vinaoneshwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa kweli ni kweli kwamba ZBC katika kutangaza vipindi hivi inatumia sana. Inatumia vifaa vingi na inatumia umeme mwingi. Nataka nisehe kwamba hivi sasa ZBC kwanza nimerithi deni la umeme la milioni mia tano (500). Wakati ZBC inaundwa nimerithi deni kutoka Radio Zanzibar na Televisheni Zanzibar deni mia tano na hivi sasa limekuwa mia sita. Kuna wakati ZECO wanakata umeme inakuwa kukimbizana.

Mhe. Spika, kuna tatizo kubwa, sasa tukipata malipo haya naamini kwamba ZBC itakuwa na uwezo wa kulipa madeni yake mbali mbali, kununua vifaa vipya vinavyokwenda na wakati, kuwalipa vizuri wafanyakazi wake, lakini pia kulipa maposho mbali mbali ikiwemo vijana wanaokuja hapa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo tuna deni kama la vikao vinne la shilingi kama milioni kumi na sita nimetakiwa nijibu. Tunaangalia utaratibu wa kuvilipa kabla ya vikao vya bajeti hali ikiwaruhusu. Lakini hali ya fedha ikiwa ngumu kama hivi inavyoweza kuendelea, sitoweza kulipa madeni ya maposho, nikaacha watu wa Shirika la ZECO wanikatie umeme, hapo lazima uamue jambo la kufanya ama uwalipe watu maposho au upunguze angalau kidogo kwa Shirika la Umeme ili vipindi viendelee kuwemo.

Mhe. Spika, kuhusu Mhe. Ismail Jussa Ladhu maoni yake kuhusiana na vikao vya Bodi tumeyachukua na tutayafanyia kazi. Wazo lake kwamba Kamati ikutane na Bodi ni jambo zuri na mimi mwenyewe katika mwezi wa nne, ninahakikisha kwamba nitakutana na Bodi kuwasikiliza kwa ujumla matatizo yao na *management* yake ili tufanye marekebisho ya jumla. Lakini kama suala ndio hivyo inaonekana kama *management* na Bodi ipo mbali kidogo jambo ambalo siwezi kuliruhusu liendelee. Nitakutana na Bodi peke yake, halafu nitakutana na Bodi ya *management* kuangalia vilio hivyo ili tuweze kurekebisha hali.

Mhe. Spika, kuhusu habari maelezo kulikuwa na suala la *stand* moja au vifaa vichache ambavyo Mhe. Ali Salim Haji, wa jimbo la Kwahani aliuliza ni kwamba vifaa hivi vilivyonunuliwa vilikuwa kwa ajili ya kuengeza tu vile vifaa vilivyopungua. Lakini kwa ujumla hivi sasa Idara ya Habari Maelezo inaseti tatu zilizokamilika kwa ajili ya kufanya shughuli mbali mbali wakati mmoja. Kwa hivyo vile vifaa vilivyonunuliwa vilikuwa vyakuongeza tu sio kwamba ndio vifaa ambavyo tunavyo. Tumejiweka vizuri katika Idara ya Habari Maelezo na tuna uwezo wa kuhudumia *functions* tatu kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, kuhusu sekta ya michezo. Kwanza naomba nichukue fursa hii kwa kupongeza (CHANEZA) Chama cha Netball Zanzibar. Kwa namna ambavyo ilikuwa na migogoro ya siku nyingi lakini sasa migogoro yao wameizika na mafanikio yao yameanza kuonekana. Wiki iliyopita walikuwa wenyeji wa mashindano ya Afrika Mashariki ya mchezo wa Netball hapa Zanzibar. Jambo ambalo nalijafanyika siku nyingi. Lakini kwa sababu wamezika tofauti zao, uongozi wanashirikiana Baraza lao la Michezo mambo sasa yameanza kubadilika na CHANEZA wanakwenda vizuri. Mbali ya hilo hivi sasa Zanzibar ni mwenyeji na ndiye Rais wa Vyama vya CHANEZA vya nchi zote za Afrika Mashariki.

Kwa hivyo ni jambo la kujivunia kwamba tumepewa taji hilo na kwamba katika mashindani yaliyopita nchi ya Kenya ndiyo iliyotoa ubingwa lakini kwa wanaume timu ya Polisi Zanzibar ndiyo iliyoletwa ubingwa kwa mashindani hayo. Katika hili naomba niseme kwamba kuna umuhimu wa vyama vyote vya michezo kuondokana na migogoro kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao bila ya matatizo, wasikubali kutumiwa na watu walionje ya uongozi. Hiyo ndiyo pekee.

Mhe. Spika, ushauri mwengine uliotolewa wizara kuhakikisha kwamba ZFA inaondokana na migogoro, tunauchukua ushauri wake na tutaendelea kuufanyia kazi.

Mhe. Salim Abdalla alizungumza kuhusu majenereta yaliyokuwepo ZBC kwa nini Pemba hakuna? Nataka nimwambie kwamba Pemba kuna majenereta matatu mawili mapya, moja lipo Bungala na moja lipo Kichunjuu na moja kongwe lipo Mkanjuni, lakini yote yanafanya kazi vizuri.

Kuhusu chuo cha habari Mhe. Nassor Salim (Jazira) ushauri wako tumeuchukua sana. Tutajitahidi jengo lile likamilike kwa wakati. Jengo limefikia asilimia 70, jengo lina madarasa matano. Ofisi tatu na vyoo na mambo mengine. Kule kulikuwa na Ofisi mbili, madarasa mawili. Tunaamini kwamba tunahitaji milioni 30, au 35 hivyo. Maombi haya yapo Wizara ya Fedha, Mhe. Waziri wa Fedha ananambia akishamaliza kulipa mishahara na baada ya kumaliza kikao hichi kidogo maana kipo kwenye shingo yake. Kikimaliza hiki basi atanipatia milioni 35 kumaliza jengo lile la Chuo cha Habari ili mwezi wa 5 kama tulivyopanga tuhakikishe kwamba jengo lile linahamiwa.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri wa Fedha hali yake itakuwa tayari kama baada ya kikao hiki mambo yangu ya milioni 35 yatakuwa mazuri basi jengo lile la Chuo cha Habari, tukijaaliwa mwezi wa tano litakuwa limemaliza na limehamiwa rasmi.

Ofisi ya Zanzibar leo Mhe. Jaku Hashim ni kweli hairidhishi, haipo mahali pazuri, serikali imo katika hatua ya mwisho ya kuhakikisha kwamba wanatafutiwa eneo jengine kwa ajili ya kufanya shughuli zao.

Kuhusu makumbusho kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri pale palikuwa na matengenezo makubwa kila mtu anayepita pale nje ataliona kwamba lile jengo la makumbusho yalikuwa na matengenezo makubwa, halikuwa vile, lilikuwa lina matengenezo makubwa sana. Katika matengenezo yake yale ilibidi tuhamishe kila kitu tupeleke Beitil-ajaibu.

Mhe. Spika, sasa Betil-ajaibu nalo tunapanga matengenezo makubwa, kwa hiyo, tutarudisha baadhi ya vifaa ambavyo tulivyovihamishia kule na vile ambavyo tulivyovitoa kutoka Betil-ajaibu tukavipeleka pale. Kwa hivyo baada ya muda mfupi jengo lile ambalo limefanyiwa matengenezo makubwa lipo zuri, halivuji tena litasheheni mambo mbali mbali ya makumbusho.

Mhe. Naibu Spika, masuala ya Z-MUX nishajibu kama nilivyosema kwamba tutahakikisha tunashirikiana na Wizara ya Fedha na Afisi nyengine kuhakikisha kwamba tukijaaliwa mwakani Z-MUX na ZBC inajiunga vizuri na huduma ya mkonga wa taifa.

Mwisho kuhusu mfumo dume ambao Mhe. Salma Mohammed amekuwa anatulalamikia sana. Ni kweli kwamba Mhe. Salma Mohammed alizungumza wakati wa bajeti. Lakini hatukulitupa kama alivyosema katika mchango wake, wala hatupuuzi. Sisi hatuna kawaida ya kupuuza hata kidogo maoni na maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza. Tunaamini kwamba Baraza hili ndilo linaloisimamia serikali, Baraza hili ndilo linalosimamia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, na chini ya usimamizi wangu maagizo mbali mbali yanatolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunayafanyia kazi.

Mhe. Spika, lilipotolewa agizo hili tulichofanya ni mambo mawili kwanza sio kwamba tunaweza tu kumchukua mwanamke kwa sababu ni mwanamke tukamuweka katika daraja la chini. Lazima tumuandae kwanza, kwa hivyo wakati wa bajeti Mhe. Salma Muhammed alitupa hili agizo. Sisi kupitia Afisi ya Katibu Mkuu ameangalia wanawake gani na wana uwezo gani, wanaweza wakapewa mafunzo ya uwongozi halafu wakapewa mafunzo.

Mhe. Spika, kuna mwanamke mmoja Pemba wa Wizara ya Habari, Maelezo ana Diploma ya Uwandishi wa Habari akapewa mafunzo ya awali ya uongozi, anaendelea kupewa mafunzo ya uwongozi ili kutayarishwa kupewa nafasi katika Idara yake. Pia katika ZBC yuko Mwanamke ambaye ana Digirii ya Uandishi wa Habari naye Shirika linaangalia kumpa mafunzo ya awali ya uongozi, ili baada apate daraja ambayo inayohusiana na uafisa katika shirika lake.

Mhe. Spika, kwa hivyo Mheshimiwa maagizo ambayo ametupa Mhe. Salma Muhammed wakati wa Bajeti tunayafanyia kazi hivi sasa, ili kuona kwamba tunawaandaa ili tutakapokuja kuwapa nafasi waweze ku - *deliver*. Isije kuwa mnaona mumewapa nafasi wanawake lakini wanaonekana hawafai. Tunawaandaa kwanza ili tutakapowapa nafasi waweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, kwa kweli kama nilivyosema kwamba michango ya Waheshimiwa yalikuwa mengi na yote yamelenga katika kuiyandaa wizara kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Yote ambayo wamechukua tutaendelea kuyafanyia kazi zaidi na tutaendelea kushirikiana na kamati ya Mhe. Mlinde Mabrouk Juma ambaye ananisaidia sana katika kuona Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, imeweza kufikisha malengo yake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maelezo haya.

Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Mifuto Utalii na Habati: Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijaalia kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu, tukifanya majumuisho kuhusu michango iliyotokana na ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa mara nyengine tena kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako hili kufanya majumuisho ya ripoti yetu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia katika ripoti yetu ya Kamati, ili kuboresha na kusisitiza kwa yale yote ambayo Kamati waliyafanyia kazi. Lakini pia niwashukuru Waheshimiwa wote ambao hawakupata nafasi ya kuchangia kwa mashirikiano yao waliyotupa tukiwa katika kazi za Kamati, lakini pia tukiwa katika Baraza hili ambayo yameisaidia Kamati kuwasilisha ripoti hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia katika ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, ripoti yetu hii imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 14 na Mawaziri wawili na Manaibu Waziri wawili. Mhe. Spika, naomba nianze kuwataja kwa majina yao kama ifuatavyo:

1) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2) Mhe. Ali Salum Haji
3) Mhe. Farida Amour Mohammed
4) Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira)
5) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6) Mhe. Salim Abdalla Hamad
7) Mhe. Hassan Hamad Omar
8) Mhe. Mohammed Haji Khalid
9) Mhe. Saleh Nassor Juma
10) Mhe. Marina Joel Thomas
11) Mhe. Rufai Said Rufai
12) Mhe. Salma Mohammed Ali
13) Mhe. Abdi Mosi Kombo na;
14) Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Kama nilivyokwisha kusema kwamba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na manaibu wao walichangia ripoti yetu hii.

Mhe. Spika, baada yakuwatambua Waheshimiwa Wajumbe waliochangia ripoti hii ya kamati yetu, sasa naomba nikumbushe tu yale maeneo ambayo waheshimiwa wajumbe wengi waliyachangia.

Kwanza deni la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, kwa sababu ZBC ni Shirika la Serikali linalojiendesha kibiashara kama yalivyo mashirika mengine ya Serikali ambayo hutegemea fedha zinazotokana na mapato yao ya ndani, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zikae pamoja, ili kulipatia ufumbuzi suala hili la fedha kwa haraka ili ZBC iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Lakini naomba ifahamike kuwa suala hili sio tu kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, bali pia kwa Taasisi zote za Serikali zinazopatiwa huduma na ZBC.

Mhe. Spika, tunaendelea kusisitiza kuwa taasisi zote iwe za Serikali au zisizo za Serikali zihakikishe kwamba zinalipa kwa wakati lakini pia tunautaka uongozi wa Hoteli ya Bwawani kuwachukulia hatua za kisheria wale wateja wake wote wanaodaiwa.

Mhe. Spika, pia ufugaji wa samaki lilizungumziwa sana, wajumbe pia walilizungumzia suala hili na wameitaka Serikali kutoa mashirikiano na kuratibu ushirikiano wa karibu sana kwa wafugaji hawa, ili nao waendelee kuwa na moyo wa kuendelea na ufugaji huu wa samaki.

Mhe. Spika, migogoro ya ZFA imezungumziwa lakini nashukuru pia Mhe. Waziri ameitolea ufafanuzi mkubwa na mpana zaidi na mimi naomba tu nizungumzie kidogo. Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia kwa masikitiko makubwa sana suala hili, tunaendelea kuitaka Serikali izingatie na ifanyie kazi maoni yaliyotolewa na Kamati ili kuokoa soka la Zanzibar.

Mhe. Spika, ujenzi wa soko la Malindi limezungumzwa hapa hususan Mhe. Jaku lakini Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi, lakini pia naomba na mimi niongezee kidogo, suala hili pia lilizungumzwa na waheshimiwa wengine lakini kwa masikitiko makubwa sana na kuitaka Serikali ichukue hatua za haraka, ili kupatiwa ufumbuzi wa suala hili na ujenzi huo uanze kwa haraka sana kwa manufaa ya watu wetu wa Zanzibar, na ni kweli kabisa tunakubaliana naye suala hili linahitaji kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, zao la mwani limezungumziwa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe lakini suala hili pia lilizungumzwa na ni kweli bei ya mwani bado ndogo sana ukilinganisha na ugumu wa kilimo chenyewe. Tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kulitafutia ufumbuzi suala hili ili wakulima wa mwani nao wafaidike na kazi zao za kila siku.

Suala la ulinzi wa watalii pia limezungumziwa, Mhe. Spika, suala hili limezungumzwa na ni kweli kabisa lina umuhimu mkubwa katika kukuza utalii hapa Zanzibar ambapo sehemu kubwa ya mapato yetu tunategemea utalii huu na sekta ya uvuvi pia pamoja na maelezo mengi yaliyotolewa na Mhe. Waziri.

Pia waheshimiwa wengi walizungumzia sana kuhusu suala la uvuvi na umuhimu wake hapa Zanzibar. Ni kweli kuwa Zanzibar ni kisiwa ambacho kinategemea raslimali ya bahari hivyo, basi sekta hii inahitaji kupewa kipaumbele ili kuinua uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad alituuliza hapa kamati kwamba ukaidi gani wa wafugaji ambao unapelekea kuwa wasipeleke mifugo yao kwenye chanjo. Hii ukiangalia ni kweli kwamba baadhi ya wafugaji hawana hii tabia ya kupeleka mifugo yao kwenye chanjo hasa wafugaji wa mbwa. Wafugaji wa mbwa wamekuwa wakiachia mbwa wao na kwa kuwa tu eti wanatakiwa mchango mdogo ambao ungeweza kuwatibu mbwa wale na kupelekea wananchi wetu kutokudhuriwa na mbwa hawa mitaani.

Kwa hivyo nadhani sisi Waheshimiwa Wawakilishi mbali ya kuwa Wizara inatoa elimu vipindi mbali mbali vya kwenye radio na televisheni, na sisi wawakilishi tuchukuwe juhudi kwa kuwa sisi ndio tunaoishi na hawa wafugaji kuwaelimisha, na kuwa nao karibu ili kama tabia hii, bado wanayo waiache na wapeleke mifugo yao kufanyiwa chanjo, ili tuishi maisha salama. Tusije tukadhuriwa na wanyama ambao ni sisi wenyewe ndio tunaowafuga.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuchukua fursa hii kwa kunipa nafasi hii na pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ninafikiri muda uliobaki hautuwezeshi kuendelea na kazi nyengine na inabidi sasa shughuli zetu tusitishe mara baada ya tangazo hili.

Waheshimiwa Wajumbe kuna tangazo moja ambalo ni taarifa ya kisomo cha arubaini. Waheshimiwa Wajumbe familia ya marehemu Mzee Awadh Salmin Awadh inapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe na watendaji wote wa Baraza hili arubaini ya marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin, itakayofanyika siku ya Jumamosi tarehe 28/03/2015 baada ya sala ya alfajiri hapo nyumbani kwao Mpendae. Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na watendaji wa chombo chetu hiki tunaarifiwa kuhudhuria kisomo hicho cha 40.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo nichukuwe nafasi kuwashukuru tena kwa mashirikiano makubwa tuliyofanya kiasi cha kumaliza kazi hii vizuri. Na sasa basi nichukuwe nafasi kuahirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni leo.

(Saa 6.46 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, 2014/2015

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru kukutana tena jioni hii na jioni hii itakuwa ni zamu ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kuanzia naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha ili kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokanana ripoti Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mwaka 2013/2014 Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutuwezesha sote kwa pamoja kukutana tena hapa leo hii.

Pili, nimesimama kutoa maelezo ya utekelezaji wa wizara yangu kuhusu maoni ya maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza hili.

Mhe. Spika, Kamati hii kwa muda mrefu imekuwa ikiongozwa na mwenzetu ambaye kwa sasa ni Marehemu Salmin Awadh Salmin naomba kuchukua fursa hii kwa niaba yangu, uongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha kutoa pole kwako Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, familia ya marehemu na Chama cha Mapinduzi kwa kifo cha mwakilishi huyo wa Jimbo la Magombeni. Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi katika Baraza hili na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Marehemu Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Spika, msiba huu ni wetu sote na kwa upande wa Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla umetugusa sana kwani tumeondokewa na Mwenyekiti shupavu, mwadilifu na mchapakazi hodari aliyeoongoza vyema Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano makubwa na wizara ninayoisimamia ikiwa pamoja na Wizara ya Fedha ninayoiongoza mimi. Naungana na wenzangu wengine wote katika kumuomba Mwenyezi Mungu ailaze peponi roho ya Marehemu Salmin Awadh Salmin nasi pia atupe mwisho mwema. *Amiin*.

Mhe. Spika, Kanuni ya 108 ya Baraza lako hili tukufu inamtaka kila waziri kuwasilisha mbele ya Baraza hili taarifa juu ya utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya sekta yake. Kwa kuwa kwa sasa mimi ndiye Waziri mwenye dhamana ya sekta ya fedha, naomba nichukue fursa hii kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara kwa mwaka 2013/2014.

Hata hivyo, kabla ya kutekeleza jukumu langu hilo naomba kwanza kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuiwezesha kamati kufanya kazi zake kwa umahiri na uweledi mkubwa. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo, utendaji mzuri wa kamati hiyo umeisadia sana adhma ya Serikali ya kuimarisha utendaji wa wizara yangu na taasisi zote zilizo chini ya sekta ya fedha.

Maoni na Maagizo ya Kamati ya Utekelezaji wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, sasa naomba niwasilishe Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014 Ripoti ya Kamati iliwasilisha maoni na maagizo 49 yanayohusu Wizara ya Fedha na taasisi zake ikiwemo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), Shirika la Bima, Benki ya Watu wa Zanzibar, Bodi ya Mapato (*ZRB*), Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*). Kimsingi maoni na maagizo haya yalijikita katika maeneo makubwa manne ambayo ni haya yafuatayo.

Kwanza, haja ya kuimarisha utoaji wa taarifa kwa umma juu ya mambo mbali mbali yanayotekelezwa na wizara.

Mhe. Spika, karibu katika kila taasisi iliyotembelewa na Kamati kumejitokeza ushauri wa kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili waelewe mambo yanayotekelezwa na Serikali kupitia taasisi hizo. Kimsingi wizara yetu imekubaliana na ushauri huo kunapokuwepo na pengo la taarifa hali halisi Serikali na kile ambacho wananchi wanachokijua au wanachokiamini kunajitokeza changamoto na hapo ni wajibu wa serikali kutoa taarifa iliyo sahihi kwa faida ya wananchi. Pamoja na kwamba majibu ya hatua za utendaji zinazochukuliwa na kila taasisi katika kuimarisha ufikiaji wa habari kwa wananchi, wizara itaendelea kuweka mkazo maalum kwa suala la utoaji wa habari zilizo sahihi na kwa wakati.

Pili, ujenzi wa uwezo wa taasisi. Mhe. Spika, katika taasisi zilizotembelewa Kamati yako imekuwa na ushauri unaoelekeza kuchukuliwa hatua maalum za kuimarisha utendaji ama kwa kuajiri watendaji wenye taaluma zaidi au kwa kuwapatia mafunzo zaidi wafanyakazi waliopo au kwa kuzipatia vitendea kazi zaidi taasisi hizi ili ziweze kutimiza wajibu wake vyema zaidi. Wizara inakiri kuwa bado kuna upungufu wa uwezo katika sehemu mbali mbali za utendaji. Hata hivyo, kama Waheshimiwa Wajumbe wanavyofahamu kazi ya kujenga uwezo wa taasisi zetu ni endelevu na ina gharama kubwa. Wizara itaendeleza jitihada zake za kujenga uwezo wa kutekeleza mageuzi mbali mbali ili kuimarisha ufanisi katika utendaji wa wizara na taasisi zake.

Tatu, haja ya kuimarisha umakini katika usimamizi wa utendaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi kadhaa ya maendeleo nchini ama imekubwa na changamoto na hivyo kuzorota au taarifa zake kutoeleweka ipasavyo na wadau ikiwemo wananchi. Kwa upande wa Wizara ya Fedha uratibu wa utekelezaji wa miradi ya *E-Government* na huduma za jamii Mjini *ZUSP* imejitokeza kuwa katika kundi hilo. Wizara imepokea ushauri wa kamati na itakuwa ikishirikiana na sekta husika kutoa taarifa za utekelezaji wa kila hatua kwa miradi mikubwa ya maendeleo ili kuondoa pengo la taarifa kama ilivyoelezwa kabla na kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Nne, uwazi zaidi kwa shughuli zinazotekelezwa Kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, hata kama hakujajitokeza wazi wazi maoni ya Kamati kwa wizara na taasisi zake yanaashiria haja ya kuimarisha uwazi katika kueleza shughuli zinazotekelezwa na wizara na taasisi hizo kwa upande wa Pemba. Huu nao ni ushauri mzuri kwani utasaidia kuweka bayana zaidi huduma na uwekezaji unaoendelea katika kuleta maendeleo kwa wananchi. Bahati njema mfumo mpya wa uwekaji taarifa wa bajeti *Chart of Account* unaanza kutekelezwa katika mwaka 2015/2016 kwa kiasi kikubwa utasaidia kuondoa kasoro za sasa kwani utawezesha matumizi kujuulikana kwa kila eneo la wizara na kwa sehemu ambako fedha hizo zinatumika.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema mambo hayo manne ni hali ambayo imebainika kujitokeza zaidi katika ushauri wa Kamati, taarifa ya utekelezaji kwa kila maoni na maagizo ni kama inavyoonekana katika *martrix* niliyoambatisha. Kwa heshima kubwa sasa naomba kuyatolea maelezo.

Agizo la kwanza

Linaeleza kwamba kwa kuwa mahitaji ya taaluma yapo katika ngazi tofauti ni vizuri wizara ikatoa pia kipaumbele chakuwapeleka masomoni wafanyakazi wake wanaohitaji kusoma katika ngazi ya Stashahada badala ya kutegemea kusomesha wafanyakazi katika ngazi ya Shahada za juu pekee.

Utekelezaji

Wizara imeendelea kuwapatia fursa wafanyakazi wake kujiendeleza kitaaluma katika ngazi ya Stashahada ambapo kwa mwaka wa masomo 2013/2014 wizara imesomesha jumla ya wafanyakazi 13. Aidha, kwa mwaka wa masomo 2014/2015 wizara inaendelea kuwasomesha wafanyakazi 10 katika ngazi ya Stashahada na wafanyakazi 2 katika ngazi ya cheti. Wafanyakazi hawa wanasomea fani tofauti zikiwemo *TEKNOHAMA*, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Uhasibu, Ununuzi na Ugavi na Usafirishaji.

Agizo la pili

Wizara kupitia Idara ya Uhakiki Mali iwe na ushirikiano wa karibu kati yake na taasisi nyengine za Serikali ili kupatikana usahihi wa taarifa za kumbukumbu za mali za Serikali zilizo sawa kwa pande zote mbili ili kuondoa migongano na taarifa hizo baina ya Idara ya Uhakiki Mali na taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Spika, utekelezaji ni kwamba idara imechukua hatua maalum za kuhakiki mali zote za Wizara za Serikali, lengo ikiwa ni kuainisha *record* baina ya idara na wizara husika. Taarifa hizi kwa sasa zimewekwa katika daftari maalum ambalo limetayarisha na idara na kusambazwa kwa wizara na taasisi zote.

Aidha, zoezi hilo lilitegemewa pia kubaini mali zote chakavu hasa vyombo vya moto vinavyohitajika kuondolewa. Orodha ya mali hizo iliwasilisha serikalini na baada ya kuidhinishwa viliuzwa kwa mnada. Hatua za kuliendeleza daftari la kudumu la mali za Serikali katika mfumo wa ki-*electoronic* zinaendelea baada ya kukamilishwa kwa wizara tano.

Agizo la tatu

Wizara itoe msukumo maalum katika Idara ya Uhakiki Mali hususan kwa upande wa Pemba kwa kukipatia nyenzo za kisasa za kufanyia kazi zitakazolingana na uzito wa majukumu iliyonayo idara hiyo.

Utekelezaji

Ni kweli idara hii bado ina upungufu mkubwa wa nyenzo za kufanyia kazi hasa vyombo vya usafiri. Utafutaji wa vyombo vya usafiri kwa Taasisi za Serikali unafanyiwa kazi kwa ujumla wake.

Agizo la nne

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uongeze njia za kutoa taaluma juu ya huduma mbali mbali zinazotolewa na mfuko huo zikiwemo huduma mpya za uchangiaji wa hiari kwa watu binafsi (*Voluntary Scheme*) ili wananchi wengi zaidi wawe na mwamko wa kuzitumia fursa zinazotolewa na mfuko huo.

Mhe. Spika, utekelezaji ni kwamba *ZSSF* imeendelea kuutangaza zaidi Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na huduma zake kwa kutumia vyombo mbali mbali vya habari, vikiwemo redio na televisheni za Serikali na watu binafsi, vijarida na machapisho ambayo hutolewa kwa wananchi na wanachama. Mfuko pia umeshiriki katika maoneshe mbali mbali yakiwemo ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na siku ya wafanyakazi Mei Mosi. Pia, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 mfuko umefanya mazungumzo na Kampuni ya Simu ya *ZANTEL* ili kuingiza huduma za uchangiaji wa hiari katika huduma za *Eazy* Pesa kwa sasa tayari mfuko umeshafunga mkataba na *ZANTEL* na inatarajiwa kwamba huduma hizo zitaanza kutolewa hivi karibuni.

Agizo la tano

Ni vyema kwa uongozi wa mfuko kufikiria suala la kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika kazi za kila siku za mfuko huo kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji

Jumla ya wafanyakazi wanne tayari wamo katika hatua za mwisho za kuajiriwa ili kutoa huduma katika tawi la Pemba. Kama ilivyo kwa mifuko mengine *ZSSF* inaendelea kuzingatia na kudhibiti gharama za utawala kabla ya kuajiri, hivyo, uajiri utafanywa pale ambapo ni lazima na kwa kuzingatia mahitaji na uwezo wa muda mfupi na mrefu.

Agizo la sita

Shirika la Bima liangalie uwezekano wa kuongeza wafanyakazi katika ofisi yake ya Pemba ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa shirika hilo katika ofisi hiyo.

Utekelezaji

Pamoja na kupokea ushauri wa Kamati, shirika tayari lina wafanyakazi wa kutosha Pemba wanne kwa kuzingatia ukubwa wa soko na gharama za uendeshaji. Jitihada za kuimarisha sehemu ya uhasibu kwa kupata muhasibu kutoka Wizara ya Fedha zimechukuliwa.

Agizo la saba

Ni vizuri kwa Serikali kulifikiria kwa moyo wa huruma suala la kulipa eneo jengine Shirika la Bima kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya shirika hilo Kisiwani Pemba. Shirika lianedelea kufuatilia upatikanaji wa jengo kutoka Wizara ya Ardhi, Makazi, Maji na Nishati ambalo litatumika kwa watumiaji wa shirika kwa upande wa Pemba.

Agizo la nane

Kamati inalitaka Shirika la Bima kuendeleza mpango wake wa kuajiri wafanyakazi wa mkataba kutoka katika Mikoa au maeneo ambayo Ofisi za Shirika la Bima zipo ili kupunguza gharama za kuwahudumia wafanyakazi wa shirika kutoka Zanzibar wanaofanya kazi katika Mikoa na maeneo hayo.

Utekelezaji

Ni kwamba agizo la kuendeleza mpango wa kuajiri wafanyakazi kwa mkataba kutoka Mikoa zilizopo ofisi za shirika limepokelewa na linaendelezwa, kila itakapotokea ajira Mikoani shirika litafanya hivyo.

Agizo la tisa

Katika azma yake ya kutaka kuwa na jengo lake shirika linashauriwa kutafuta haraka katika kutekeleza azma hiyo kwa kuwa gharama za kiwanja na ujenzi wake ni kubwa zaidi katika Mji wa Arusha. Hivyo, shirika linaombwa kujipanga vizuri lisije kuterereka kutokana na matumizi makubwa ya kazi hiyo.

Utekelezaji

Ni kwamba ushauri umepokelewa uamuzi wa mwisho wa shirika juu ya kununua au kuanza ujenzi wa Ofisi ya Arusha bado haujatolewa na utaendelea kuzingatia ushauri wa kamati.

Agizo la 10

Shirika linapaswa kuzidisha mashirikiano yake na mawakala ikiwa ni pamoja na viongozi wa shirika katika kanda kuwatembelea mara kwa mara mawakala na kuwasikiliza maoni yao. Viongozi wa shirika wanatembelea mawakala kila mwaka katika sehemu zote ambapo mawakala wao wapo, tayari mawaka wa Mbeya, Dodoma na Kanda ya Pwani wameshatembelewa kwa mwaka huu wa fedha.

Agizo la 11
Kwa kuwa wananchi wengi wa kawaida hawana taaluma ya bima, Kamati inashauri kwa shirika kuendelea kutoa elimu na mafunzo kwa wana jamii kuhusiana na umuhimu wa bima.

Ushauri umepokelewa na kwa kutumia njia za ziada za kujitangaza tayari *programmes* maalum za matangazo, redio, televisheni na vipindi vya maswali na majibu vinavyohusiana na mambo ya bima vimeandaliwa na vitaanza kurushwa hivi karibuni, mbali ya vile vya kawaida.

Agizo la 12

Shirika la Bima libuni na kutumia njia za ziada za kujitangaza ikiwemo kutumia fursa za maeneo ya mkusanyiko au mikutano ya viongozi wa kisiasa na mengineyo.

Ushauri umepokelewa wa kutoa elimu ya bima. Uongozi ulichukua juhudi za kufanya semina Unguja, Pemba na Dar es Salaam na kukutana na wadau kuwaelimisha mambo mbali mbali yanayohusiana na bima.

Agizo la 13

Shirika libuni mbinu na mikakati imara itakayowezesha kukabiliana na ushindani unaotokana na ongezeko la kampuni nyingi za bima. Shirika linaelewa hali ya ushindani uliopo na haja ya kuimarisha zaidi huduma zake kimkakati shirika limejielekeza katika maeneo yafuatayo:

1. Jitihada kubwa zaidi kutafuta masoko;

2. Kuongeza wigo wa huduma za shirika;

3. Kulipa madai yaliyo sahihi kwa muda mfupi ikiwezekana na

4. Kuimarisha maslahi ya wafanyakazi wataalamu ili kuwabakisha katika shirika.

Agizo la 14

Watendaji wa Shirika la Bima wazidishe umakini katika kufanya tathmini na ukaguzi wa madai ya wateja ili kuweza kugundua madai mengi zaidi ya udanganyifu na hivyo kuokoa zaidi upotevu wa fedha.

Utekelezaji

Ni kwamba shirika litaendeleza umakini katika kufanya tathmini na ukaguzi wa madai ya wateja. Madai yote ambayo yanayoonekana sio sahihi yanafanyiwa uchunguzi wa kina kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kitengo cha Upelelezi kama taratibu za kisheria zinavyotaka.

Agizo la 15

Kamati inaishauri Serikali kuongeza mtaji Benki ya Watu wa Zanzibar ili iweze kupanua masoko yake ya kifedha na kuweza kwenda sambamba na kiasi cha maendeleo ya teckonolojia za kibenki duniani hivi sasa.

Utekelezaji

Ni kwamba wizara imetumia mbinu mbali mbali kuiongezea mtaji Benki ya Watu wa Zanzibar ikiwemo kulipa madeni yake, kushajihisha taasisi na wafanyakazi wa Serikali kuitumia *PBZ*, kusamehe kodi ya mapato na gawio kutokana na faida iliyoipata benki ili iweze kuekeza. Hata hivyo, tokea awali ilikubalika kuwa utaratibu huu utakuwa wa muda ili Serikali nayo iweze kupata fedha kwa kutoa huduma nyengine kwa wananchi.

Mahitaji ya sasa ya mtaji wa benki yanaendelea kuzungumzwa baina ya Wizara ya Fedha na Benki ili kuona mahitaji halisi na namna ya kuyashughulikia.

Agizo la 16

Mikakati maalum inahitajika katika kuimarisha utendaji wa wafanyakazi wa *PBZ,* hususan wanaotoa huduma za moja kwa moja kwa watendaji ili kupunguza malalamiko ya wateja kutokana na usumbufu wanaoupata.

Utekelezaji

Ni kwamba benki inatoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wake wa ndani (*In house training*) na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wake kwa lengo la kutoa huduma nzuri kwa wateja wake. Hata hivyo, ili kupunguza haja ya kuonana na wafanyakazi wakati wa kutoa huduma na kwa dhamira ya kufikisha huduma karibu zaidi na wateja, benki imeendelea kuimarisha huduma za *ATM*, huduma za kupitia mitandao ya simu na *internet*. Kwa sasa *PBZ* inafanyia kazi uanzishwaji wa huduma za benki kupitia mawakala (*Agency Banking*) ambazo zitapelekea kupunguza idadi ya wateja katika matawi ya *PBZ*. Hatua hiyo itawapa fursa wafanyakazi wa benki kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Agizo la 17

Ni vyema kwa taasisi za SMZ zenye ofisi zao Dar es Salaam kufungua *accounts* zao katika Benki ya Watu wa Zanzibar ili kusaidia kuendeleza shughuli za benki hiyo huko Tanzania Bara. Ushauri umepokelewa na wizara inaendeleza juhudi zake kuhamasisha taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufungua *accounts* katika Benki ya Watu wa Zanzibar. Kwa sasa taasisi nyingi za SMZ zina *accounts* zao *PBZ*.

Agizo la 18

PBZ inapaswa kusaidia kutoa elimu na mafunzo kwa jamii kuhusiana na mfumo wa Benki ya Kiislamu. *PBZ* inatoa elimu juu ya Benki ya Kiislamu kwa jamii kupitia semina tunazoandaliwa na benki, kushiriki makongamano mbali mbali Zanzibar na Tanzania Bara pamoja nakusambaza vipeperushi, itaendelea kutumia njia hizo kuelimisha zaidi suala la Benki ya Kiislamu kama ilivyoshauriwa na Kamati.

Agizo la 19

Kamati inapendekeza kuwa *PBZ* iongeze mikakati mingine ili benki hiyo iweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni. Kama ilivyoelezwa hapo kabla tayari benki inatoa huduma mbali mbali kwa kutumia simu na intaneti. Aidha, benki imo katika hatua za kubadilisha mfumo wake mkuu wa teknolojia wa kutoa huduma za benki kwa benki ya kawaida na Benki ya Kiislamu, mfumo ambao utawezesha kuboresha huduma za benki.

Agizo la 20

Kamati imeona ipo haja kwa *PBZ* kutekeleza kwa vitendo wazo la kutafuta eneo la kujenga jengo lake kwa ajili ya kupunguza ngarama za kukodi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ushauri wa Kamati ni mzuri. Hata hivyo, kwa kuwa ujenzi unahitaji rasilimali nyingi, *PBZ* inahitaji kujipanua kwa kuzingatia uwezo wake wa mtaji na hali ya soko la ushindani. Kwa sasa benki ipo katika hatua za kujenga makao makuu yake Mazizini, ujenzi katika maeneo mengine utakuja kwa awamu.

Agizo la 21

PBZ izidishe mashirikiano na Shirika la Bima la Zanzibar kwa kulisaidia shirika hilo liweze kufungua Bima ya Kiislamu. Benki inashirikiana kwa karibu na Shirika la Bima la Zanzibar kwa nia ya kuanzisha huduma za bima ya Kiislamu yaani (*Takaful*). Hata hivyo, suala hili kwa upande wa bima linategemea kuruhusiwa rasmi na msimamizi wa huduma za bima, *TIRA*. Taarifa ni kwamba tayari *TIRA* imeshaandaa Kanuni za kusimamia huduma za Bima ya Kiislamu na zipo katika hatua za mwisho za kuidhinishwa.

Agizo la 22

Kamati imeshauri kuwa Bodi ya Mapato Zanzibar kuanzisha kuweka mikakati maalum ili kuhamasisha wafanyabiashara wanaotoa risiti wakati wanapofanya mauzo katika biashara zao. Aidha, Kamati inaona ni vyema *ZRB* ikajifunza kikamilifu njia zinazotumika nchini Kenya katika kuwafanya wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa kutoa risiti mara baada ya mauzo. Kwa sasa *ZRB* imekuwa ikifanya mazoezi maalum ya kufuatilia utoaji wa risiti kwa wafanyabiashara na kuwaadhibu wale wanaopatikana na makosa, suala la kujifunza katika nchi za jirani zilizofanya vizuri katika utoaji wa risiti ikiwemo Kenya na Ethiopia ni muhimu na litafanyiwa kazi. Kwa sasa Serikali imo katika hatua za kuanzishwa utaratibu wa kutoa risiti za kiteknolojia (*EFD's*) ambao utasaidia suala zima la utoaji wa risiti.

Agizo la 23

Serikali iangalie uwezekano kuanzisha mfumo wa ulipaji risiti kwa elektroniki (*EFD's*). Serikali imelipokea suala hili na sasa limo katika hatua za kukamilisha mazingira ya kuanzisha matumizi ya vifaa hivyo ikiwemo utayarishaji wa Kanuni kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko chini ya Sheria ya Biashara ya Zanzibar ya mwaka 2013.

Agizo la 24

Kamati inapendekeza kuwa *ZRB* izidishe mashirikiano na taasisi na vyombo vya ulinzi pamoja na wananchi ili kuweza kukabiliana na biashara ya magendo ya mafuta. *ZRB* imekuwa ikishirikiana na Kikosi cha KMKM, Jeshi la Polisi, Masheha pamoja na raia wema katika kupambana na kupiga vita biashara ya magendo ya mafuta kama ilivyoshauriwa. Jitihada hizi zitaendelezwa zaidi.

Agizo la 25

Kamati inasisitiza kuwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar kuendelea kuimarisha elimu kwa walipa kodi na wananchi kwa ujumla ili kujua kikamilifu taratibu za ulipaji kodi na hatimaye kuweza kulipa kodi kwa hiari. *ZRB* inatoa na itaendelea kutoa elimu kwa walipa kodi na wananchi kwa ujumla kupitia njia mbali mbali ikiwemo semina, mikutano, matangazo, televisheni na vyombo vyengine vya kupasha habari.

Agizo la 26

Kamati inashauri kuwa ni vyema kwa Serikali kuchunguza kwa makini mfumo wa watalii kulipia wanakotoka na kuangalia taratibu zinazohusika na uwezekano wa kuondoa kwa kuwa unaonekana kuwa hauna tija ya kutosha hapa nchini. Ushauri umepokelewa hata hivyo, kutokana na uzoefu wa nchi nyengine za utalii kama vile Mauritius ni vigumu kuondoa utalii wa aina hii, kinachohitajika zaidi ni kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato hasa kwa kutumia utaratibu wa "*transfer pricing",* kwa muda mrefu Tanzania haikuwa na Kanuni zinazoongoza uzuiaji wa "*transfer pricing"*. Kwa sasa tayari Kanuni hizo zimetiwa saini na Waziri wa Fedha wa *SMT* na wizara kupitia *ZRB* itaangalia jinsi zinavyoweza kutumia kwa mapato ya *VAT* na hoteli hapa Zanzibar.

Agizo la 27

Kuna haja kwa Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla kufanya utafiti wa kina ili kujua namna na kwa kiasi gani misamaha ya kodi inavyolinufaisha Taifa.

Utekelezaji

Ni kwamba kwa kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar wizara imeshafanya utafiti juu ya misamaha ya kodi, ripoti ya utafiti imeshawasilishwa kwa sasa inafanyiwa uchambuzi.

Agizo la 28

Kamati inashauri *TRA* kuongeza idadi ya wafanyakazi hususan katika ofisi yake ya Pemba, ambapo Kamati ilibaini kuwa kuna wafanyakazi wachache ikilinganishwa na wingi na uzito wa majukumu yanayotekelezwa na wafanyakazi hao katika kufuatilia masuala ya kodi katika maeneo mbali mbali.

Utekelezaji

Ni kwamba ni kweli kuwa kuna upungufu wa wafanyakai katika baadhi ya maeneo ya *TRA*. Wakati mamlaka yenyewe ikiendelea na utaratibu wa kuajiri, wizara na *TRA* zilikubaliana kupeleka wafanyakazi kwa njia ya kuazimwa ili kuimarisha utendaji. Jumla ya wafanyakazi 20 wamehusika na utaratibu huo kati yao wafanyakazi wanne wamepangiwa kufanya kazi katika ofisi za *TRA* zilizoko Pemba. Upangaji wa wafanyakazi unazingatia pia uzito wa kazi na mchango wa mapato.

Agizo la 29

TRA ilishauriwa kufanya utaratibu wakupatikana mwanasheria katika ofisi yake ya Zazibar badala ya ofisi hiyo kutegemea mwanasheria kutoka Makao Makuu Dar es Salaam. Mwanasheria kwa ajili ya ofisi ya Zanzibar tayari ameshaajiriwa na ameanza kazi tokea mwezi wa Septemba mwaka 2011.

Agizo la 30

Kamati pia ilipendekeza kuwa *TRA* kuongeza kasi ya kupatia fursa ya masomo kwa wafanyakazi wake ili waweze kumudu masuala ya kodi na kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya teknolojia iliyotumika katika sekta mbali mbali zikiwemo za mawasiliano na utalii ambazo *TRA* inakusanya kodi.

Utekelezaji

Ni kwamba jumla ya wafanyakazi 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 54 mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali zikiwemo fani ya uchumi, uhasibu, uongozi na kodi katika mwaka 2013/2014.

Agizo la 31

Kamati inashauri *TRA* kufuatilia kwa makini malalamiko ya usumbufu wanaoupata wananchi wa Zanzibar wanaosafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara, ili kubaini kama kuna upungufu au vikwanzo vyovyote visivyo vya lazima viweze kuchukuliwa hatua.

Utekelezaji

Ni kwamba tatizo kubwa ni kutumia mifumo tafauti ya kutathmini bidhaa ambapo Tanzania Bara wanatumia mfumo wa *Import Export Commodity Data Base (IECDB)* na Zanzibar wanatumia mfumo wa zamani. Hali hiyo ndiyo inayopelekea kufanyika tathmini mkpya kwa bidhaa zote zinazopelekwa Tanzania Bara kutoka Zanzibar na hatimaye kutakiwa kulipa tafauti ya kodi inayojitokeza kama ipo.

Agizo la 32

Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zinazohusika kufanya juhudi za makusudi za kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika sekta ya viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuweza kukuza uchumi wa nchi.

Utekelezaji

Mamlaka inaandaa vipeperushi kwa lugha ya Kiswahili kushiriki katika maonesho mbali mbali ili kutoa mafunzo kwa wawekezaji wa ndani katika kuwashajihisha waweze kuwekeza katika sekta mbali mbali zikiwemo za viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, lengo ni kukuza uchumi kwa wananchi.

Agizo la 33

Serikali inapaswa kuweka mkazo maalum kwa sekta binafsi kuhamasishwa kufungua biashara kubwa kubwa Pemba na Serikali kuwekeza kwenye miundombinu, mitaji, masoko na kupatikana kwa mikopo. Tayari kuna miradi imewekeza kwa upande wa Pemba na kuna miradi mipya pia inatarajiwa kuzinduliwa na kuwekeza hivi karibuni. Serikali imechukua juhudi kubwa kuimarisha miundombinu kama vile barabara na sasa inaelekeza nguvu zake katika kiwanja cha ndege cha Pemba. Suala la fedha za mtaji bado limeendelea kuwa ni changamoto kwa Zanzibar.

Agizo la 34

Kuna haja kubwa ya kuimarisha kwa ulinzi wa doria baharini na vyombo vya ukusanyaji mapato kupatiwa mashirikiano ya karibu kutoka taasisi za ulinzi na Vyombo vya Serikali ili kudhibiti biashara ya magendo. Kwa sasa Bodi ya Mapato inafanya kazi kwa karibu sana na vikosi mbali mbali vya ulinzi na usalama vikiwemo vikosi vya kuzuia magendo, madiwani na masheha na kadhalika.

Utekelezaji

Aidha, utaratibu wa kuweza kuzitumia boti za Mamlaka ya Mapato Tanzania zilizopo Zanzibar ili kuhakikisha udhibiti wa suala zima la magendo unaangaliwa, kwani una gharama kubwa.

Agizo la 35

Kuna haja kwa Benki Kuu ya Tanzania kuishauri mara kwa mara Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mbali mbali ya kiuchumi ilikusaidia kuimarisha uchumi wake. Wizara ya Fedha imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana na Benki Kuu ya Tanzania kadiri inapojitokeza haja kama vile wakati wa kasi kubwa ya mfumko wa bei, mgogoro wa kifedha wa dunia, uanzishwaji wa hifadhi ya chakula, utafiti juu ya matumizi ya fedha zitokanazo na mauzo ya karafuu na utafiti wa mitaji binafsi nchini.

Utekelezaji

Wizara pia inashiriki katika Kamati ya Sera za Fedha ambayo inajadili masuala mbali mbali ikiwemo masuala yanayohusu uchumi wa Zanzibar pamoja na kutoa ushauri.

Agizo la 36

Mikakati madhubuti inahitajika kuwekwa ili kudhibiti kikamilifu wizi wa fedha kwa kutumai mitandao pamoja na udhibiti wa noti bandia.

Utekelezaji

Benki Kuu imeandaa mkakati maalum wa kukagua mifumo (*systems*) ya benki zilizopo Tanzania ili kuhakikisha wizi wa kutumia mitandao unadhibitiwa. Aidha, Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu inaendelea kutumika.

Agizo la 37

Elimu kwa umma juu ya umuhimu wa utunzaji mzuri wa fedha ni jambo la msingi kutolewa hasa ikizingatiwa kuwa Serikali hugharamika katika kuchapisha noti mpya.

Utekelezaji

Benki Kuu imeendelea kutoa elimu hiyo kwa njia tafauti jitihada zaidi zitaendelea kuchukuliwa.

Agizo la 38

Kamati iliagiza wizara kufanya kila inaloliweza kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya utayarishwaji wa *master plan* ya maeneo huru Fumba zinapatikana na hivyo kazi hiyo kukamilika kama ilivyokusudiwa.

Utekelezaji

Serikali imetekeleza kwa vitendo agizo hilo la Kamati na fedha zimeingizwa na utekelezwaji wa *master plan* umetekelezwa kwa mwaka 2012/2013. Serikali imeingiza shilingi milioni mia moja na hamsini na kwa mwaka huu 2014/2015 serikali imeingiza shilingi milioni mia moja na ishirini.

Agizo la 39

Kuna haja kwa mamlaka ya utunzaji vitega uchumi *ZIPA* kuzidisha utoaji wa elimu kwa wananchi, viongozi na wawekezaji mbali mbali juu ya taratibu za Serikali katika ardhi ya wawekezaji.

Utekelezaji

Ni kwamba kabla ya uwekezaji kutekelezwa mamlaka huwa inashirikisha kikamilifu wananchi kupitia masheha wao juu ya umuhimu wa uwekezaji na pia kuwapatia taratibu za Serikali katika ardhi ya wawekezaji. Hata hivyo, mamlaka itazidisha utoaji wa elimu kwa wananchi.

Agizo la 40

Serikali iangalie vizuri suala la kuboresha taasisi zake katika upande wa mtandao wa ndani (*Lan Network*) pamoja na vyumba vya kufungia vifaa vya mkongo wa Taifa *(E-Government).*

Utekelezaji

Ni kwamba Wizara ya Fedha imeshawapatia fedha wizara na taasisi zote za Serikali kwa ajili ya kuweka mazingira ya kuunganisha huduma za mkonga wa Taifa, yaani *local Area Network* katika taasisi zote za Serikali.

Agizo la 41

Elimu ya kutosha inahitajika kutolewa kwa wafanyakazi na wananchi mbali mbali kuhusu masuala ya *E-Government* pamoja na uhifadhi wa mkongo ili kujua matumizi halisi ya mtandao wenyewe thamani yake na athari zake pindi utakapoharibika.

Utekelezaji

Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zimekuwa zikitoa elimu hususan masuala ya *E-Government* na mkongo wa mawasiliano na haja ya kuulinda, elimu zaidi itaendelea kutolewa kwa wananchi.

Agizo la 42

Maandalizi ya kutosha yanahitajika kufanywa kwa taasisi za Serikali ambazo zinahitajiwa kuunganishwa na mkongo ili kupata vyumba vya mitambo, yaani *Server room* vilivyokidhi vigezo.

Utekelezaji

Ni kwamba kwa namna ya muundo wa matumizi ya *E-Government* wizara na taasisi za Serikali hazihitaji kuwa na *server room* ili kuunganishwa na mkongo huo. *Server room* ni moja tu na ipo katika kituo cha mawasiliano (*Data centre*). Kinachohitajika kwa wizara ni vifaa maalum vya kuunganisha mfumo wa ndani wa wizara na ule wa mkongo wa Taifa ambapo kwa sasa tayari majengo 83 yameshaunganishwa kama ilivyoagizwa awali.

Agizo la 43

Ni vyema kwa viongozi na watendaji wa Serikali kuwa waangalifu sana inapotaka kuanzisha miradi mikubwa kwa vile inaonekana kuwa utekelezaji wa miradi mikubwa hapa nchini huwa una mashaka na hivyo kuwafanya wananchi ambao ndio serikali inaowatumia kukosa imani na Serikali yao.

Utekelezaji

Ni kwamba ushauri umepokelewa na maelekezo yake ni kama nilivyotangulia kusema katika maelezo yangu ya jumla. Hata hivyo, ni lazima tukubali miradi mikubwa ina changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na utaalamu wa hali ya juu. Vile vile. kuna haja ya wananchi kuelimishwa juu ya maendeleo yake.

Agizo la 44

Serikali ianze kufikiria nama itakavyochukua hatua muwafaka kuhusu hatma ya kuunganisha mtandao wa *E-Government* katika majengo ambayo Aerikali imeyakodi kwa ajili ya shughuli zake. Mhe. Spika, kwa sasa mtandao huo utawekwa katika majengo hayo ili wizara ziendelee kupata huduma hiyo, pale wizara au taasisi zitakapokuwa na majengo yake yenyewe pia hatua itachukuliwa ili kufikisha huduma hiyo kupitia mkongo huo.

Agizo la 45

Kuna haja kubwa ya kuzidisha jitihada za utoaji wa elimu kwa wananchi na viongozi juu ya mradi wa huduma ya jamii mijini (*ZUSP*) pamoja na kutoa taarifa za maendeleo ya mradi kwa wananchi, kwani mradi huu unawagusa wananchi moja kwa moja

Utekelezaji

Ni kwamba wizara kupitia timu ya uratibu wa mradi wa *ZUSP*, imefanya vikao kwa kuwahusisha wadau mbali mbali wakiwemo masheha, madiwani, wakuu wa vyombo vya usalama na wanafaika wa baadhi ya maeneo, miradi kwa lengo la kutoa uelewa juu ya mradi huu. Aidha, *ZUSP* imeandaa programu maalum kupitia vyombo vya habari vya ndani kwa ajili ya kujenga ufahamu kwa wananchi juu ya mradi wa huduma za jamii mijini.

Agizo la 46

Wizara ya Fedha imepaswa kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa miradi inayoisimamia na kujua vizuri iwapo fedha za miradi hiyo zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Utekelezaji
Mhe. Spika, ni kwamba, kupitia kitengo cha ufuatiliaji na tathmini, wizara inaendelea na ufuatiliai wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa kwa kufanya ziara maalum kila mwezi kuangalia utekelezaji wa miradi hiyo na pia kuhakikisha fedha za miradi hiyo zinatumika kama zilivyokusudiwa. Pili, kutayarisha ripoti ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Agizo la 47

Kamati inaitaka wizara kuhakikisha kuwa Ofisi ya Mdhamini Wizara ya Fedha Pemba inashirikishwa kikamilifu katika kazi za miradi ya maendeleo zinazofanyika Pemba ili kurahisisha usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi hiyo pamoja na upatikanaji wa taarifa za miradi hiyo inayotekelezwa Pemba.

Utekelezaji

Mhe. Spika, ushauri umepokelewa na wizara inamshirikisha Afisa Mdhamini katika miradi hiyo kwa upande wa Pemba, kwa kuanzia ofisa huyo amekuwa akishiriki katika usimamizi wa miradi inayotekelezwa na wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo *ZUSP*. Utaratibu wa kumshirikisha kwa miradi yote ya Serikali utaandaliwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Agizo la 48

Ni vyema kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuandaa utaratibu utaoweka wazi bajeti ya maendeleo kwa Pemba ambao utaweza kusaidia kurahisisha ufuatiliaji wa karibu wa matumizi ya fedha.

Utekelezaji

Ni kwamba, mfumo mpya wa takwimu za kihasibu (*Chart of Account)* unatarajiwa kuanza kutumika mwaka 2015/2016, sambamba na bajeti inayotegemewa (*Programme Based Budget (PBB)*)

utawezesha kujulikana matumizi kwa kila eneo la sekta kijiografia ikiwemo mikoa ya Pemba na hivyo kutatua kwa kiasi kikubwa kasoro iliyobainishwa sasa. Matayarisho ya mfumo tayari yameshakamilika kwa kuzingatiwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha. Waheshimiwa Wajumbe, jioni ya leo kuna wageni ambao wanatoka kwenye Taasisi ya *Global Peace Foundation*. Taasisi hii Waheshimiwa Wajumbe kwa kifupi inashughulika na masuala ya kuleta amani na utulivu nchini na kuleta maendeleo endelevu duniani.

Taasisi hii ina viongozi wake ambao kwa mujibu wa kabrasha nililoletewa viongozi wa taasisi ya *Global Peace Foundation* ni pamoja na marais wastaafu watano akiwemo Rais Mstaafu Obasanjo kutoka Nigeria, Rais Mstaafu Kenneth Kaunda kutoka Zambia, vile vile *His Excellency* Star Jemas Mattam, huyu ndiye *Found of President* kutoka Seychelles, Rais mstaafu. Hao ninaowataja hawapo hapa hii ni hiyo *foundation* yenyewe inayoongozwa na marais hawa wastaafu. Mwengine ni Rais *His Excellency* Germar Ude Georges huyu ni rais wa *Federal Democratic Republic of Ethiopia*, pamoja na Rais mstaafu *His Excellency* Mhe. Aman Abeid Karume. Marais watano hawa wastaafu ndio wanaunda hiyo *Global Peace Foundation.* Sasa wageni wetu wa leo ni Maafisa ambao wanatayarisha mkutano na wako hapa Zanzibar na kwa jioni ya leo wamefika hapa katkka Ofisi zetu za Baraza la Wawakilishi.

Ujumbe huo unaongozwa na ndugu yetu *Can I now know recognize the delegation we have today this evening is the Speaker's gallery* the Mr. James P. Flynn *International President Global Peace Foundation* yule pale. *Other Members* is Mr. Michael Sommer *International of Repetitive Global Peace Foundation* yule pale, mwengine ni Mr Daniel Juma Omondi *Director Global Peace Foundation Kenya* Mr. Omondi yule pale. Mwengine ni Mr Insu Choi *Regional Representative African Region Global Peace Foundation* yule pale na mwenyengine watano ni Mr. Arnold Kashembe *Country Director, Global peace Foundation - Ireland* yule pale.

Wageni hawa leo wamependa kuja kutembea hapa Barazani ili kuona shughuli zetu zinandelea namna gani, lakini kimsingi wako Zanzibar kwa ajili ya matayarisho ya huu mkutanao ambao *Global Peace Foundation* ambao viongozi wake ni wale watano niliowataja kabla *you are most welcome to our session in the House of Representative, you are most welcome, thank you*.

Ahsanteni sana Wahehimiwa Wajumbe, sasa tunaendelea. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, lkulu na Utawala Bora: (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, nakushukuru sana kupata nafasi hii kuja kutoa utekelezaji wa hoja na maagizo mbali mbali yaliyoagizwa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo katika upande wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2013/14.

Kabla sijaendelea naomba kumshukuru sana Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Hija Hassan Hija wa Jimbo la Kiwani. Lakini vile vile Mhe. Spika, sote tumefiwa na mwenzetu kama tunavyotambua Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Marehemu Salmin Awadh Salmin, yeye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, sote tunajua alikuwa ni mpiganaji shujaa na mfatiliaji makini wa shughuli za Kamati.

Kwa kweli Mhe. Spika, naungana na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza mbali ya kuwapa pole familia lakini pia kuipa pole Kamati. Wenzetu ndio walikuwa nae muda mwingi na wakifanyakazi pamoja. Kwa kweli wataona lile pengo ambalo tumelipata, naomba wawe na subira, hii ndio imeandikwa na Mwenyezi Mungu sote safari hiyo tutakwenda, tuwe wastahamilivu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba nisema kwamba kamati imeagiza wizara hii jumla ya maagizo 34 ambayo yamesambazwa katika kabrasha hilo mlilonalo. Sasa naomba bila ya kupoteza muda niwachukuwe haraka haraka ule utekelezaji wake.

Kwanza kabisa Mhe. Spika, iliangizwa na Kamati kwamba wizara iwapatiwa wafanyakazi maslahi yao wanayostahiki japo kwa awamu ili kujenga ari na morali ya kazi. Kuhusu utekelezaji wizara imefanya jitihada kuwa ya kuwapatiwa wafanyakazi maslahi yao. Lakini kutokana na uhaba wa fedha walizopatiwa wizara, inalazimika wafanyakazi wapatiwe maslahi yao kwa awamu. Hata hivyo, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 maslahi ya wafanyakazi yalikuwa kama yafuatayo.

Wafanyakazi wote elfu mbili mia moja hamsini na mbili wa wizara wamepatiwa mishahara yao kwa wakati ili jumla ya wafanyakazi mia moja na moja wamepatiwa pesa zao za likozo na tatu wafanyakazi mia mbili na hamisini wamepatiwa malipo ya baada ya saa za kazi. Wizara kwa ujumla inafanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapatiwa maslahi yao kulingana na fedha kadri zinavyopatikana.

Agizo la pili

Mhe. Spika, ni kwamba kwa kushirikiana na wizara husika ya ajira iliajiri wafanyakazi watakaojaza nafasi za wafanyakazi waliostafu na waliofariki kabla ya kushughulikia ajira mpya.

Utekelezaji

Mhe. Spika, wizara zetu mbili zilikaa pamoja na kulijadiliana jinsi ya kujaza nafasi tupu na kukubaliana na wizara itakuwa na ruksa ya kujaza nafasi husika mara tu itakapotokea nafasi hizo tupo. Wizara iliziomba nafasi tupu 72 Unguja na 52 Pemba, hata hivyo ruksa ya kuzijaza nafasi hizo bado haijatolewa. Kwa kuwa suala hili la ajira linasimamiwa na wizara nyengine imepelekea kuchelewa kuzijaza nafasi hizo kwa wakati. Hata hivyo, mazungumzo yanaendelea.

Agizo la tatu

Mhe. Spika, Mhe. Spika, ni kutoa kupaumbele maalum na kwa vitendo kwa matayarisho ya kilimo cha mpunga ikiwemo upatikanaji wa fedha tena kwa wakati pamoja na vitende kazi. Vile vile, kuwafanya wafanyakazi wazoefu wenye moyo wa kujituma ili kuwaondoshea usumbufu wakulima juu ya athari ya kuchelewa kulimiwa kwa wakati.

Utekelezaji

Mhe. Spika, wa agizo hili ni kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kukipa umuhimu mkubwa wa kilimo cham mpunga ili kupunguza uagizaji wa mchele nchini. Kutokana na umuhimu wa kilimo cha Mpunga wizara imetayarisha warka wa kupendekeza zao la mpunga na tayari umeridhiwa warka huo na Baraza la Mapinduzi. Warka huo umekuwa chachu katika kuwapatia wakulima mpunga ruzuku ya wastani wa 80% ya pembebeo.

Aidha, wizara inaendelea kushajihisha matumizi wa kilimo cha matrekta makubwa na madogo pamoja na dhana nyengine za kilimo ili kufikia dhamira ya kukifanya kilimo cha mpunga kiwe cha kisasa na chenye tija. Vile vile, Mhe. Spika, wizara inaendelea kusambaza taaluma za ukulima bora wa mpunga na uzalishali wa mbegu kwa kuanzisha na kuzutumia skuli za wakulima, jumuiya za wakulima, vishamba vya maeonesho, maonesho ya wakulima, ziara za kimafunzo za wakulima na mashamba ya majaribio.

Agizo la nne

Mhe. Spika, ni kuwapatia sare, yaani *overall* kwa mafundi ili kuongeza nidhamu na haiba nzuri ya kazi zao.

Utekelezaji

Wizara huwapatia vitendea kazi wafanyakazi wake pale hali ya fedha inaporuhusu. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2013/14 wizara ilitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa nguo za kazi za mafundi wa matrekta, hadi sasa fedha hizo hazijapatikaja.

Agizo la tano

Mhe. Spika, kubuni miradi mipya kuendelea na kuwasaidia wakulima kifedha na vifaa kwa wakulima wenye taaluma ya kutosha kilimo cha kisasa ikiwemo kilimo cha umwagiliaji maji.

Utekelezaji

Ni kwamba naomba kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba wizara imejipanga katika kubudi miradi mipya ya kuendeleza na kuwasaidia kifedha na vifaa wakulima wenye taaluma ya kutosha ya kilimo cha kisasa, ikiwemo cha umwagiliaji maji kwa kuunganisha na taasisi zisizo za kiserikali na washirika wa maendeleo wakiwemo *UWAMWIMA*, *TAHA*, *TAPP*, *ZAIDI* na *USID, Nafaka Project* kwa kupata nyezo na vifaa vya uzalishaji.

Agizo la sita

Mhe. Spika, ni kwamba wizara imeagizwa kwa kushirikiana na Idara ya Umwagiliaji maji Pemba wakae pamoja na wakulima wa bonde la Makombeni kwa ajili ya kukubaliana juu ya suala la kuweka sawa ardhi, yaani *land leveling and banding.*

Utekelezaji

Mhe. Spika, ni kwamba kazi ya kuweka sawa ardhi ya bonde la Makombeni imefanyika ambapo eneo la hekta tisa limewekwa sawa.

Agizo la saba

Mhe. Spika, ni kwamba kwa vile muda wa kukamika kwa matayarisho ya kilimo cha umwagiliaji maji katika bonde la Makombeni haujulikani, ni vizuri wakulima wa bonde hilo wakaruhusiwa kuendelea na kilimo chao cha kawaida kwa kufuata masharti na taratibu zilizowekwa za matumizi ya eneo hilo zikiwemo za kutuathiri mazingira ya eneo hilo ambayo yatahitaji katika shughuli za umwagiliaji maji.

Utekelezaji

Ni kwamba kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa miundo mbinu ya umwaguliaji maji katika bonde la Makombeni Mkoani huko Pemba. Wakulima wa bonde hilo wameanza kuingia katika kilimo cha mpunga wa umwaguliaji maji msimu wa vuli kwa mwaka 2014, kwa kufuata taratibu zote za kitaalum ikiwemo matumizi bora ya pembejeo na utunzani bora wa mashamba.

Mhe. Spika, kukamilika huku Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo walijionea wenyewe wakati wa ziara yao kisiwani Pemba.

Agizo la nane

Mhe. Spika, ni kwamba wizara imetakiwa kutoa elimu ya umwagiliaji maji wakulima waliomo katika mpango wa umwagiliaji maji.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Katika jitihada za makusudi za kuendeleza wakulima kiuzalishaji. wizara imeanzisha mpango mahususi wa kuwapatia elimu wa umwagiliaji maji ya kilimo cha mpunga wakulima wanaolima katika mabonde yaliomo katika mpango huo kwa mashirikiano kwa washirika wa maendeleo waliwemo *JICA* na *USID*.

Pia, juhudi zimechukuliwa kuanzishwa vishamba vya maonyesho katika mabonde ya umwagiliaji maji ambapo wakulima kadhaa katika mabonde mbali mbali na konde za umwagiliaji maji za Unguja na Pemba wameshikrikishwa katika ziara maalum za mafunzo ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji katika vituo vya mafunzo na utafiti ikiwemo *KTC* Moshi Tanzania Bara, Chuo cha Kilimo Kizimabi na *DACAO* Morogoro.

Agizo la tisa

Mhe. Spika, wizara imeagizwa kufatilia Shirila la Umeme (*ZECO)* kuona kuwa umeme unapelekwa katika vibanda vya kuendeshea *pump* katika bonde la Mtwango.Hasa ikizingatiwa kwamba malipo kwa ajili ya kazi hiyo yameshafanywa muda mrefu uliopita.

Utekelezaji

Mchakato wa kuunga umeme katika vibanda vya kuendeshea *pump* katika bonde la Mtwango umekamilika na hivi sasa wakulima tayari wanapata huduma ya maji ya kumwagilia mashambani kutoka kwenye *pumps* hizo.

Agizo la 10

Mhe. Spika, ni kwamba wizara imeagizwa kuharakisha taratibu za malipo ya fidia ya wananchi na wakulima waliokatiwa vipando vyao katika bonde la Mtwango.

Utekelezaji

Ni kwamba zoezi la malipo ya fidia kwa wananchi waliokatiwa vipando vyao kwa ajili ya kuunga umeme katika bonde la Mtwango limekamilika.

Agizo la 11

Mhe. Spika, wizara imeagizwa kwamba uongozi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani usimamie vyema taratibu za kazi ili kila *staff* akabidhiwe hadidu rejea zake. Aidha, manunuzi yote yafanywe kama sheria na taratibu za manuuzi za Serikali zinavyoelekeza.

Utekelezaji

Chuo cha Kilimo Kizimbani kimeshaanda Rasimu ya Muundo wa Utumishi ambao umeonesha majukumu ya kila mfanyakazi anapowajibika na dhamana zake. Vile vile, kwa sasa chuo kinae Afisa Manunuzi ambaye hufanya manunuzi kwa mujibu wa taratibu za Serikali. Kwa manunuzi makubwa yanayofikia kiwango cha tenda hufanywa kwa kupitia Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa maelezo zaidi muundo huu tayari umeshawasilishwa na Kamisheni ya Utumishi Serikalini na marekebisho ya awali yameshafanyika baada ya kufanyiwa mapitia na kamisheni hiyo.

Agizo la 12

Mhe. Spika, ni kwamba Chuo cha Kilimo Kizimbani kiwe na ulinzi wa uhakika usiku na mchana kwa masaa ishirini na nne.

Utekelezaji

Tume ya Utumishi Serikalini tayari imeshafanya usajili kwa kada ya ulinzi ili kuongeza ulinzi katika idara zake ikiwemo Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Agizo la 13

Chuo cha Kilimo Kizimbani kianzishe matumizi ya mawasiliano ya kisasa na kuwa na *website* yake wenyewe.

Utekelezaji

Mhe. Spika, chuo kimo katika mchakato katika kuanzisha *website* yake wenyewe kama ilivyoagizwa na Kamati, kwa sasa chuo kinatumia mtandao wa wizara kwa ajili ya mawasiliano na kuesha kazi zake. Aidha, chuo kinatumia mtandao wa *Agora* na *Hinari* kuongeza wigo wa upatikanaji wa taarifa za masomo na utafiti wa wanafunzi, wakulima, walimu na watafiti.

Agizo la 14

Ni kwamba Chuo cha Kilimo Kizimbani kipate mtalamu wa maabara ya mifugo.

Utekelezaji

Wizara iliomba nafasi mbili za wataalamu wa Maabara ya Mifugo na Kilimo kupitia taasisi husika.Bado tunaendelea kusubiri jawabu kutoka Utumishi Serikalini.

Agizo la 15

Mhe. Spika, ni kwamba Kitengo cha Lishe kwa kushirikiana na taasisi nyengine kama Wizara ya Afya kutoa mafunzo ya lishe kwa wananchi wengi zaidi na kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yaliyotolewa yanatumiwa ipasavyo kwa lengo la kupunguza idadi ya watoto waliodumaa.

Utekelezaji

Mhe. Spika, katika jitihada za kupunguza idadi ya watoto waliodumaa, Wizara ya Kilimo kwa mashirikiano na Wizara ya Afya zinaendelea kuchukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1.Kutoa mafunzo kwa akinamama juu ya njia sahihi za unyonyeshaji wa maziwa ya mama. Utayarishaji wa chakula bora kwa kutumia vyakula vya asili kwa ajili ya watoto wanaoachishwa maziwa, njia sahihi za utunzaji watoto walio chini ya umri wa miaka miwili. Mhe. Spika, mafunzo haya pia yanatolewa kwa akina baba kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya majukumu katika kuhakikisha lishe bora inapatikana kwa watoto wao.

2.Jitihada za wizara hizi mbili pia zimeelekezwa katika kushajihisha mabadiliko ya tabia ya ulaji (*eating habit*) kwa kuishawishi jamii kuachana na mila na tabia zilizo zoeleka ambazo kwa njia moja au nyengine zinaathiri lishe bora ya mtoto.

Agizo la 16

Mhe. Spika, Wizara iliagizwa kwamba elimu ya kutosha itolewe kwa wanajamii waliopo vijijini juu ya athari za kimangira zinatokana na uchimbaji ovyo wa mchanga na matofali.

Utekelezaji

Mhe. Spika, imetolewa katika maeneo ya Mwambe, Uwandani, Kiuyu Mbuyuni, Kangani, Finya, Tumbe, Kiungoni na Chambani kwa upande wa Pemba na Zingwezingwe, Donge na Pangatupu kwa upande wa Unguja kwa njia ya mikutano na semina.

Aidha, maeneo yanayochimbwa matofali na mchanga yamepandwa miti katika maeneo ya Zingwezingwe, Pangatupu na Dongembiji kwa upande kwa Unguja na Uwandani, Kiuyu Mbuyuni, Maziwa ng'ombe, Kishindeni, Kiungoni na Kangani kwa upande wa Pemba.

Kwa ujumla Mhe. Spika, kuhusu suala hili viongozi wa Wizara na Idara wanafanya ziara za mara kwa mara katika maeneo husika kuona kwamba utekelezaji wa agizo hili unakwenda kama ulivyopangwa.

Agizo la 16

Mhe. Spika, Wizara imeagizwa kusimamia kwamba utozaji wa ada kwa wenye magari makubwa ya kuchimba mchanga utizamwe upya kuepusha Serikali na upotevu wa fedha unaoweza kutokea kwa kutoza ada ya kifusi ya gari kubwa sawa na gari ndogo.

Utekelezaji

Mhe. Spika, mali asili zote zisizorejesheka ikiwa mawe, kifusi, mchanga, kokoto, udongo au vumbi zinatozwa kwa mujibu wa kiwango cha tani moja ni shilingi elfu moja. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya Mazingira Na. 6466 ya 2011 *Vol.* CXX2.

Agizo la 18

Wizara iwaelekeze wakulima na wafugaji njia watakazoweza kupata mikopo ili waweze kupata mitaji ya kujiendeleza.

Utekelezaji

Mhe. Spika, juhudi kubwa zimeshafanyika kuwasaidia wakulima hao kupitia programu na miradi mbali mbali ikiwemo miradi ya *PADEP* na *MACEMP* kwa kuwezesha wakulima na wafugaji kuzalisha mazao ya chakula, mboga mboga, kupatiwa ng'ombe, maboti ya kuvulia pamoja na mashine zake kwa lengo la kuwakomboa wananchi hao kiuchumi.

Hata hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana na Wanawake na Watoto katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Agizo la 19

Wizara ya Kilimo na Maliasili imeagizwa ibuni miradi mengine ya kuwanufaisha wakulima na wafugaji kwa lengo la kuwaendeleza baada ya miradi iliopo kumaliza au kumalizika muda wake.

Utekelezaji

Wizara ya Kilimo na Maliasili Mhe. Spika, umeupokea ushauri huo na inaendelea na juhudi za kuandika mapendekezo *(project proposal)* ya miradi na kuiwasilisha au kuwasilisha mapendekezo hayo kwa washirika wa maendeleo. Sambamba na hilo, Wizara inaendelea na kufanya mazungumzo na Shirika la Maendeleo la Kimataifa *(IFAD)* kuhusiana na kuendelea na programu ya huduma za mifugo kwa wafugaji *(ASDP- Livestock).*

Agizo la 20

Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ishirikiane na Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) na Shirika la Umme (*ZECO*) kutafuta uwezekano wa kuwasaidia wanajamii juu ya kupata unafuu wa gharama za matumizi ya maji katika mashamba yao.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara imejipanga kushirikiana na Shirika la Umeme (*ZECO*) kwa ajili ya kuona uwezekano wa namna ya kuwasaidia wanajamii katika kupata unafuu wa gharama za matumizi ya maji kwenye mashamba yao na maeneo mengine ya kilimo. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa uvunaji wa maji ya mvua katika mabonde yote ya umwagiliaji maji.

Agizo la 21

Mhe. Spika, ni kwamba Serikali kwa haraka isaidie kudhibiti wimbi la wizi wa mifugo na mazao ya kilimo kwa lengo la kuwaondoshea kero wakulima.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara ilitayarisha na kuwasilisha ripoti ya wizi wa mazao mbele ya Baraza la Mapinduzi iliyokuwa ikielezea suala la wizi kwa upande wa Unguja na Pemba kwa madhumuni ya kupata ushauri juu ya udhibiti wa wimbi la wizi wa mifugo na mazao ya kilimo.

Baada ya uwasilishaji wa ripoti hiyo Wajumbe walishauri kwamba vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na viongozi wa Wilaya na Mikoa, nao washirikishwe kufanikisha suala hili.

Agizo la 22

Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ipunguze urasimu na kufanya juhudi za makusudi kuongeza kasi ya utekelezaji katika maeneo yanayopaswa kufanywa na Wizara katika mradi wa *MIVARF*.

Utekelezaji

Utekelezaji wa kazi za *MIVARF* ni sekta binafsi na kazi ya Wizara ni uratibu, usimamizi na ufuatiliaji. Katika hilo Wizara inashirikiana na Ofisi ya Programu Arusha na kuwasiliana na washirika wa maendeleo kuhimiza utekelezaji wa majukumu yao na hasa suala la kupata ridhaa *(no objection)* ya kuendelea hatua nyengine ya utekelezaji. Kwa ujumla kazi tatu za *MIVARF* ikiwa ni ukarabati wa barabara, kuwawezesha wazalishaji na kuwaunganisha na masoko na kazi zinazohusika na huduma za kifedha vijijini zinatekelezwa na Idara ya Ushirika na zinaendelea kwa kasi ya kuridhisha.

Agizo la 23

Mhe. Spika, linahusu mikakati inayohusisha wahisani wa maendeleo ambayo ina tija kubwa zaidi kwa wananchi iharakishwe kukamilishwa. Taasisi za Serikali zitoe kipa umbele maalum katika jambo hili ili kuzidisha moyo wa imani ya washirika wa maendeleo kwa Serikali yetu.

Utekelezaji

Wizara ya Kilimo na Maliasili inalichukua pendekezo hili la suala la taasisi ya Serikali kutoa kipaumbele katika kuharakisha na kukamilisha mikataba inayohusisha wahisani wa maendeleo ambayo ina tija zaidi kubwa zaidi kwa wananchi.Wizara itaendeleza juhudi hizi hasa kwa upande wa mikataba inayoihusu sekta ya kilimo ili tulete mafanikio kwa wananchi na kwa washirika wa maendeleo.

Agizo la 24

Mhe. Spika, ni kwamba pawepo utaratibu maalum utakaowashughulikia watendaji watakaopata ajali wakiwemo kazini katika ukarabati wa barabara.

Utekelezaji

Kwa kuwa kazi za programu zinatekelezwa na watoa huduma binafsi. Kwa mfano wakandarasi wanaokarabati barabara. Utaratibu wa kushughulikia wafanyakazi wao pindi wakipata matatizo wakiwa kazini upo kupitia Bima za kampuni.

Agizo la 25

Mhe. Spika, linasema kwamba kupitia mradi wa ujenzi wa fusi ya *MIVARF,* Wizara iangalie uwekezekano wa kuiunganisha barabara ya Ukutini Mtangani huko Pemba itengenezwe hadi Kichaka ambako kuna vikundi vingi vya *SACCO's* na kilimo kikubwa cha migomba.

Utekelezaji

Ushauri huu ni mzuri lakini utekelezaji wake ni mgumu kwa kuwa sehemu hiyo ya barabara haikuwemo kwenye mpango wa awali uliowasilishwa na kupitishwa kufanyiwa usanifu na baadae bajeti yake.Hata hivyo, huenda suala hili likazungumzika kati ya pande mbili husika wakati mkandarasi akifika kwenye eneo hilo na ikiwa mazingira ya kiutawala na kifedha yatakuwa mazuri na salama.

Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan Hija, tunakuomba usubiri asaa kheri mambo huenda yakawa mazuri. *(Makofi)*

Agizo la 26

Mhe. Spika, linahusu Wizara itayarishe kati ya barabara zilizomo katika mpango wa kujengwa kwa lami na Serikali na zile ziliomo katika mradi *MIVARF* kwa kujengwa kwa kifusi. Yaani Wizara itafuatishe zile ambazo zitajengwa kwa lami na zile ambazo zitajengwa na fusi katika mradi huu wa *MIVARF*.

Utekelezaji

Wizara kwa mashirikiano na uongozi wa Wilaya ilizitoa barabara zote ambazo awali ziliorodheshwa kwenye mpango wa *MIVARF* na ukarabati kwa kiwango cha kifusi. Baada ya kupata taarifa kuwa baadhi ya barabara hizo zimo kwenye mpango mkuu wa Serikali wa kuzijenga kwa kiwango cha lami. Mfano wa barabara hizo ni Kitope/Pangeni, Kilombero, Jendele/Mchele-Unguja Ukuu na barabara ya Jumbi/Mkoani.

Agizo la 27

Mhe. Spika, linasema kwamba Wizara iharakishe kupata hati miliki za maeneo yote ya misitu yaliopo katika kuhifadhi kuepusha migogoro na uvamizi wa ardhi unaoweza kujitokeza.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara imeshapima maeneo yote ya hifadhi ya misitu na kupatiwa michoro. Hivi sasa jitihada za ufuatiliaji wa kupatikana kwa hati miliki za maeneo hayo pamoja na mabonde mengine yaliyokwishapimwa bado zinaendelea.

Agizo la 28

Mhe. Spika, linazungumzia kwamba miche itunzwe vitaluni mpaka inapokuwa mikubwa kidogo kabla ya kupelekwa shambani kuepuka kufa kwa wingi baada ya kupandikizwa.

Suala kama hili Mhe. Naibu Waziri, alijibu asubuhi hii ya leo.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kawaida hutoa miche ya mikarafuu kuanzia miezi 18 ikiwa na urefu wa kuanzia *centimeters* 30 na kuendelea kulingana na aina ya mche wenyewe. Kwa mfano miche ya matunda ni kati ya miezi mitatu hadi tisa na urefu inategemea aina ya mti.

Mhe. Spika, miche yote hutolewa kwa wakulima ni lazima iwe imetimiza muda wake uliopangiwa kwa kukaa kwenye vitalu ili kupunguza vifo vya miche hiyo ya kupandikizwa mashambani.

Mhe. Naibu Waziri, alizungumza kwa kujibu suala hili vizuri sana asubuhi.

Agizo la 29

Mhe. Spika, linazungumzia kwamba Wizara itoe elimu zaidi juu ya athari kubwa ya kukatwa miti kwa matumizi mbali mbali ya wananchi.

Utekelezaji

Wizara inaendelea kutoa elimu kuhusu athari za ukataji wa miti kupitia magazeti, redio, televisheni, makongamano na mikutano.

Agizo la 30

Mhe. Spika, Wizara imeagizwa iwahamasishe wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya misitu ya asili wanaojishughulika moja kwa moja na ukataji wa miti, wakiwemo wachomaji chokaa, kuunda vikundi kupatia elimu na kuhamasishwa kupanda miti kwa wingi itakayoweza kufyoza hewa ukaa *(carbondioxide)* kwa kiasi kikubwa.

Utekelezaji

Wizara imehamasisha wananchi na imewezesha kuunda kuunda vikundi 45; Unguja vipo 29 na Pemba vipo 16 kwa lengo la kusimamia raslimali za misitu ya asili kwa ajili ya kuhifadhi ya misitu na kuuza hewa ukaa *(carbondioxide)*.

Agizo la 31

Mhe. Spika, linasema kwamba elimu maalum itolewe kwa wananchi kuwafahamisha kwamba ujenzi kwa kutumia saruji una nafuu zaidi kigharama kuliko kutumia chokaa. Elimu hiyo itapunguza kasi ya kukatwa miti kwa uchomaji wa chokaa.

Utekelezaji

Katika jitihada za kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya uchomaji wa chokaa, Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikiendelea kuelimisha jamii. Aidha, jamii yenyewe imekuwa na mwamko mkubwa juu ya matumizi ya saruji kwenye ujenzi ukilinganisha na chokaa.

Agizo la 32

Mhe. Spika, linazungumzia kwamba Wizara kwa kushirikiana na wananchi ipande mikandaa katika maeneo yaliopo kwenye hatari ya kuathiriwa na uharibifu wa mazingira yakiwemo maeneo ya Mwambe kule Pemba ili kupunguza uharibu mkubwa wa mazingira unaofanywa katika maeneo hayo na kuongeza uhifadhi wa ardhi.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara imekuwa ikiwashirikisha wanajamii katika upandaji wa miti ya mikanda maeneo ya wazi, kiasi cha *hectare* 123 zimeshapanda mikanda ikiwemo Mwambe na Kangagani. Aidha, wanajamii wamehamasishwa kuweka mizinga ya nyuki ili kuongeza uhifadhi wa maeneo hayo.

Agizo la 33

Mhe. Spika, walililopewa Wizara linahusu au linazungumzia kwamba katika mpango wa kuimarisha msitu wa Kangagani, Wizara iwakutanishe wana kijiji wa Shehia zote zinazohusika ili kusuluhisha migogoro iliyojitokeza na kupata maoni yao juu ya msitu huo kabla ya kuanza kutekeleza mpango uliokusudiwa.

Utekelezaji

Mhe. Spika, Wizara imekusanya maoni kutoka vijiji vyote vilivyo karibu na msitu wa Kangagani. Vijiji vya Ole, Kiuyu Minungwini, Kojani, kambini na Mjini Ole vyote vilishirikishwa.

Aidha, Wizara iliwashirikisha wafuatao:-

- Mkuu wa Wilaya ya Wete
- Waheshimiwa Madiwani
- Masheha wa vijiji husika

Ili kuweza kutambua mipaka ya msitu huo. Baada ya makubaliano hayo ya pamoja jina la msitu huo litaitwa Malilini. Lakini zaidi ni kwamba hati ya tangazo la dhamira ya kuhifadhi *(Notice of Intent)* ya siku 90 imeshapelekwa kwa ajili ya kujitangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali kwa jina la msitu wa hifadhi liitwe Malilini.

Agizo la 34

Mhe. Spika, Wizara imetakiwa izidishe kazi ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi katika ufugaji wa nyuki ili waweze kupata asali ambayo kwa sasa ina soko zaidi na kuweza kuinua kipato chao.

Utekelezaji

Wizara inaendelea kuwahamasisha wana jamii kwa kuwapatia elimu na mizinga ya kufugia nyuki bila ya malipo. Jumla ya vikundi 126; vikundi 75 vipo Unguja na vikundi 51 vipo Pemba na wafugaji mmoja mmoja wapatao 1264 ambapo 2100 wapo Unguja na 564 wapo Pemba wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki kwa lengo kujiongezea mapato sambamba na uhifadhi wa misitu.

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndiyo maagizo yaliyopatiwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka uliopita na utekelezaji wa Wizara kama tulivyouonesha.

Lakini niishukuru sana Kamati kwa kweli kwa michango yao zaidi waliyotupa wakati tulipokuwa *field* na huko hasa ndiko kwenye kilimo. Kwa hivyo, naomba sana tuzidi kushirikiana kuwaendeleza wakulima wetu na wapandaji miti wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe.Waziri. Sasa tukamilishe safu ya kusikiliza ripoti za utekelezaji kwa kumkaribisha Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kwa heshima zote nitowe maelezo ya utekelezaji kwa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kushirikiana kwa mara nyengine tena kukutana tukiwa wazima wa afya njema. Naomba kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua fursa hii adhimu kutoa mkono wangu wa pole kwa msiba mkubwa uliotokea wa kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Marehemu Salmin Awadh Salmin, ambaye pia alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni. Mwenyezi Mungu atupe subra kwa sote na amlaze Marehemu pahala pema peponi, *Amin*.

Mhe. Spika, pia naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Makamu Mwenyekiti Mhe. Hija Hassan Hija, pamoja na Kamati yake yote ya Fedha, Biashara na Kilimo, kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia na yote yanayopatikana hapa katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sehemu kubwa, inatokana na ushauri pamoja na miongozo na maelekezo yanayochangiwa na Kamati hiyo. Ushirikiano wetu baina ya Kamati na wizara ni mzuri na ndio unatufanya kuweza kutumia majukumu yetu ya kuendeleza biashara, viwanda na kuwasaidia wazalishaji na wajasiriamali kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa wizara yangu. Tumaini ni kuwa maelekezo ya Baraza hili tukufu ni sehemu kubwa ya wizara yangu kupata mafanikio katika utekelezaji wa malengo yake. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote muendelee kushirikiana na wizara yangu ili tuweze kuimarisha na kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelekezo haya ya shukrani, naomba kueleza kwamba katika Ripoti za Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka 2013/2014, wizara iliagizwa na Kamati kutekeleza maagizo 20, ambayo utekelezaji wake umo kama ulivyo katika taarifa hii, ambapo la kwanza ilikuwa;

Agizo la kwanza

Wizara iandae mikakati na taratibu maalum tulofanya ukaguzi maalum wa kuwepo katika maduka yao, wakati wa ukaguzi wa maduka ulipofanyika, ikiwemo kuwapatia elimu zaidi juu ya umuhimu wa ukaguzi na athari za kuwepo kwao wakati wa ukaguzi huo.

Utekelezaji

Wizara yangu imetekeleza agizo hilo kwa kutoa elimu na elimu hiyo itaendelea kutolewa na hasa wakati wa ukaguzi kwa kuwashirikisha pamoja na Masheha, juu ya umuhimu kufanyiwa uhakiki wa mezani na maduka kwa lengo la kumlinda mtumiaji.

Agizo la pili

Wizara iandae utaratibu katika kuwapatia Kanuni za biashara wafanyabiashara wanaopewa leseni, ili kuongeza uelewa juu ya taratibu za uendeshaji wa uendeshaji biashara kisheria.

Utekelezaji

Hatua hii inachukuliwa kugawa Kanuni baada ya kukamilika hivi karibuni.

Agizo la tatu

Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza posho la shilingi 10, 000 kwa siku, ambalo hulipwa Masheha wanaposhirikiana na wakaguzi wa mezani, kwani posho hiyo hailingani na hali ya maisha kwa sasa.

Utekelezaji
Wizara yangu imeona suala hilo ni kweli na linazingatiwa kulingana na hali ya bajeti itakavyokuwa mwaka unaokuja.

Agizo la nne

Kutokana na umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa kiwanda cha usarifu wa chumvi Wawi Pemba, katika kutoa fursa za ajira na kuchangia hali ya afya za wananchi, kwa kuwaonesha chumvi yenye madini joto. Kamati inaisihi wizara kuendelea kuwa karibu zaidi na kiwanda hicho, ikiwa ni pamoja na kufuatilia kwa karibu matokeo ya utafiti kwa kiwanda hicho, ilichofanywa na Shirika la Utafiti na *TIRDO.*

Utekelezaji

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kutumia wataalamu wa ndani walifanya tafiti mbili kuhusu kiwanda hicho.
Agizo la kwanza

Mfumo wa kiutawala wa kiwanda.

Agizo la pili

Utafutaji masoko ya kudumu ya chumvi. Kwa upande wa utafutaji wa matokeo ya utafiti yalifanywa na *TIRDO,* baadhi ya kasoro za kiwanda hicho zilielezwa, ni pamoja na kutokuwepo na uongozi mzuri na madhubuti wa kuanzisha kiwanda kama mradi wa biashara.

Utekelezaji

Kukosekana kwa mpango madhubuti wa kutatua na kumwilika chumvi inayosafirishwa kiwandani.

Agizo la tatu

Jumuiya ya *ZASPO* imeandikishwa kama *NGO*, na huo sio mfumo sahihi wa kuanzisha kiwanda kinachotarajiwa kutoa faida na kufanya biashara.

Utekelezaji

Wizara inaendelea na mazungumzo na kiwanda hicho, ili kuzitafutia ufumbuzi taarifa zote hizo, ili kiwanda hicho kiwe Kiwanda cha Biashara na sio *NGO*.

Agizo la tano

Kamati inaitaka Serikali kukabidhi nyumba 150 za Kiwanda cha Sukari Mahonda kwa uongozi wa kiwanda hicho, ili waweze kuzitumia kwa ajili ya wafanyakazi wake kama ilivyo lengo lililokusudiwa la kujengwa kwa nyumba hizo.

Utekelezaji

Suala la nyumba za Kiwanda cha Sukari liko katika mkataba kati ya kiwanda na Serikali na linashughulikiwa na Wizara ya Fedha.

Agizo la sita

Taasisi zinazohusika pamoja na wananchi wanapaswa kutoa mashirikiano ya dhati kwa uongozi wa kiwanda hicho cha sukari katika kudhibiti vitendo vya kukihujumu kiwanda hivyo, ikiwemo uharibifu na wizi wa miwa, kwa vile manufaa ya kiwanda hicho ikiwemo ajira ni ya wananchi wenyewe.

Utekelezaji

Viongozi mbali mbali wa Mkoa wa Kaskazini na Wilaya ya Kaskazini B, pamoja na viongozi wa kitaifa kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiwaasa wananchi wanaopakana na mashamba ya miwa, kuepusha hujuma za aina zote kwa mali za kiwanda, yakiwemo mashamba ya miwa.

Agizo la saba

Kwa vile vikundi vya uhamasishaji vina umuhimu mkubwa katika kupunguza tatizo sugu la ajira hapa nchini, wizara inapaswa kuwa karibu zaidi na vikundi hivyo, kwa kuvishughulikia na kuvisaidia kikamilifu ili kuviimarisha.

Utekelezaji

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inavitembelea nakuvipa msaada wa mafunzo na ushauri vikundi vya wajasiriamali mara kwa mara. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai/Disemba wizara imetoa mafunzo ya siku tatu, kwa vikundi 17 vya Mkoa wa Kaskazini Unguja na vikundi vya wajasiriamali 104 vimekaguliwa kwa Unguja na Pemba.

Agizo la nane

Kamati inaishauri taasisi ya viwango Zanzibar kufanya jitihada za kutafuta wataalamu wa fani zinazohitajika, ili taasisi iweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Utekelezaji

Kazi hii inatekelezwa, hivi karibuni wataalamu 11 wapya wameshaajiriwa.

Agizo la tisa

Kwa kuwa gharama za kuanzisha maabara ni kubwa, Kamati inaishauri Serikali kujidhatiti kikamilifu kifedha, ili malengo ya kuanzishwa kwa taasisi za *ZBS* yaweze kufanikiwa.

Utekelezaji

ZBS inaangalia uwezekano wa maabara ziliopo nchini, ili iweze kufanyakazi zake kwa kuanzia.

Agizo la 10

Kuna haja kubwa ya kutilia mkazo zaidi suala la kuongeza ununuzi wa mizani za kisasa za upimaji wa karafuu, ili kuondoa malalamiko mbali mbali yanayohusiana na upimaji wa karafuu.

Utekelezaji

Juhudi zimeendelea kuchukuliwa kuongeza mizani hizo, ambapo mizani 14 zimeshanunuliwa.

Agizo la 11

Wizara kwa kushirikiana na wananchi pamoja na vyombo husika, ibuni mikakati maalum ya kudhibiti wizi wa karafuu unaofanyika kwa kukata matawi ya karafuu yenye karafuu nyingi, kwani aina hiyo ya wizi hudhoofisha pia ustawi wa mikarafuu yenyewe.

Utekelezaji

Shirika la Biashara la Taifa la *ZSTC*, linaendelea na taratibu za kutoa elimu juu ya taathira au athari za ukataji wa mikarafuu michanga.

Agizo la 12

Kwa sababu Shirika la *ZSTC* liko katika mageuzi makubwa, hoteli ya makonyo nayo inahitaji mageuzi kwa kufanyiwa ukarabati mkubwa, kuimarisha kuwa safi na kuweka utaratibu mzuri wa zamu za wafanyakazi.

Utekelezaji

Aidha, wizara itowe ushirikiano mkubwa katika kufanikisha usafishaji wa hoteli hiyo. Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC* limekamilisha ukarabati wa ukumbi wa makonyo, pamoja na kuimarisha ulinzi katika eneo hilo kwa kujenga uzio.

Aidha, *ZSTC* itaifanyia ukarabati hoteli ya Makonyo, ili nayo iweze kuwa katika hadhi ya ukumbi huo.

Agizo la 13

Kamati inalitaka shirika kuhakikisha kwamba karafuu kidogo zinazobakia baada ya kupimwa, zinarudishwa kwa wauzaji wenyewe na iwapo zikihitajika kuchukuliwa na shirika zilipiwe au zichukuliwe na shirika baada ya kupatikana ridhaa kutoka kwa wauzaji wenyewe.

Utekelezaji

Mizani 14 zilizonunuliwa zina uwezo wa kupima uzito hata uzito mdogo, kwa hivyo, tatizo hilo litaondoka.

Agizo la 14

Pindi inapotokezea mchukuzi kufariki, shirika ni vizuri kuwa mstari wa mbele katika kutoa mchango wake, hususan wa kifedha kwa ajili ya mazishi na wafiwa wa marehemu.

Utekelezaji

Suala hili limezingatiwa katika Sheria ya Maendeleo ya Karafuu na Kanuni zake na zitatekelezwa.

Agizo la 15

Kwa vile wachukuzi wanafanya kazi muhimu katika kufanikisha usafirishaji wa karafuu. Kamati inashauri kuwa ipo haja kwa Shirika la *ZSTC* kuangalia kwa jicho la huruma kwa kuyazingatia madai yao ya msingi, yakiwemo nyongeza ya malipo ya uchukuzi wa magunia ya karafuu, nyongeza ilipwe baada ya saa za kazi au *overtime*.

Utekelezaji

Shirika la *ZSTC* tayari limeshafanya marekebisho ya malipo ya wachukuzi, kwa kufanya nyongeza ya asilimia 50 ya malipo ya awali na malipo ya muda wa ziada, analipwa asilimia 30 kwa kazi ya siku hiyo.

Agizo la 16

Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, zioneshe juhudi ya kudhibiti magendo ya karafuu kwa kuwa karibu zaidi na wananchi, ili kuweza kutambua mbinu mbali mbali inayotumiwa na wajanja wanaosafirisha karafuu kwa njia za magendo na kuchukua hatua zifaazo.

Utekelezaji

Kikosi maalum kilichoundwa na Serikali kinaendelea na kushirikiana na vyombo vya ulinzi katika ulinzi wa karafuu na hali ni nzuri.

Agizo la 17

Kuna haja kwa shirika kufanya juhudi kubwa zaidi ya kuzitangaza na kuzitafutia masoko makubwa zaidi ya ndani na nje, bidhaa zinazozalishwa katika shamba la Mtakata Pemba, yakiwemo mafuta ya aina mbali mbali.

Utekelezaji

Shirika la *ZSTC* limesaini hati ya makubaliano na Kampuni ya *Lane* ya Japani, kwa ajili ya kuzisarifu na kuzitafutia masoko bidhaa zinazotokana na mafuta ya mimea.

Agizo la 18

Kamati inatoa ombi kwa Serikali kuwa Ofisi ya *ZSTC* Dar es Salaam isifungwe, kwa vile itaweza kutangaza bidhaa za shirika la Zanzibar katika Soko la Afrika Mashariki na kwengineko. Huo ndio msimamo wa Serikali pia, kwa hivyo, haitofungwa ofisi ya Dar es Salaam.

Kamati inapendekeza kuwa shirika lifanye utafiti wa kina juu ya namna kituo hicho kitakavyoendelezwa.

Utekelezaji

Shirika la *ZSTC* limeshasaini mkataba na Chuo cha Uongozi wa Fedha *ZIFA*, kwa ajili ya kufanya utafiti kulifanyia kulifanyia tathmini tawi la Dar es Salaam.

Agizo la 20

Imeagizwa kwamba shirika linafanya mageuzi kwa upande wa Zanzibar, linapaswa pia kuyaagiza mageuzi yake katika ofisi yake ya Dar es Salaam, ili kutumia na soko liliopo Dar es Salaam.

Utekelezaji

Shirika linakubaliana na maelekezo hayo na itaingiza katika mpango kazi wake wa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo, nashukuru sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ili na yeye kuwasilisha ripoti ya mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo): Muhutasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kutukutanisha hapa leo, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kikatiba ya kuisimamia Serikali na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa.

Aidha, naomba nikushukuru wewe Mhe Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kuwasilisha muhutasari wa ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, lakini kabla ya kuwasilisha muhtasari huo, naomba kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na mimi kuchukua nafasi hii kuungana na walio wengi kwa kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa, familia, marafiki na wananchi wa Jimbo la Magomeni kutokana na kifo cha Mhe. Salmin Awadh Salmin ambae pamoja na nyadhifa kadhaa alizokuwa nazo, alikuwa pia ni Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, kwa hakika Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepokea kwa huzuni na mshtuko mkubwa kifo cha Mwenyekiti wake huyo mahiri, kilichotokea siku ya Alhamis, tarehe 19/2/2015 baada ya kuugua ghafla akiwa katika kikao cha kikazi cha kichama hapo Kisiwandui.

Mhe. Spika, akiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mhe. Salmin alikuwa ni kiongozi imara, mbunifu, mchapakazi wa kweli, mstahamilivu, mwenye nidhamu, mwenye wingi wa hekima, busara, upendo na mashirikiano. Mhe. Salmin, alikuwa ni Kiongozi shupavu, mwenye kujiamini na mwenye msimamo usioyumba katika kutetea masuala mbali mbali yanayohusu maslahi ya nchi hii na watu wake.

Mhe. Spika, sisi wajumbe wako wa Kamati hii tumejifunza mengi mazuri, kutoka kwa Mhe. Salmin, ikiwemo ujasiri na kuwa na upeo na mawazo ya kujenga na kutetea hoja zenye maslahi ya nchi. Bila ya shaka sisi wajumbe wa Kamati hii tuliobakia tutaendelea kuthamini na kuuenzi mchango mkubwa alioutoa kiongozi wetu huyo mpendwa alipokuwa na Kamati hii, kwa kuiga na kufuata yale yote mazuri aliyotuachia.Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke pahala pema Peponi roho ya Marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin. *Amin*.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2014/2015, kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza lako tukufu toleo la 2012.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba nikushukuru wewe Mhe, Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Mratibu wa Shughuli za Kamati na watendaji wako wote kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake zote bila ya matatizo kwa kipindi chote.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati, kwa wajumbe na makatibu wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo, kwa mashirikiano yao makubwa waliyoonesha katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi za Kamati. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano yao ndio nyenzo pekee iliyoifanya Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 ya Kanuni za Baraza lako tukufu toleo la 2012. Aidha, majukumu ya Kamati hii yamefafanuliwa katika

kanuni ya 110 ya Kanuni hizo za Baraza. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati hii imepewa dhima ya kusimamia wizara tatu (3) zifuatazo:-

1. Wizara ya Kilimo na Maliasili
2. Wizara ya Fedha na
3. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Spika, kwa upande wa muundo wa kamati, Kabla ya Kifo cha Mhe Salmin Awadh Salmin, ambae alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati hii, ilikuwa imeundwa na wajumbe saba (7) na makatibu wawili. Lakini kwa sasa Kamati hii imeundwa na wajumbe sita (6) na makatibu wawili. Kama nilivyoeleza hapo awali kuwa Kamati imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa baina ya wajumbe, pamoja na makatibu wake. Hivyo, kwa kuthamini mchango wao mkubwa, naomba niwatambulishe kwa majina wajumbe na makatibu hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hija Hassan Hija -Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. Asha Abdu Haji -Mjumbe
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub -Mjumbe
4. Mhe. Hamad Masoud Hamad -Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad -Mjumbe
6. Mhe. Viwe Khamis Abdalla -Mjumbe
7. Ndg. Haji Khatib Haji -Katibu
8. Ndg. Fatma Omar Ali -Katibu

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Kamati pia ilipata nafasi ya kwenda Dubai kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Ofisi ya Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) iliyopo huko Dubai mnamo mwezi wa Oktoba, 2014.

WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Mhe. Spika, Sekta ya Kilimo na Maliasili bado inaenedelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar, kwa kutoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, uhakika wa chakula, lishe na afya za wananchi walio wengi vijijini na mijini. Takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, sekta za kilimo na maliasili, zilichangia asilimia 30 ya pato la Taifa na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hii kwa ajira na kipato.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu huo Kamati inaiomba sana Serikali kufanya juhudi za makusudi, zitakazowezesha kazi za wizara hii kupata fedha za kutosha hususan zile kazi za maendeleo, ili ile kauli mbiu ya "Kuleta Mapinduzi ya Kilimo" iweze kutekelezwa kwa vitendo, kwani kwa vyovyote vile asilimia 15 tu ya fedha za maendeleo iliyopatikana hadi Novemba, 2014 ni finyu sana na kamwe haiwezi kutimiza kikamilifu azma ya Serikali ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa kuona kuwa kazi ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha Usarifu wa Mazao kiichopo Kizimbani, imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu sasa na Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla imeshindwa kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ambao imebakia kwa asilimia ishirini (20) tu kwani asilimia 80 ya ujenzi huo imekamilika wakati ujenzi huo ulipokuwa chini ya usimamizi wa *KOICA* kupitia kandarasi walioajiriwa na shirika hilo.

Mhe. Spika, Kamati ilizidi kusononeshwa kuona kuwa Wizara imeshindwa kupata Shillingi Mia Tatu Sitini na Moja Millioni, Laki Nane na Themanini Elfu tu ambazo zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho. Cha kutia uchungu zaidi ni pale Kamati iliposhuhudia mashine na vifaa mbali mbali vilivyopo katika ghala la Wizara, Bandarini, Malindi ambavyo viliingizwa nchini

muda mrefu sasa, vimekaa bure vikisubiri muda wa kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho ambao haujulikani na baadhi ya vifaa hivyo zikiwemo *chamical reagents* za maabara vimeanza kuharibika.

Mhe. Spika, kwa kuwa kituo hicho kitakachokuwa na maabara mbali mbali za usarifu wa mazao ni muhimu sana sio tu kwa wakulima lakini pia kwa wadau wengine ikiwemo Taasisi ya Viwango (*ZBS*). Na kwa kuwa ujenzi wa kituo hicho umeshafikia hatua kubwa za ujenzi wake.Na kwa kuwa mashine na vifaa kwa ajili ya kituo hicho vimekaa bure kwa muda mrefu vikisubiri kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho.

Hivyo basi, Kamati inaitaka Wizara na Serikali kwa ujumla kutoa kipaumbele maalum katika kulikamilisha jengo la kituo hicho cha usarifu wa mazao Kizimbani kwani Kamati haioni sababu za msingi kwa Serikali kushindwa kulikamilisha jengo hilo muhmu isipokuwa ni kukosa kuwa na mipango madhubuti na kukosa kupanga vipaumbele vyake kwa umakini.

PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA MASOKO NA UONGEZAJI THAMANI, MAZAO NA HUDUMA ZA FEDHA VIJIJINI (*MIVARF*)

Mhe. Spika, pamoja na kuendelea vizuri kwa ujenzi wa barabara zinazojengwa kwa kiwango cha kifusi kupitia mradi wa *'MIVARF'*, Kamati imebaini changamoto kadhaa ikiwemo ile ya kusambaa kwa vumbi linalotokana na barabara hizo kunakohatarisha afya za wananchi wanaoishi katika maeneo ya karibu na barabara hizo pamoja na kuchafua mazingira na haiba ya maeneo hayo.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaitaka Wizara ya Kilimo na Maliasili ishirikiane na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kuona uwezekano wa kuziimarisha zaidi barabara hizo kwa ajili ya kuwaepusha wananchi wanaoishi karibu na barabara hizo kutokana na athari ya vumbi kwa afya zao pamoja na kuzifanya barabara hizo ziwe imara zaidi.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Spika, Uhaba na uchelewaji wa fedha za matayarisho ya kilimo cha mpunga, upungufu na uchakavu wa vitendea kazi ikiwemo majembe ya matrekta, uhaba wa mafundi na madereva wa matrekta pamoja na kuchelewa kwa wakulima kulipia gharama za kulimiwa mashamba yao kwa wakati, zimeendelea kuwa ni miongoni mwa changamoto sugu zinazorotesha kazi za idara hii ambayo ndio kiini cha Wizara hii.

Mhe. Spika, Kwa kuwa matayarisho ya kilimo cha mpunga hufanywa kwa wakati maalum ni vyema Wizara na Serikali kujipanga vizuri zaidi kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha wa uhakika na wa wakati ili kuwaondoshea wakulima usumbufu unaotokana na athari ya kuchelewa kwa matayarisho ya mapema ya kilimo hicho.

Mhe. Spika, kwa kuwa kumejitokeza tatizo la udhaifu wa vifaa vya matrekta mapya kulingana na ugumu wa ardhi yetu, Kamati inaishauri Wizara kufanya utafiti wa kina juu ya vifaa vilivyomo katika matrekta kabla ya kununua matrekta hayo ili matrekta yanayonunuliwa yaweze kumudu hali halisi ya ardhi katika mashamba mbali mbali.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Spika, Kamati hairidhishwi hata kidogo na kitendo cha kutoingiziwa fedha kazi muhimu ya ukarabati wa ghala la Hifadhi ya Chakula na kwa kuwa ni muda mrefu sasa kazi hii haijafanyika kutokana na kutoingiziwa fedha, ipo haja sasa kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuona umuhimu mkubwa wa nchi yetu kuwa na ghala la Hifadhi ya Chakula linalofanyakazi ili kuweza kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula hapa nchini.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Jukumu kubwa la Chuo hiki ni kutoa mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti. Pamoja na jukumu hilo, Chuo pia kina jukumu la kulisimamia na kuliendeleza shamba la RAZABA lililopo Bagamoyo, Tanzania Bara.

SHAMBA LA RAZABA, MAKURUNGE - BAGAMOYO.

Mhe. Spika, Wakati Kamati ilipokuwa katika shamba la Makurunge, Bagamoyo ilipewa taarifa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha shamba hilo la Mifugo ya Ngo'mbe wa nyama mnamo mwaka 1976 ili kukidhi mahitajio yake ya kitoweo nchini ambapo wakati huo shamba hilo lilikuwa na ukubwa wa hekta zaidi ya 28,000.

Aidha, licha ya kusitishwa kwa shughuli za mifugo kwa muda mrefu, mnamo mwaka 2007, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliridhiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuligawa shamba hilo sehemu mbili zenye ukubwa wa hekta 22,000 na 6200 kila moja ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa imebakiwa na hekta 6200 na hekta 22,000 zimechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maendeleo mengine chini ya uwekezaji wa ubia na kampuni ya kigeni.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada mbali mbali zilizochukuliwa na Serikali katika eneo la shamba hilo lililobakishwa, Kamati imebaini changamoto mbali mbali katika shamba hilo ikiwemo baadhi ya maeneo ya shamba hilo kuvamiwa na wananchi kwa ujenzi, malishio ya wanyama na kilimo. Aidha, Licha ya juhudi za Wizara za kuomba hatimiliki ya eneo hilo, hadi Kamati ilipolitembelea shamba hilo (tarehe 17/12/2014), hatimiliki ya shamba hilo ilikuwa bado haijapatikana.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto zote hizo Kamati inaishauri Wizara pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla kuendeelea kukaa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupata njia muafaka ya kuzitatua changamoto za shamba hilo la Makurunge ikiwa ni pamoja na kufanikisha kupatikana kwa hatimiliki ya shamba hilo.

Aidha, kwa kuwa shamba hilo lina maeneo tofauti likiwemo eneo la ufukweni kuna haja kwa Serikali kuzingatia kwa makini matumizi ya shamba hilo ili matumizi hayo yalingane na maumbile halisi ya eneo hilo na hatimae kuweza kutoa tija kubwa zaidi kwa Serikali na kwa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO, KIZIMBANI

Mhe. Spika, Pamoja na ufinyu wa bajeti unaoikabili taasisi hii, Kamati inashangazwa sana kuona kuwa taasisi hii imefanywa kama kijitengo tu cha Wizara wakati taasisi hii imepewa nguvu na mamlaka ya kisheria ya kutekeleza majukumu yake. Kamati imegundua kuwa tangu mwaka 2012 ilipopitishwa sheria ya kuanzisha taasisi hii, taasisi hii imekuwa ikifanyakazi bila ya kuwa na Kanuni wala Baraza lake ambalo limetajwa katika sheria hiyo. Hali ambayo inaifanya taasisi hii kufanya kazi zake katika mazingira magumu kiutendaji na kifedha.

Mhe. Spika, kutokana mapungufu hayo Kamati inaitaka Wizara kukamilisha Kanuni za Sheria ya Utafiti wa Kilimo ili Taasisi hii ya Utafiti wa Kilimo iwe na nguvu za kuweza kufanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu za sheria. Sambamba na hilo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Matangatuani, Pemba Kamati inaitaka Wizara kufanya kila jitihada ili kuwezesha upatikanaiji wa Tsh. millioni 15 zinazohitajika kwa ajili ya kukamilisha utafiti wa miche ya mikarafuu kutokana na umuhimu mkubwa wa utafiti huo katika uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na maeneo hayo niliyoyaeleza, Kamati pia iligundua changamoto kadhaa katika maeneo mbali mbali yakiwemo ya Idara ya Umwagiliaji Maji na Idara ya Misitu na Maliasili

Zisizorejesheka na kutoa maoni na maagizo yanayaakisi maeneo hayo kama inavyoonekana katika Ripoti ya Kamati hii.

WIZARA YA FEDHA

Mhe. Spika, kama inavyofahamika kuwa Wizara hii ina majukumu makubwa katika nchi yakiwemo ya kusimamia Mapato ya Serikali yakijumuisha ya ndani na kutoka nje ya nchi, kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma, kusimamia Mali za Serikali pamoja na kusimamia Sekta ya Fedha nchini na mandeleo yake.

Mhe. Spika, ni miaka mingi sasa suala la upatikanaji wa mapato kutoka nje hasa misaada ya Washirika wa Maendeleo limekuwa likikabiliwa na changamoto kadhaa zinazopelekea upatikanaji wa misaada hiyo kutokuwa na uhakika. Kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015, upatikanaji wa misaada ya Washirika wa Maendeleo hasa misaada ya kibajeti (*GBS*) umekumbwa na dhuruba kubwa.

Mhe. Spika, Kamati ilistushwa kuona kuwa hadi mwezi wa Disemba, 2014 wakati Kamati ilipokuwa inapokea taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara hii kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2014, kwa kiasi kikubwa misaada ya kibajeti (*GBS*) kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa imesitishwa na wafadhili kutokana na sakata la Akaunti ya "*Tegeta Escrow*" lililotokea katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hali ambayo imepelekea mambo mengi hususan ya kiutendaji kuzorota.

Mhe. Spika, "Ndege mmoja aliye mkononi ni bora zaidi kuliko kumi walio kichakani". Hivyo basi, kutokana na mwenendo wa kusuasua kwa upatikanaji wa misaada hiyo ya Washirika wa Maendeleo, kuna haja kwa Serikali kuandaa mikakati madhabuti ya kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kupanga mipango na bajeti zetu kulingana na hali halisi ya mapato yatokanayo na vianzio vya ndani vya mapato.

Aidha, Serikali iweke mikakati imara ya kudhibiti kisawasawa mianya ya upotevu wa mapato, ibuni mikakati mipya ya kuongeza mapato pamoja na kuweka mikakati mahsusi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini ikiwemo bahari kuwekeza hapa nchini ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na viwanda vya samaki.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Kamati ilishuhudia kuwa jengo linalotumiwa na Ofisi ya Wizara ya Fedha, Pemba kwa sasa ni bovu na Kamati imebaini kuwa hata ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara hiyo ina nyufa zinazohatarisha usalama wa wafanyakazi wa ofisi hiyo. Aidha, Ofisi hiyo imekuwa inakosa baadhi ya kumbukumbu muhimu za kikazi zikiwemo za matumizi ya fedha za maendeleo za taasisi mbali mbali za Serikali zilizoko Pemba, pamoja na kumbukumbu za wastaafu kutoka Pemba waliopewa kiinua mgongo.

Mhe. Spika, Kamati pia imegundua kuwepo kwa mgongano wa kimuundo baina ya Ofisi ya Wizara ya Fedha, Pemba na Wizara nyengine kwa Pemba ambapo Ofisi hiyo imezigawa sehemu zake na kuziita kuwa Divisheni wakati Wizara nyengine kwa Pemba zimegawa sehemu zao na kuziita kuwa ni Idara kama vile zilivyo kwa Unguja.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaitaka Wizara ichukue hatua za haraka za kuzitatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja tatizo la ubovu wa jengo linalotumiwa na Wizara kwa Pemba kwa kuwa jengo hilo linahatarisha maisha ya wafanyakazi wa ofisi hiyo.

Aidha, Kuna haja kwa Wizara kuweka mfumo mzuri zaidi wa kuiunganisha Ofisi ya Wizara iliyopo Pemba ili kumbukumbu muhimu za kikazi zikiwemo za matumizi ya fedha za maendeleo za taasisi za Serikali zilizopo Pemba pamoja na kumbukumbu za wastaafu waliopewa kiinua mgongo ziweze kupatikana katika Ofisi hiyo.

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI (*ZIPA*)

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kushajiisha wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza nchini pamoja kuwasaidia wawekezaji kufikia malengo yao ya uwekezaji.

Mhe. Spika, Uvamizi katika baadhi ya maeneo huru ya Uwekezaji, Fumba unaofanywa na wananchi kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kuishi unaonekana kuwa ni changamoto sugu inayoikabili Mamlaka hii. Hivyo, Kamati inaona bado kuna haja kwa Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) kuzidisha kasi ya utoaji wa elimu kwa wananchi, viongozi na wawekezaji wenyewe juu ya taratibu za Serikali katika ardhi ya wawekezaji.

Aidha, Kamati inaitaka Mamlaka iharakishe juhudi zake za kukamilisha miundombinu mbali mbali katika maeneo huru ya uwekezaji ikiwemo miundombinu ya barabara.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Shirika la Bima lilitayarisha mapendekezo ya Mishahara mipya pamoja na muundo mpya wa Utumishi wa Shirika hilo *(Scheme of Services)* ambapo fedha kwa ajili ya utekelezaji wake tayari zimeshatengwa na shirika. Hata hivyo, Kamati haikufurahishwa baada ya kupata taarifa kuwa barua iliyopelekwa Kamisheni ya Umma mwezi wa Oktoba, 2014 inayohusu dhamira ya marekebisho hayo imejibiwa mwezi Januari, 2015 kwa kueleza tu kuwa ombi hilo linashughulikiwa.

Mhe. Spika, Mwenendo huu wa Kamisheni kuwa ni kikwazo katika maslahi ya watumishi wa Umma umesababisha baadhi ya wataalamu kukimbia kufanya kazi katika Shirika hilo la Bima na badala yake kujiunga na mashirika mengine yenye maslahi mazuri zaidi.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utumishi wa Umma isiwe kikwazo cha kukwamisha maslahi na maendeleo ya watumishi wa Umma na kudhorotesha wataalamu wetu. Kama tatizo ni sheria yenyewe ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake basi zirekebishwe, kama kasoro zipo katika utekelezaji wa Sheria hiyo basi kasoro hizo zichukuliwe hatua na kama tatizo ni Kamisheni yenyewe ya Utumishi ya Umma basi Kamisheni hiyo ivunjwe na iundwe upya, lakini haiwezekani hata kidogo kuendelea kuwa na taasisi ambayo kila kukicha inaibebesha Serikali mzigo wa lawama na kuwaacha baadhi ya watumishi wa Taasisi za Serikali wakisononeka na kunyong'onyea huku baadhi ya taasisi hizo zikikimbiwa na wataalamu wake.

Mhe. Spika, Kuna haja kwa Serikali kuzirekebisha kasoro zilizopo ili Mashirika na Taasisi za Serikali zinazojiendesha wenyewe kifedha, zisiwekewe vikwazo pindi zinapotaka kuongeza maslahi ya wafanyakazi wake kwani taasisi hizo maalum zinazozalisha fedha zina umuhimu wa pekee hapa nchini na zinafanya kazi katika ushindani mkubwa wa kimaslahi na hivyo zinahitaji fedha za kutosha kuwalipa wafanyakazi wake ili waweze kubakia katika taasisi hizo na kuongeza huduma za kuzalisha mapato zaidi.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (*PBZ*)

Kamati ilipata nafasi ya kupata taarifa za utekelezaji za Benki ya Watu wa Zanzibar katika tawi lake la Chake Chake (Pemba) pamoja na kukutana na Bodi ya Benki hiyo hapo Mpirani, Unguja.

Suala la PBZ kuongezewa mtaji ni jambo lililo katika mjadala mzito baina ya Benki hiyo na mmiliki wake ambae ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, kwa kuwa suala hilo limekuwa likijadiliwa kwa muda mrefu, Kamati inaona kuwa kuna haja kwa *PBZ* pamoja na Wizara kuangalia kwa kina hoja za kitaalamu zitakazoiwezesha *PBZ* kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kibiashara, kitaaluma na kiteknolojia.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Kamati inaipongeza sana *ZRB* kwa kazi nzuri ya kuhakikisha inafikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kama inavyopangiwa kwani hadi kufikia mwezi Januari 2015, Bodi hiyo ilikuwa imeshakusanya mapato ya asilimia 57 ya makadirio, Hata hivyo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaamini kuwa mapato mengi zaidi yanaweza kupatikana iwapo Bodi hii itaongeza juhudi za kubuni mikakati mengine ya muda mrefu ya ukusanyaji wa mapato. Pamoja kuongeza juhudi za kuweza kutambua mianya ya kukwepa kulipa kodi ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali zinazotokana na mapato ya kodi mbali mbali.

MAMLAKA YA MAPATO (*TRA*) OFISI YA ZANZIBAR

Pamoja na changamoto kadhaa za masuala ya kodi zinazoikabili Mamlaka ya Mapato *TRA* kwa upande wa Zanzibar, Kamati imegundua changamoto ya kimuundo ambayo inaishushia hadhi Ofisi ya *TRA*, Zanzibar

Muundo wa *TRA* Zanzibar unaonesha kuwa *TRA* Zanzibar inaongozwa na Naibu Kamishna ambae anawajibika moja kwa moja kwa Kamishna wa Forodha Tanzania. Hali hii inaonesha kuwa Naibu Kamishna wa *TRA* Zanzibar yupo katika ngazi ya nne katika mtiririko wa ngazi za uongozi wa *TRA* ambazo ni Kamishna Mkuu wa *TRA,* Naibu Kamshna Mkuu wa *TRA*, Makamishna wa *TRA* na Naibu Kamishna wa *TRA*.

Kamati inaona kuwa hii ni kasoro kubwa na hivyo inaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ishirikiane na *TRA* Makao Makuu ili kasoro hii ya kumfanya Naibu Kamishna wa *TRA* Zanzibar kuwa katika ngazi ya nne katika ngazi za uongozi wa *TRA* anaewajibika kwa Kamishna wa Forodha iweze kurekebishwa.

Aidha, Kamati inaitaka *TRA* kushirikiana na *ZRB* ili kuandaa mkutano wa pamoja utakao wajumuisha wadau mbali mbali wa kulipa kodi ili kujadili masuala muhimu yakiwemo ya ulipaji wa ushuru wa bidhaa hasa magari, misamaha ya kodi, udhibiti wa mianya ya ukwepaji kodi na mengine kama hayo.

WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO

Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko ina jukumu la kusimamia masuala ya biashara na maendeleo ya viwanda nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunakuwa na masoko ya uhakika ya bidhaa zetu ndani na nje ya nchi yetu. Majukumu haya sio madogo, ni makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa ukizingatia kuwa sekta hii ya biashara na viwanda ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya uchumi popote pale duniani.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Idara hii ina dhamana ya kusimamia masuala ya biashara na kukuza masoko. Katika kutekeleza wajibu wake, Idara hii pia ina wajibu wa kuzitafutia masoko endelevu ya ndani na nje bidhaa zinazozalishwa nchini na kuitangaza Zanzibar katika masoko ya ndani na nje.

Mhe. Spika, bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaoingiza biashara zilizopigwa marufuku hapa nchini. Aidha, katika miaka ya hivi karibuni kumejitokeza tofauti kubwa ya bei za bidhaa mbali mbali kati ya Unguja na Pemba kwa bidhaa za Pemba kuuzwa kwa bei ghali zaidi. Hivyo, kuna haja kwa Wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika kusimama kidete katika kuhakikisha kuwa chanagomto hizo zinachukuliwa hatua ili wananchi wetu wasizidi kuumia kutokana na athari za changamoto hizo.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (*ZSTC*)

Kamati inalipongeza sana Shirika hili la *ZSTC* kwa jitihada kubwa linazochukuwa katika kuhakikisha kuwa biashara zinazofanywa na Shirika hili zinaimarika na hatimae kupata tija na faida kubwa zaidi kwa maslahi ya nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inalihimiza Shirika hili kuendelea na juhudi zake za kufanya utafiti katika maeneo mbali mbali yakiwemo soko la karafuu, miche ya mikarafuu yenyewe pamoja na kutoa elimu kwa wakulima wa karafuu juu ya namna bora zaidi ya kuzishughulikia karafuu ili karafuu zinazozalishwa Zanzibar ziendelee kuwa na ubora unaokubalika Kimataifa.

TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR

Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Na. 1 ya Zanzibar ya mwaka 2011. Taasisi hii imeanza kazi zake rasmi September, 2012 ikiwa na jukumu la kuweka viwango na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma nchini, iwe zinazozalishwa au kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi. Hali hiyo inatarajiwa kuwa ni chachu ya maendeleo, kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini pamoja na kulinda afya na usalama kwa watumiaji wa bidhaa na huduma pamoja na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu.

Taasisi ya Viwango (*ZBS*) ni Taasisi inayohitaji fedha nyingi ili kukamilisha ipasavyo malengo yake. Hivyo, kuna haja kwa Serikali kuongeza kiwango na kasi ya uingizaji wa fedha kwa taasisi hii ili iweze kuongeza kasi ya ufanisi katika utendaji wake.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara hizo tatu zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na taasisi zao kwa juhudi wanazochukua katika utekelezaji wa kazi zao. Kamati pia inapenda kutoa shukurani tena kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii pamoja na wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa usikilizaji mzuri wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati inatoa wito kwa Serikali kutekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na Kamati ili kuongeza ufanisi katika Wizara hizo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana umeniona kwa kuwa nina kawaida ya kuleta labda umeona sijaleta ukaona unipe nafasi hii. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa upendeleo mzuri na Mwenyezi Mungu akujaalie kila la kheri na akupe afya njema.

Mhe. Spika, mimi naingia ukurasa huu wa biashara. Kwa kweli nimeingia ukurasa huu katika maagizo ya Kamati Namba 6. Hapa nina masikitiko makubwa sana. Siku moja Mheshimiwa wangu Muhammedraza alisema kuna wawekezaji wengine wakitaka kupewa kuekezwa waangaliwe kuwa wana uwezo au hawana uwezo halafu baadae ndio tuwape miradi.

Mhe. Spika, kusema ukweli Kiwanda cha Sukari hakijapata muwekezaji, hilo tusifiche na tuseme wazi. Historia hii mimi naijua ya Kiwanda cha Sukari. Siku zote hapa mimi hukaa ubavuni na Mzee Ali kwa kutafuta kumbukumbu ya historia ya jambo. Muwekezaji huyu alipewa kiwanda kwa sababu ya jambo. Mwanzo aliingia katika kuwekeza Zanzibar alikuwa na majengo Matemwe kwa kutaka kujenga Hoteli.

Mhe. Spika, *lease* nnayo, sisemi kwa kubahatisha. Alinyang'anywa *lease* ile na ikafutwa na wakati alikuwa tayari majengo ameshajenga makubwa bado kupiga bati tu. Eneo hilo nimekwenda nikaliona nimekwenda kuonyeshwa na nikaliona. Alinambia nimtetee kanyang'anywa *lease y*ake bila ya sababu yoyote, hakuwa na indhari wala hakuna wa nini.

Lakini tumezunguka kwa mlango mwengine tumempa Kiwanda. Hapa kapewa hidaya, nasema kapewa hidaya au kapewa kifutio cha kufuta jasho. Hatari yake ndio hii inayotuka mpaka leo mradi ule Serikali bado haijapata tija. Ndio ukweli tuseme.

Mhe. Spika, lakini pia kuna masikitiko makubwa sana ya wafanyakazi ndani ya hicho kiwanda chenyewe. Lakini mimi nataka niseme kwa kuwasomesha watu kidogo. Kuna watu wengi hawatufahamu kama wawekezaji hao na watu wengine, sisi nini kazi yetu, Mhe. Spika, naomba niwaelimishe.

Mhe. Spika, mimi mle nina wananchi wangu wengi sana wanafanya kazi katika kiwanda kile. Wanapofukuzwa na kunyanyaswa mimi ndio wao, mimi ndio Mwakilishi wao, ndio mtetezi wao, mimi ndio mtafutaji haki zao wale. Kwa sababu kuna wengine hawajui sheria, sisi tunatakiwa tuwasaidie sheria. Sasa mtu anapotoka mle ndani kwenye kiwanda akasema kwamba huyu Mwakilishi anaingilia kutaka nini. Mimi namuona ovyo kweli, kwa kweli hafahamu.

Mhe. Spika, kuna wafanyakazi 40, wamefukuzwa kazi katika kiwanda cha Sukari hichi, wakati kuna wafanyakazi wana miaka miwili, mitatu, minne, mitano hadi sita, leo tunawatetea wapewe nyumba 150. Kamati inatetea na ndio wajibu wetu tumtetee, lakini na wajibu wetu tumseme, sasa wafahamu hivyo. Leo tunamtetea apewe nyumba zake 150 na nitaiuliza Serikali kwa nini mpaka leo hamjampa nyumba zake. Kwa sababu gani? Mtwambie sababu. Lakini na mimi hapo hapo nitasema kuwa hawatendei haki wafanyakazi. Sikubaliani naye miye kabisa.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi namuomba sana huyu kijana huyu kaka jina lake anaitwa Bashiru, anifahamu mimi nini ninachokitetea na wala hilo sitokubaliana nalo. Maana yake yeye alifika alisema jeuri anawambia wale, mmekwenda kumchukua kimwakilishi chenu hata aje Rais hapa, hamtofanikiwa.

Oh! Nilishangaa sana nikasame *Alhamdulillahi* ama kweli Mswahili unakwenda kuwakandamiza Waswahili wenzako, wewe hujui kama na wewe umealikwa tu pale, kesho shughuli ikisha na wewe unafukuzwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa, naomba sana.

Mheshimiwa wa Wizara husika, unajua siku moja nilikwambia jambo kwamba kule kuna wizi na unaibiwa waya. Mheshimiwa ulikwenda mara moja, wananchi wakanambia, Mheshimiwa keshakuja Waziri kufuatilia na waya keshauzuia. Ulifanya jambo la ujasiri kweli. Sasa na hili nakwambia Mheshimiwa wananchi wanadhalilishwa vibaya sana wafanyakazi wa kiwanda cha Sukari. Hawakupewa mikataba, inasikitisha sana.

Wapo katika Ushauri wa Kitengo cha Kamishna *Labour* wanakwenda wakirudi tu. Ni haki yao ipo *open* kabisa ya kupewa, lakini bado wanakwenda wakirudi. Lakini nawashukuru na wao kitengo kile kuwa bado kinajaribu kubembeleza kwa mujibu wa sheria. Mimi siingilii muhimili husika, sio mgonjwa na sio pumba mimi. Kama sheria niziingilie hilo haiwezekani lakini ni wajibu kuuliza na kufuatilia.

Mhe. Spika, wananchi wetu wanadhalilishwa, ardhi yetu wenyewe wanafanywa watumwa ambao wanaokiukwa kwa mujibu wa sheria. Inasikitisha sana, Mhe. Waziri nakuomba sana mara moja hili suala lifuatilieni ili hii haki itendeke vizuri kwa mujibu wa sheria.

Kila siku wanalima wanatia madawa, mihogo inakufa, sumu tupu, bila ya kutafuta waumini ambao wenye sifa kwa mambo ya kemikali, wao wanafanya wanavyotaka wao. Naomba sana, naomba sana sana sana, lazima uwe na mapenzi na wafanyakazi wako, sio wewe Mswahili unakuwa unawadhalilisha kwa kumuokoa bwana mkubwa, doo! pole sana.

Mhe. Spika, kwa kweli hili suala linasikitisha sana. Nione mimi hapa kwenye biashara, haya yote leo nitasema mazuri, lakini kwa hili nasema sio zuri. Kwa sababu inasikitisha sana ni wananchi wetu, ni

wazalendo wetu kwa leo wananyanyaswa kwenye haki yao ya Kiwanda cha Sukari. Hiyo ni *massage* siku hiyo ya bajeti ndio nitakuja kumwaga vitu zaidi, leo naomba kidogo nisaidie hapo tu.

Mhe. Spika, niende katika kilimo. Mara nyingi sana sisi labda niseme Waheshimiwa Mawaziri sisi Wawakilishi watafutaji kuleta maendeleo katika nchi yetu. Unajua mara nyingi sisi tunauchungu sana na nchi yetu, hasa tukiona nje wenzetu wanaendelea sisi tunaumia ndani ya roho, bora sasa usitutoe nje tuwache tukae humu humu ndani wala usitupeleke nje, haina maana, wambie *UNDP* wachukue pesa zao bora.

Kwa sababu unapotutoa nje tunayapata mambo mazuri ya kule nje, tukiyaleta ndani inakuwa Mheshimiwa hayafanyiki kazi, hilo ni suala linasikitisha sana. Unapompeleka mtu nje anaanza urafiki, kila mtu pale anatoa *introduction* yake mimi hivi, mimi nina kiwanda fulani, mimi nina uwezo wa kuleta jambo fulani. Na ukiingia kwenye mitandao inakuonesha hasa kuna watu ambao wanataka kuekeza katika nchi za kiafrika. Kwa hivyo, hili jambo kwa kweli linasikitisha sana.

Mhe. Spika, tumepata muekezaji hapa nimeona katika ripoti kuna mambo mengi sana; kuna mambo ya matrekta na mbolea, yote hiyo tunajitahidi katika ulimaji wa mpunga. Lakini sasa kuna muekezaji tayari, lakini la kusikitisha tunaposema kuwa hatuna uchungu na nchi mpaka leo tunampiga danedane, sababu zipi, haieleweki. Muekezaji anataka sasa kutulisha mpunga wa Zanzibar, amefanya *research* yake, tumempeleka kwenye mabonde, amekaa na wakulima, wamekubaliana vizuri na ingekuwa kama Serikali yetu iko *faster,* basi sasa hivi matrekta yangekuwa yemeshakuja.

Maana yake tunataka tupelekwe tukaangalie matrekta gani ambayo yataweza kusaidia Serikali. Lakini kwa kuwa bado tuna kawaida ya ku-*delay* katika upokeaji wa miradi. tuna kawaida tusikatae, tuna kawaida sana.

Kwa sababu unajua mimi kitu kinachonishangaza tatizo liko wapi, wewe hutakiwi utoe pesa wakati huyu mtu anakuja na mapesa yake, wewe unatoa nafasi ya kumwambia nenda akafanye kazi. Sasa ni kitu gani kinachotushughulisha mpaka leo anazungushwa. Tunashindwa kupata mchele wa Zanzibar, ameshafanya *researches* zake zote, lakini kukaa pamoja na watu wa| wizara wahusika wakubwa mnaona tabu, hamuwezi wacheni kazi jamani. Mnatushughulisha na mnawapa watu njaa, wakulima sasa hivi wamekaa. Naomba sana lazima hili suala litizamwe kwa hali ya kina kabisa. Kwa kweli tuna-*delay* katika masuala ya kuwapokea wawekezaji.

Mhe. Spika, kulikuwa na bonde ambalo limefanyiwa *research* ya umwagiliaji mpunga Pangeni na Kilombero imeishia wapi *research* yake. Naomba sana hili lijaribiwe kusaidiwa, lakini kifungu cha 4 basi tunashindwa hata *overrall* kuwasaidia maafisa tunashindwa. Naomba sana tujitahidi sana, hapo mimi naona tabu sana na kila siku tunaambiwa bajeti finyu, haya *Inshaallah* salama.

Mhe. Spika, lakini kuna taarifa kama ni kweli au uongo nambieni na ndio maana kulikuwa na muekezaji wa kuweka Kiwanda cha Sukari Pemba na hata Rais alisema *Alhamdulillah*, sasa sijui muekezaji huu ilikuwaje hata akaondoka na akarudi Dar es Salaam kutaka kuekeza huko.

Lakini yuko mpaka leo ana hamu ya kutaka kuekeza Kiwanda cha Sukari Pemba, ingekuwa huyu karuhusika huyu wa sasa hivi asingeleta jeuri hiyo, watu wengi wangekwenda huko kwa sababu kila mtu ana mvuto wake wa utendaji wake wa kazi. Sasa hilo Mhe. Waziri hebu naomba sana uje kunambia ili niweze kufahamu kabla kwenye bajeti nisije nikapiga buti kidogo.

Mhe. Spika, sitokuwa na mchango makubwa sana leo, niingie kwenye jungu kuu Wizara ya Fedha. Tatizo la kuwa na miradi mingi hapa Zanzibar na ndio maana tunakuwa na bajeti finyu hatujawa na fedha za kuweza kutosheleza. Namuomba sana Mhe. Waziri leo anisikilize vizuri sana, mimi si mchumi, lakini nina *experience* ndogo tu ambazo zinaweza zikatuletea tija kwa kuwa tuna uchumi ndani ya sekta zetu, lakini hawaangalii jambo gani ambalo litaweza kututilia uchumi. Unajua niseme mfano Mheshimiwa, nina watu wanataka kuleta kiwanda cha kutengeneza maziwa kwa kupitia kokwa

za fenesi, maziwa hayo ni *pure* mazuri haya *cholesterol,* ninaogopa sana kuwaondoa huko nikawaleta hapa wakati nishaona kuna miradi mengine mpaka sasa inapigwa danedane, inasikitisha sana.

Na sasa hivi tuna Sheria hii ya *PPP* hii, naomba sana watu wengine tunasema itakuwa ndio *delay* zaidi lakini ninamuomba *faster* kiongozi wangu dokta atufanyie haraka haraka hii miradi.

Mhe. Spika, niende mbio mbio, sasa hili ni suala ambalo kuwa kila tukiwa miradi mingi nchi hii ndio bajeti finyu inaondoka. Mheshimiwa na wawekezaji wengine wanataka kuleta yale majani ya karafuu yanatoa mafuta yale tena mazuri sana, hao wapo lakini tunashindwa kuwa-*organize* kuwaleta kutokana na ile tuliyosema utaratibu wake. Lakini kwa kupitia mlango wa sasa hivi wa Dr. Mwinyi hapa tutaweza kuwa-*convice* na kuweza kuwaleta ili waonane nao labda azungumze kuwaleta *faster*.

Mhe. Spika, haraka haraka niende na *ZSSF* kwanza hawa nikubaliane nao kwa sababu wanaifanya kazi vizuri katika kuokoa na kutafuta *funds* ambazo za wafanyakazi, lakini kuna tatizo moja hapa. Katika Ripoti ya Elimu tumeona jinsi gani watakaa na kuweza kukopesha wananfunzi. Ninamwambia Mheshimiwa na hawa waangalie jinsi gani ya kuweza kuwakopesha sasa hawa wafanyakazi.

Kwa kuwa ni muda mrefu wa siku nyingi ambazo hata kuja kupata haki yake, basi hapa angeonja utamu huu na wao wakaekewa mkopo wa kuweza kuwainua katika uwekezaji wa nyumba. Ningeomba sana hilo ili kuweza kutekelezwa zaidi.

Mhe. Spika, lakini niende *ZPA*. Utekelezaji wa *ZIPA* unajitahidi sana, inapotoa miradi ikaelekeza kwa mradi huu unakubalika, lakini kuna chombo ambacho mkikipelekea huko aidha ni Baraza la Mapinduzi au wapi unakuwa mradi ule unapigwa na chini. Sasa imekuwa hapa inakuwa ni vichekecho sana. Lakini kwa kuwa mradi huu wa *PPP* na katika *PPP* pengine na yeye atakuwa ni mjumbe kutokana na sheria inavyoelekeza. Ningemuomba sana Mheshimiwa ili ajitahidi katika ile hali halisi ya kuweza kufanikisha lengo linalotakiwa.

Mhe. Spika, nina mengi sana, niwapongeze sana *ZRB* kwa mkusanyo wao wa kila mwezi tunaambiwa ni bilioni thalathini na, kama ni kweli au uongo naomba sana wazidishe kasi.

Mhe. Spika, hili jambo ni zuri sana kwa kuwa mapato yetu ya ndani yanafika katika mabilioni. Kwa hivyo, naomba sana na muelekeo wa kuweza kupata mishahara inayopanda itakuwa ni vizuri sana. Lakini kwa kumalizia Mheshimiwa tukifanya mchezo maofisa wetu hasa katika kilimo, unakuta watu wana ma-*degrees* lakini mishahara bado ingali midogo. Naomba sana Mhe. Waziri wahusika hawa tuwapandishie mishahara kutokana na ile hali halisi ilivyo, kwa kweli mishahara Mheshimiwa hata kuisema unaona tabu na kulinganisha mishahara ya *degrees* na sehemu nyengine inakuwepo.

Mhe. Spika, naomba niunge mkono Ripoti ya Kamati. Ahsante sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa pumzi mpaka kwa wakati huu, vile vile, nichukuwe nafasi kukushukuru binafsi kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia.

Mhe. Spika, nimefarijika sana na wizara hizi zilizotoa taarifa pamoja na Mwenyekiti wa Kamati. Mimi nichukuwe nafasi kwa kweli kuwashukuru Mawaziri wote wa Fedha, Kilimo, Biashara, kwa usikivu na kufahamu kazi pamoja na watendaji wake wote waliokuwa nao nasema ni kazi ambayo inataka kuendelezwa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nashauri vitu viwili, Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti amesoma ripoti, sasa Mhe. Spika, *it is very serious* na hili jambo tulitafakari.

Mhe. Spika, ripoti imezungumza kwamba wenzetu wa *EU* na wahisani wetu walikatisha misaada kwa Tanzania na kuathirika vile vile Zanzibar kutokana na *Account* ya *ESCROW* na kwa kweli Mhe.

Spika, Zanzibar tumeathirika kibajeti. Sasa sijui Mhe. Waziri wa Fedha ni makini sana na msikivu ana hekma na busara, sisi sote tunamueheshimu, mimi binafsi ninamuheshimu sana pamoja na wenzake.

Mhe.Spika, lakini kama nilivyosema tuna kumbukumbu nyingi, hujafa hujaumbika. Hii *ESCROW* kwanza haipo kwenye Muungano, maana Wizara ya Nishati, la kwanza. La pili, hawa wanafahamika waliochota pesa, sasa mimi nina kumbukumbu na ushahidi mwaka 1996/1997/1998 Zanzibar tuliwekea vikwazo, ninazo kumbukumbu mpaka Bungeni, Waziri wa Fedha wa Tanzania Bara alisema, namnukuu;

"Kwamba tumekupuuzieni kukupeni msaada Zanzibar kwa sababu mmeekewa vikwazo wahisani walitwambia tusikupeni pesa".

Sasa *Alhamdulillahi* hujafa hujaumbika na mkuki kwa nguruwe kwa binaadamu mchungu, leo tupo wenzetu Tanzania Bara walichofanya ufisadi huo wa kuingiziana fedha katika *Accounts,* ilikuwa sio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa tuwaambie wahisani kwamba sisi hakuna Mzanzibari anayehusika na wala hili suala si la Muungano, hii iko wazi Mhe. Spika, hii ripoti imezungumza hapa na mimi nimekwenda kwenye ripoti.

Sasa tunafanyaje kwa sababu Mhe. Spika, sisi sote hapa Wawakilishi na tumekuja *with people power,* mimi nimekuja na kiti hiki kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi hapa.

Lakini Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kutoa ushauri kwa Waziri wa Fedha, sisi kama Wawakilishi wa wananchi ahadi nyingi zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa bajeti wa mwaka uliopita, Waziri wa Fedha mwenyewe alishuhudia changamoto alizozipata kwa Wawakilishi, viatu vilikuwa vingi na buti zilikuwa nyingi.

Sasa Mhe. Spika, tunakuja tena hapa tushaathirika kibajetim maana bajeti imevurugika, tunachokipata tunakitumia, kuna ahadi ambazo zimetolewa na Serikali katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, asilimia 50 hatujaweza kuitekeleza, tunakwenda kuiandaa tena bajeti nyengine.

Mimi Mhe. Spika, ningelimshauri Waziri wa Fedha kabisa kwamba kutokana na maathiriko haya tuliyoyapata, Serikali yenyewe ingelikaa chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa; kwa maana kwamba Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, hii bajeti ambayo haijakamilika ikarejewa tena ili ikatekelezwa vile vilio vya wananchi na wawakilishi waliotoa ahadi.

Kwa sababu Mhe. Spika, Serikali imetoa ahadi nyingi na sisi tukasema itatekelezwam tunakuja tena bajeti hii ya Kamati inasema kwamba Zanzibar tumekosa misaada kwa watu wachache tu wenye kushiba matumbo yao, yaani nchi nzima tumeathirika na hawa watu wamejiuzulu hawakuambiwa pesa warejeshe *and then* tunaumia sisi sote, *at the end of the loser, we are the losers*.

Sasa Mhe. Spika, mimi ninamuheshimu sana lakini katika vitu hivyo tutapokuja tena kwenye bajeti hapa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali, Waziri wa Fedha alisimama kwa niaba ya baadhi ya mawizara kama Afya, Elimu, Kilimo, Wawakilishi kila mmoja walipata ahadi na kama huu ni mtihani ushafika.

Sasa Mhe. Spika, tunachotaka kwenda kuna vitu vingi ambavyo havijaweza kukamilika, kuandaa bajeti nyengine halafu sisi tukaja kwa niaba ya wananchi Mhe. Spika, hili suala litakuwa gumu sana, mimi ningelipenda kushauri namuheshimu sana Waziri kwa sababu bajeti kama hivi imeathirika. Mawaziri wetu waliosema hali yao tulikuwa tunashuhudia juzi Naibu Waziri wa Elimu anasema katika bilioni kama arubaini sikosei, lakini hata hiyo 40% haijafika, kuna pesa za watoto kwenda kuwasomesha ilikuwa *something about* 1.4 *billion,* lakini wamepata milioni mia saba. Sasa *that you can't blame* Serikali au Waziri wa Fedha.

Kwa hivyo, Waziri wa Fedha anapata kile kinachoingia kwenye mapato. Lakini kutokana na bajeti hali hii ilibidi ina maana sisi tumejifunga mkanda kwa watu wachache, ilikuwa sisi tutoke tukawaambie sasa, maana yake hawa wenzetu walisema hivyo *openly* kwamba bwana nyinyi Zanzibar tumeambiwa tusikupeni msaada kwa sababu mna matatizo. Leo kilichofanywa hakimo ndani ya Muungano ni taasisi tu.

Mhe. Spika, sasa ningependa kutoa ushauri mimi nazipongeza Wizara zote; ninaipongeza Wizara ya Kilimo Mhe. Waziri Mwinyihaji Makame kwa niaba ya Waziri, Waziri wa Biashara Nassor Mazrui na Waziri wa Fedha ni mawaziri wasikivu. Mhe. Nassor Mazrui nimekuwa nae, tumekuwa nae na tutaendelea kuwa nae kwa sababu ya jitihada zake, Waziri wa Fedha na mawaziri wote.

Lakini kama hakuna Mheshimiwa hivi vitu havitekelezeki, ripoti imezungumza mambo yote haya ya Kamati na sisi tunakwenda kwenye Kamati. Mimi nimeingia kwenye Kamati nzima. Kwa hivyo, ukisema kilimo tatizo itakuwa ni fedha kuingiziwa, ukisema biashara, pesa kuingiziwa, ukisema elimu, pesa kuingiziwa na ukisema afya,...maana yake kama juzi afya hali inavyokuwa. Kwa sababu siku nyengine pesa hawakuingiziwa.

Sasa Mhe. Spika, kutokana na muda mimi nashauri kwa heshima zote namstahi sana Mhe. Waziri wa Fedha tena sana na nitaendelea kumstahi kama kaka yangu Mhe. Omar Yussuf kama hajafanya marekebisho ya bajeti hii, tunakuja tena Mwenyezi Mungu akitujaalia tukiwa uhai na uzima *Inshaallah* kwa uwezo wake, maana tunaringa na pumzi, tukifika tena Wawakilishi tuliokuwepo, maaana ya kila mmoja mimi mwakilishi wa Uzini na mambo yangu nimeahidiwa kwa niaba ya wananchi. Kuna mwakilishi wa Wawi Said na yeye kaahidiwa, kwa hivyo, tuko pamoja maana rafiki yangu maalim Said eee, *we are together*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachotaka kushauri kwamba nazipongeza Kamati zote na nazipongeza wizara zote, lakini Mhe.Waziri kama hajafanya utaratibu huu wa bajeti ambayo haikutekelezwa, *in fact,* Mhe. Waziri tutaumia na tutaathirika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilichoomba kumwambia Waziri wa Fedha iwe historia, kaka yangu, iwe historia kwamba bajeti hii irejewe. Kwa sababu kuandaa bajeti nyengine na bajeti ambayo haikuweza kutekelezwa ina maana tunarejea tena na Mhe. Spika, kwa sababu Baraza hili ni kubwa sana la kihistoria, majukumu yote tuliyosimama hapa tunazungumza kwa niaba ya wananchi, hatuzungumzi *personal issues.*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilichokuwa nacho naziunga mkoni wizara hizo na Kamati hizo zote na hizo Kamati zote za Waziri wa Fedha asilimia 120 lakini Mheshimiwa tatizo lipo.

La mwisho, Mhe. Spika, mimi ningelimuomba Waziri wa Fedha kwenye Kamati hii tunaambiwa Naibu Kamishna wa Zanzibar mtu wa nne. Mhe. Spika, unajua funika kombo mwanaharamu apite. Lakini *just* Kamati inazungumza kwamba Naibu Kamishna ni wanne, tumekaa hapa tuna Katiba yetu, tuna bendera yetu, tuna Rais wetu na tuna wimbo wetu *and then* mtu wa nne! Tunaambiwa kwenye Kamati, sisemi mimi kwenye Kamati imesema hayo, sifaham.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa sababu ya muda, tukakimbilie *ishaa* kusali. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Raza, nakushukuru sana kwa mchango wako huo. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru wote kwa jumla kwa kazi nzuri tuliyoshirikiana nayo hadi kufikia muda huu. Na sasa basi niahirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 25 Machi, 2015 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:39 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 25/03/2015 saa 3:00 asubuhi)